**2 JUNI, 2022**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Thelathini na Sita – Tarehe 2 Juni, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Ahsante, Katibu!

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**2 JUNI, 2022**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 316

**Hitaji la Kituo cha Afya Kata ya Kwihancha – Tarime**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza:-

Je, ni lini Kata ya Kwihancha itapata Kituo cha Afya na ni lini huduma za afya zitaimarishwa katika Hospitali ya Nyamwaga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022, imetenga Shilingi Milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wa Nje *(OPD)* na Maabara katika kituo cha afya. Fedha hiyo itapelekwa kabla ya tarehe 30 Juni, 2022. Aidha katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga shilingi Milioni 400 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, huduma za afya katika Hospitali ya Nyamwaga zinaendelea kuimarika ambapo Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022, imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa hospitali hiyo. Ujenzi wa wodi mbili za wanaume na wanawake umekamilika na ujenzi wa majengo ya maabara, wodi ya watoto na jengo la kuhifadhia dawa upo katika hatua za umaliziaji. Aidha, huduma zinaendelea kutolewa ikiwemo huduma za uzazi na upasuaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza ni kwamba, wakati wa bajeti tarehe 26 Machi, 2022 kwenye Kamati ya TAMISEMI, waliahidi wataalam kwamba watapeleka fedha hizi tarehe 30 Machi. Leo Waziri anasema tarehe 30 Mwezi Juni, maana yake miezi mitatu baadaye. Kama hii kauli ya mwanzo iliahidi Kamati ya Fedha, fedha haijaenda mpaka leo tunavyozungumza, tarehe 30 Juni, fedha itaenda kweli?

**SPIKA:** Swali Mheshimiwa Mwita.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Swali la kwanza, fedha hiyo inaenda lini Ili iweze kujenga kituo cha afya pale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; hapo Hospitali ya Mwaga ilikuwa ni zahanati kama kituo cha afya, sasa ni Hospitali ya Halmashauri mpya, hakuna mgao wa dawa pale, lakini hizi huduma ninazozizungumza wodi ya akinamama haijakamilika, wodi ya watoto haijakamilika,

wodi ya wanaume haijakamilika, pharmacy haijakamilika, fedha ipo milioni 78 kwenye mgodi wa North Mara, Mheshimiwa Waziri wa Madini aliagiza kwamba ndani ya siku 14 fedha iende haijaenda, Waziri wa TAMISEMI aliagiza fedha haijaenda...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Waitara, ngoja kwanza. Jibu la msingi la Waziri, wewe kwa hilo swali lako la pili unalotaka kuuliza ni kwamba, hili jibu lake la msingi halitoi uhalisi wa kilichoko huko ndiyo unachojaribu kusema? Simama.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli.

**SPIKA:** Kwa hiyo, hakuna hizo wodi mbili zilizokamilika.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Hazijakamilika.

**SPIKA:** Basi hilo swali lako la nyongeza la kwanza nitampa nafasi Mheshimiwa Waziri alijibu, hilo la pili unalosema hayo majibu hayako halisi Mheshimiwa Naibu Waziri atakapomaliza kujibu maswali hapa, nitampa nafasi aende akalifuatilie aniletee majibu hapa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tupe majibu ya hilo swali lake la nyongeza la kwanza, halafu swali lake la nyongeza la pili utaniletea majibu hapa, kwa sababu anasema jibu la msingi limesema kuna wodi ya wanawake na wanaume na yeye anasema hakuna hizo wodi. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Waitara, Mbunge wa Jimbo wa Tarime Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Tarime Vijijini walitakiwa kupeleka milioni 100 lakini hawakupeleka milioni 100 katika kata hii kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha afya tarehe 30 Machi na jana nimewasiliana na Mkurugenzi na Katibu Tawala wa Mkoa na watapeleka ndani ya mwezi huu kwa sababu walikuwa hawajapata makusanyo ya kutosha kupeleka fedha hiyo kwa mujibu wa vipaumbele ambavyo vilikuwa vimewekwa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Venant Daud Protas, swali la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Lutende, mwaka 2019 walipeleka shilingi bilioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya na jengo la OPD limekamilika. Palikuwa pana ongezeko la milioni 300 lakini kata hiyo haijapelekewa fedha hiyo. Je, ni lini watapeleka fedha hiyo ili tuweze kumaliza Kituo cha Afya cha Kata ya Lutende?

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais,– TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nnaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Jimbo la Igalula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kituo hiki kilipelekewa milioni 200 na kama ilivyo kwa vituo vyote ambavyo vilipelekewa milioni 200 au milioni 250, awamu inayofuata wanapewa milioni 300 au milioni 250 kukamilisha milioni 500 ili kukamilisha vituo vya afya. Kwa hiyo, fedha hiyo itapelekwa kwenye kituo hicho cha afya. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Miluwi iko umbali wa kilomita 80 kutoka Liwale Mjini ambako kuna hospitali ya wilaya na uhitaji wa kituo cha afya pale ni mkubwa sana na wananchi wameshaanza ujenzi wa kituo cha afya pale. Je, Serikali iko tayari kusaidia kwenye bajeti hii kuunga mkono juhudi zile za wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mbunge wa Jimbo la Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze sana wananchi wa Kata hii ya Miluwi ambao wameanza kuchangia nguvu zao kujenga kituo cha afya na niwahakikishie kwamba Serikali itaendelea kuchangia katika hizo nguvu za wananchi ili kuhakikisha kwamba

kituo hicho kinakamilika kwa awamu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Wananchi wa Kata ya Dalai walijihamisha wakaanza ujenzi wa kituo cha afya. Lini sasa Serikali nayo itaweka nguvu zao ili kituo kile kimalizike? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Jimbo la Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wananchi wameanza ujenzi wa kituo cha afya kwa nguvu zao, tumewapongeza kwa juhudi hizo, lakini Serikali itaendelea kutafuta fedha kama ilivyo kwa majimbo mengine yote ili kuchangia nguvu za wananchi kukamilisha vituo ambavyo vimeanza ujenzi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira kwamba Serikali inatambua hilo na italifanyia kazi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Zahanati za Tandika pamoja na Mibulani zitaanza

kufanya kazi kwa sababu majengo yako tayari na kila kitu na yameanza kupata ufa, tusiipoteze Serikali fedha zile. Je, ni lini zitaanza kufanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dorothy Kilave, Mbunge wa Jimbo la Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vituo vyote vilivyokamilika vinatakiwa vianze kutoa huduma mapema iwezekanavyo na natoa maelekezo kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke kuhakikisha zahanati au vituo hivi vya Tandika na Mibulani vinasajiliwa haraka iwezekanavyo na vinaanza kutoa huduma kwa wananchi kama ilivyotarajiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 317

**Utekelezaji wa ahadi ya Rais kukarabati stendi ya Bweri-Musoma**

**MHE. GHATI Z. CHOMETE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya ukarabati wa Stendi Kuu ya Mabasi Bweri iliyopo Manispaa ya Musoma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Stendi ya Mabasi ya Bweri katika Manispaa ya Musoma ilijengwa mwaka 2007 kwa mapato ya ndani ya halmashauri kwa kutumia Mkandarasi *CMG Construction Company Limited* aliyeingia Mkataba wa shilingi bilioni 1.36 ambapo Mkandarasi huyo alifanya kazi zenye thamani ya shilingi milioni 921.17.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ilikuwa kujenga stendi hiyo kupitia ufadhili wa Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA)*. Hata hivyo kutokana na majadiliano kutozaa matunda, Serikali imeiweka stendi hiyo kwenye Mpango wa *TACTIC* ambapo shilingi bilioni 1.35 zimetengwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ghati Chomete, swali la nyongeza.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwa kuwa miradi ya *TACTIC*, imeshaanza na Halmashauri ya Manispaa ya Mji wa Musoma haimo kwenye miradi hiyo kwa sasa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha mradi huo unaanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Stendi ya Mabasi ya Mji wa Musoma ina hudumia wananchi kutoka Tarime, Serengeti, Rorya, Butiama, Musoma Vijijini na maeneo mengine yanayozunguka Mkoa wa Mara. Kwa sasa stendi ile ni chakavu sana na haipitiki hasa mvua ikinyesha. Je, Serikali ina mkakati upi wa muda mfupi, kuhakikisha stendi ile inaendelea kuingilika ili kusubiri mkakati wa muda mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Miradi ya *TACTIC*, itaanza utekelezaji wake rasmi mwaka wa fedha 2022/2023, lakini Halmashauri hii ya Musoma pia ipo kati ya zile *lot* ya kwanza, ya pili na ya tatu ambapo tutakwenda kutekeleza. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba itapokuwa inaanza mwaka ujao wa fedha, basi Manispaa hii ya Musoma hii stendi itakuwa miongoni mwa zile *lot* tatu ambazo zipo kwenye *TACTIC*.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Stendi ya Mabasi ya Musoma Mjini kuwa ni chakavu sana na inahudumia wananchi wengi. Natoa maelekezo kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Musoma kuhakikisha wanatenga fedha za

mapato ya ndani, kwa sababu stendi ni kipaumbele lakini ni chanzo cha mapato. Kwa hiyo, lazima mapato ya ndani yaanze kuboresha stendi ile wakati wanaandaa andiko la kuomba fedha kama mradi wa mkakati kwa ajili ya kukamilisha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wananchi wa Mkoa wa Rukwa wanateseka sana kuhusiana na stendi, stendi iko mbali na stendi ya zamani iko mjini. Je, ni lini sasa Serikali itaruhusu wananchi wa Mkoa wa Rukwa watumie stendi zote mbili kama inavyotumia Mkoa wa Mbeya, wanashusha Uyole, wanashusha Nane Nane na wanashusha stendi ya zamani. Hivyo, ni lini sasa Serikali itaruhusu wananchi wa Rukwa watumie stendi ya zamani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, sisi Mbeya hatuoni kama tunayo stendi, sasa ukisema Mbeya tuna stendi nashindwa kuelewa sisi tunajihesabu kama Jiji hatuna stendi. Kwa hiyo, usitutajie stendi hizo, hizo ni stendi ndogo sana kwa Jiji kama la Mbeya.

Mheshimiwa Waziri majibu kwa swali la Mkoa wa Rukwa, Mbeya haipo hapo, kwa sababu haina stendi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maamuzi ya mkoa kwa maana ya Viongozi wa Mkoa; Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala na Menejimenti za Halmashauri zetu zote, nawaelekeza wakae wafanye tathmini kwamba kwa nini stendi ya zamani haitumiki na inatumika stendi mpya ambayo iko mbali na waone uwezekano wa kufanya maamuzi stendi ipi itumike au zitumike zote na watupe mrejesho Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwa hiyo, suala hilo litafanyiwa kazi na Serikali. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Regina Qwaray, swali la nyongeza.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Ni muda mrefu sasa katika Mji wa Babati hatuna stendi na stendi haijamaliziwa. Je, ni lini Serikali italeta fedha ili ujenzi ule wa stendi ya Babati ukamilike kama ulivyoahidiwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Regina Qwaray, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa stendi na miradi mingine yote ya kimkakati, kwanza ni jukumu la halmashauri kuainisha gharama, lakini pia kuwasiliana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kuona kwanza kama wana uwezo wa kuzijenga kupitia mapato ya ndani, lakini pili kama wanahitaji kupata fedha kutoka Serikali. Kwa hiyo, mamlaka ya Halmashauri ya Babati, ilete taarifa ya

mpango wa utekelezaji wa stendi ile ili Serikali tuone namna ya kufanya, kama watajenga kwa mapato ya ndani au kama tutafuta fedha kwa ajili ya kujenga kama mradi wa kimkakati. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa stendi ya mabasi ya Shinyanga Manispaa imechakaa na ni ya zamani haijajengwa kisasa, je, ni lini Serikali itajenga Stendi Kuu ya Mabasi, Manispaa ya Shinyanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christine Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, stendi hizi zote kama nilivyotangulia kujibu kwenye jibu la awali la halmashauri husika, Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, wafanye tathmini na kuona gharama ambazo zinahitajika kukamilisha au kujenga stendi ile, lakini waone uwezo wao wa mapato ya ndani kutenga kwenye bajeti. Kama inahitaji gharama kubwa, walete andiko hilo Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ili tuweze kufanya tathmini na kutafuta vyanzo vya fedha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda,

Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba.

Na. 318

**Sifa za vijana kupata mikopo**

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA K.n.y MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Je, Serikali ina kauli gani kuhusu mikopo inayotolewa na Halmashauri kwa kuwa mfumo unawaacha nje vijana wengi kwa kukosa sifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 6 ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu ya Mwaka 2018 pamoja na marekebisho yake inaelekeza sifa na vigezo vya kuzingatiwa kwenye utoaji mikopo kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, vigezo na sifa hizo ni pamoja na kikundi kinachofanya shughuli za ujasiriamali au kinachotarajia kuanza shughuli hizo, Kikundi kiwe kimetambuliwa kama kikundi cha vijana; Wanakikundi

wawe Watanzania wenye umri kati ya miaka 18 hadi 35; Kikundi cha vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea; Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya kikundi; na Kikundi hakitajumuisha wajumbe wenye ajira rasmi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia sifa hizo, katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya Vikundi 1,441 vya Vijana vilikopeshwa mikopo yenye thamani ya shillingi Bilioni 13.5nchini kote.

Mheshimiwa Spika, kauli ya Serikali ni kwamba, vijana wenye sifa tajwa waendelee kujiunga katika vikundi vya wajasiriamali na kuomba mikopo hiyo ili kuinua uchumi wao. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zainabu Katimba swali la nyongeza.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza. Je, Serikali ina mkakati gani wa kufanya ulezi kwa vikundi hivi si tu vya vijana lakini vikundi vya wanawake na watu wenye ulemavu, ili viweze kuwa na ufanisi katika kufanya shughuli zake za ujasiriamali?

Swali langu la pili, tathmini inaonesha kwamba malipo ya fedha hizi za mikopo zinazotoka kwenye Halmashauri bado zinasuasua. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba mikopo hii inalipwa kwa wakati ili waweze kunufaika vijana wanawake na watu wenye ulemavu wengi zaidi? (*Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tamisemi majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zainab Katimba Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkakati ambao Serikali imekuwa inaufanyiakazi katika kuhakikisha vikundi hivi ambavyo vinakopeshwa wajasiliamali wadogo wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuwa endelevu lakini pia kuweza kuwa na tija ni Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri husika kwanza kuwatembelea mara kwa mara, kuwafanyia mafunzo ya mara kwa mara, pia kuwashauri kuona kwamba wanakwenda vizuri na huo ndiyo ulezi wenyewe kwa maana ya kwamba viongozi wa Halmashauri lakini katika ngazi za Kata, Waheshimiwa Madiwani na Viongozi wengine wanahusika kuvifuatilia pia kuvishauri. Tutaendelea kufanya hivyo ili kuhakikisha kwamba vikundi hivi vinakopa lakini vinarejesha kwa tija.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na malipo ya fedha kusuasua ni kweli, kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya Watendaji kuchelewesha malipo haya na Serikali ilishatoa maelekezo kwamba kama kikundi kina kinakidhi vigezo kipate fedha mapema iwezekanavyo ili shughuli ziweze kuendelea, lakini mara nyingine zinacheleweshwa kutokana na baadhi ya vikundi kutokidhi vile vigezo vinavyotakiwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa

Wabunge, sasa baada ya kumaliza hilo lile swali lake la pili Mheshimiwa Mwita Waitara nitaomba utalifuatilia halafu utaniletea mimi hapa taarifa nitakupa fursa ya kulizungumzia.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mohamed Said Issa Mbunge wa Konde sasa aulize swali lake.

Na. 319

**Kilimo cha zao la Mwani**

**MHE. MOHAMED SAID ISSA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza kuhamasisha kilimo cha zao la Mwani?

**SPIKA:** Mheshimiwa ahaa ! Kumbe umeshafika hapo mbele nilikuwa natafuta yuko wapi? Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mbunge wa Jimbo la Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilishaanza kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu zao la mwani na tayari jumla ya wakulima 4,569 wamepatiwa mafunzo ya uzalishaji, uhifadhi na kuongeza thamani katika zao la mwani. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Said Issa swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Swali langu la nyongeza ni kwamba nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Je, Pamoja na juhudi nzuri walizofanya kuhakikisha zao la mwani linakuzwa.

Je, Serikali imefanya juhudi gani kuhakikisha wakulima hawa wanapata soko ambalo litakidhi haja ya kilimo chao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Said Issa Mbunge wa Konde kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya jitihada ya kutafuta masoko na kwa sasa tuna masoko katika nchi za Marekani, Ufaransa na Spain. Kwa umuhimu zaidi tumeanza mazungumzo na Shirika la Usafirishaji, Tumeanza mazungumzo na shirika la usafirishaji la *DHL* ili kuweza kuhakikisha kwamba wazalishaji kwa maana ya wakulima wanapata masoko Kimataifa moja kwa moja kwa kuwa tumeshapata kujua juu ya nini soko linahitaji, mawasiliano ya moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili tunashukuru katika bajeti ya mwaka huu tunaouendea 2022/2023 Serikali imetenga fedha za kutosha za kuhakikisha wakulima

wanaongeza thamani ya zao hili. Kwa hivyo, tutakuwa na mashine za ukaushaji wa Mwani katika mwambao wote wa Pwani, kuanzia Tanga, Pwani mpaka Lindi na Mtwara kwa lengo la kuhakikisha tunaongeza thamani ya zao letu la Mwani ili tuweze kulingana na mahitaji ya soko. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issay. Waheshimiwa Wabunge mliosimama naamini mmelisoma swali la msingi. Mheshimiwa Zacharia Issay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Maeneo mengi nchini yamekosa mazao ya kibiashara hususan Wilaya ya Mbulu na maeneo mengine nchini. Je, Serikali kwa mkakati gani wa kutumia tafiti zake na kuweza kuhamasisha baadhi ya maeneo kupata mazao ya kibiashara?

**SPIKA:** Mazao ya kibiashara Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Juma Usonge Hamad swali la nyongeza.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kunipatia fursa ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Kwa vile zao hili la Mwani zaidi ya asilimia 80 ndiyo tunategemea mauzo ya nje, lakini zaidi ya asilimia 20 ndiyo inabakia kwa ajili ya kulichakata na kutengeneza bidhaa mbalimbali ambazo zinabaki ndani ya nchi. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kutoa elimu hasa kwa wale wakulima wetu ndani ya nchi kuweze kutengeneza bidhaa ambazo zitakuwa na soko pia zitakuwa na *quality* pia zitakuwa zinauzika ndani ya nchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Usonge swali la nyongeza huwa ni moja tu. Swali la nyongeza huwa ni moja siyo mawili.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Haya ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu kwa swali moja.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamad kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, juu ya mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba tunaongeza thamani kama nilivyokwisha kueleza kwenye jibu la msingi. Kwanza Mwani wetu mwingi unakaushwa katika michanga, Mheshimiwa Hamad na Wabunge wa kutoka katika Mikoa hii ya huku Pwani inayolima Mwani wanaweza kuwa ni mashahidi wangu. Ndiyo maana tumejielekeza katika kuhakikisha kwamba tunapata kitu kilicho na ubora kwa kwenda kupeleka mashine za kukausha huu Mwani ili kusudi twende katika hatua inayofuata sasa ya kuongeza thamani kutengeneza sabuni, shampoos, bidhaa za chakula kwa ajili ya kuongeza hii thamani. Kama haitoshi, mbele zaidi tunataka tuanze kufanya *extraction.*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ngoja ngoja kwa sababu muda wa kujibu swali ni mfupi, anataka kujua mpango wa elimu kwa hao wakulima wa Mwani.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, shukrani sana. Kama nilivyoeleza katika jibu la msingi elimu tayari ilishatolewa na tunaendelea kutoa. Kwa hivyo, tutaendelea na mpango wa utoaji wa elimu katika vikundi vyote tunawaunganisha

wakulima wa Mwani ili kuweza kuwa rahisi kwa kazi yetu ya utoaji wa elimu katika Mwambao mzima wa Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa vile wanaojishughulisha sana na zao la Mwani ni wanawake. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapa wanawake hao nyenzo za kisasa kwa ajili ya kilimo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tulishakwisha kuanza kutoa zana kama vile Kamba na ipo zana inaitwa taitai na hilo zoezi tutaendelea nalo ikiwa ni pamoja na matarajio yetu ya kununua boti ambazo zitakwenda kwa ajili ya wavuvi lakini na vikundi vya akina mama kwa ajili ya wakulima wa Mwani kuweza kuyafikia maeneo yale pale maji yanapokuwa mengi na uvunaji wa ule Mwani. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar swali nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Nyang'wale ni wakulima, wachimbaji na wafugaji, tuna mifugo mingi

lakini cha ajabu unamkuta mfugaji ana ng'ombe zaidi ya 100 hapati hata lita moja ya maziwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuja kuwaelimisha wafugaji wangu katika Jimbo la Nyang'wale ili waweze kunufaika na mifugo?

**SPIKA:** Swali la msingi sana hilo lakini haliendaji na swali la msingi lililoulizwa na mwenye swali. Mheshimiwa Catherine Magige swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa wafugaji wengi wa Wilaya ya Longido mabwawa yao yamepasuka na mengine kujaa udongo. Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha wana karabati mabwawa haya au kuyajenga upya kabisa?

**SPIKA:** Swali la msingi sana lakini halina majibu kwa sasa kwa sababu swali la msingi lililoulizwa halihusu mabwawa. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Sasa tunaelekea Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 320

**Kuongeza miundombinu katika Vyuo Vikuu nchini**

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza miundombinu ya Vyuo Vikuu nchini kutokana na ongezeko kubwa la aanafunzi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mradi wa *Higher Education for Economic Transformation (HEET)* itajenga Chuo Kikuu kipya cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Butiama chenye uwezo wa kudahili wanafunzi 5,620. Vilevile Kampasi mpya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika Mkoa wa Lindi kitakachokuwa na uwezo wa kubeba wanafunzi 360, Kampasi mpya ya Mloganzila ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili wanafunzi 11,000, Kampasi mpya ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo cha Mizengo Pinda Mkoa wa Katavi wanafunzi 2,500, Kampasi mpya ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya Kampasi ya Rukwa wanafunzi 3,000. Vilevile, mradi wa *HEET* utafanya ujenzi wa Kampasi mpya za Vyuo Vikuu katika Mikoa ya pembezoni ikiwemo Mikoa ya Kagera, Tanga, Kigoma, Shinyanga, Mwanza, Simiyu, Ruvuma, Manyara na Singida.

Mheshimiwa Spika, mradi huo kwa ujumla unatarajia kuboresha Taasisi za Elimu ya Juu 19 kwa kujenga Hosteli 34 zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 9,042, vyumba vya mihadhara 130 vitakavyokuwa na uwezo wa kubeba wanafunzi 27,254, maabara na karakana zitakazokuwa na uwezo wa kubeba wanafunzi 7,850, kumbi za

mikutano ya Kisayansi 23, miundombinu ya mashambani pamoja na Vituo Atamizi 10. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, pamoja na jitihada za Serikali kuongeza miundombinu zinazoendelea, bado kuna baadhi ya kozi hazitolewi hapa nchini.

Je, Serikali haioni haja ya kushirikiana na vyuo vingine nchi za nje ili kutoa kozi hizo hasa katika sekta ya afya.

Swali la pili, pamoja na mkakati huu wa miundombinu, Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Wahadhiri katika Vyuo Vikuu hapa nchini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri hilo swali la kwanza linaongelea kozi ambazo hazipo. Sasa Mbunge mwenyewe hajazitaja ni zipi ambazo hazipo, kwa hivyo unao uhuru wa kujibu kama unataka kujibu kwa ujumla maana Kanuni zetu zinataka jibu liwe ni jibu halisi kwa ajili ya swali husika, sasa yeye hajataja ni kozi gani kwa hiyo wewe utaangalia jibu kwa ujumla. Haya karibu kwa majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Pauline Nahato kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la kwanza, kwanza tukiri kwamba kuna baadhi ya kozi katika Sekta ya Afya ni kweli hazitolewi hapa nchini. Lakini nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, katika kipindi kifupi tumeweza kupata uzoefu kutokana na janga hili la UVIKO-19 kuna wanafunzi wengi sana walirejeshwa hapa nchini, vilevile kama mnavyofahamu mwezi Februari, Machi mwaka huu kutokana na vita vya Ukraine pamoja na Urusi wanafunzi wengi wameweza kurejeshwa miongoni mwao ni wale ambao walikuwa wanachukua kozi ya ambazo hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza mjadala wa kuangalia namna gani tunaweza kuangalia mashirikiano ya karibu ya kuangalia tunaweza kushirikiana vipi na vyuo vingine vya nje ya nchi ili kozi hizo zinaweza zikatolewa kule kwa ushirikiano vilevile na hapa nchini. Naomba tulibebe wazo hili lakini tubebe ushauri huu wa Mheshimiwa Paulina tuendelee kuufanyia kazi kuweza kuangalia kozi hizi ambazo hazitolewi namna gani tunaweza tukazifanya kwa mashirikiano na vyuo vingine vya nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa eneo la pili la uongezaji wa Wahadhiri, nadhani swali hili nimeshawahi kulijibu hapa Bungeni. Kwanza kupitia mradi wa *HEET* tunakwenda kusomesha Wahadhiri wapya zaidi ya 1,000. Kwa hiyo, pamoja na uongezaji huu wa miundombinu lakini utakwenda sambamba na kusomesha Wahadhiri katika awamu ya kwanza karibu Wahadhiri 625 tunakwenda kuwasomesha wa kozi ndefu lakini wale kozi fupi zaidi ya Wahadhiri 400. Kwa hiyo, tunaamini tunaweza kupunguza uhitaji huo wa Wahadhiri kwenye vyuo vyetu.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili Serikali mara nyingi sana huwa inatoa vibali vya kuajiri walimu wapya, wahadhiri wapya nao vilevile mfumo huo tutautumia. Lakini vyuoni kule kuna mpango vilevile vyuo vyenyewe huwa vinakuwa na mpango wa kusomesha Wahadhiri na kuajiri wale Wahadhiri wa mikataba ya muda mfupi. Kwa hiyo, mipango hii yote tukiijumuisha tunakwenda kuondoa tatizo hili la Wahadhiri.

Mheshimiwa Spika, kama mnavyofahamu Serikali yetu imeweza kuongeza mikopo ile ya elimu ya juu kwa wanafunzi wale ambao wanaoingia katika elimu ya juu, eneo hili kwa vile tutakuwa na udahili mkubwa wa wanafunzi wa elimu ya juu, ni dhahiri kabisa tutaweza kupata wahadhiri wa kutosha kwenye vyuo vyetu hivi ambavyo tunatarajia kuvijenga. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mkoa wa Kagera ni miongoni mwa Mikoa mikubwa sana hapa nchini na wenye wanafunzi wengi. Je, ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa Kampasi ya Chuo Kikuu katika Mkoa wa Kagera?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza Mheshimiwa Dkt. Kikoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati najibu swali la msingi nimezungumza mradi wetu wa *HEET*, kwamba pamoja na mambo mengine unakwenda vilevile kujenga vyuo katika Mikoa ya pembezoni na miongoni mwa Mikoa ambayo niliitaja ni pamoja na Mkoa wa Kagera. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nadhani Mkoa huu upo na upo kwenye *program* hii HEET tutakwenda kujenga chuo katika Mkoa huo wa Kagera pamoja na Mikoa mingine ya pembezoni. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Rashid swali la nyongeza.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar imeshatoa eneo kwa ujenzi wa Chuo Kikuu Huria na Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere katika eneo la Mfikiwa. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Rashid Rashid kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyowaeleza kwenye majibu ya msingi, mradi wetu wa *HEET* unakwenda ku-*cover* karibu maeneo mengine sana. Amezungumza hapa suala la Chuo Kikuu Huria pamoja na Chuo chetu cha Mwalimu Nyerere ambayo tayari ina Kampasi kule Zanzibar, kwa hiyo, ni suala tu la upanuzi Kwa vile amezungumza hapa kwamba kuna eneo ambalo tayari limeshatolewa tunaomba tuchukue wazo hili tuweze kuangalia namna gani ile Kampasi iliyopo pale Zanzibar inaweza kupanuliwa kwa ajili ya kwenda eneo hilo

ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitaja. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, sasa aulize swali lake.

Na. 321

**Mgogoro wa mpaka kati ya wananchi na Kambi ya Jeshi - Itaka**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro wa mpaka kati ya Kambi ya Jeshi 845 Itaka na Wananchi wa Vijiji vya Sesenga na Itewe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Jeshi Itaka ilikuwa ni mashamba ya walowezi wa kikoloni *(settlers)*, yaliyotwaliwa na Serikali kwa mujibu wa sheria. Mashamba hayo yaligawiwa kwa Jeshi kati ya mwaka 1980 na 1981. Mashamba hayo yalikuwa chini ya umiliki

wa Jeshi la Kujenga Taifa Kambi ya Itende. Baada ya mafunzo ya JKT kusitishwa mwaka 1994, wananchi walianza kuvamia na kuendesha shughuli za kibinadamu, hususan kilimo na makazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mwenisongole kwa kuendelea kulifuatilia suala hili kwa karibu. Kufuatia ufuatiliaji wake Wizara imeunda Timu ya Wataalam mbayo imepewa jukumu la kuangalia namna bora ya kutatua mgogoro huu. Timu hii ipo uwandani, ikishirikiana na viongozi, lakini pia pamoja na wananchi katika eneo husika. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge kwa heshima, awe na subira wakati tukisubiri timu hiyo ikamilishe kazi na mapendekezo yawasilishwe na timu hiyo ya wataalam. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri na niko tayari kuvuta subira kusubiri hiyo tume itakayotuletea majibu ila nilikuwa nina ombi moja kwa Mheshimiwa Waziri, je, tume hiyo itakapomaliza kazi, yuko tayari kwenda na mimi Mbozi kuzungumza na wananchi wa hivyo vijiji na kutoa majibu kwa wananchi hao? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kama nilivyokwishamuahidi Mheshimiwa Mbunge, tumeshazungumza suala hili mara

nyingi na nathibitisha tu kwamba, niko tayari kwenda kuongea na wananchi wake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 322

**Uhitaji wa bei elekezi kwenye vifaa tiba**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa bei elekezi ya vifaa vya tiba hasa vya macho, pua na koo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imeandaa kanuni za kudhibiti bei za dawa na tayari zimekwishawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Bei elekezi za vifa tiba zitaandaliwa mara baada ya kukamilika kwa kanuni za bei za dawa elekezi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ninapozungumzia tiba ya macho, pua na koo, nazungumzia ongezeko la mabubu na viziwi nchini. Sasa kwa kuwa, kumekuwa na ongezeko kubwa la mabubu na viziwi nchini ambalo limesababisha Serikali kupeleka ruzuku kwa wanafunzi kutoka bilioni 3.6 mwaka 2018/2019 mpaka bilioni 6.3 mwaka 2021/2022. Je, Serikali haioni haja ya kupeleka vifaa vya kupima usikivu kwenye hospitali za wilaya ili kila mtoto anapozaliwa aweze kupimwa usikivu ili kupunguza tatizo la ububu na uziwi nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa, tangu mwaka 2016/2017, Serikali ilianzisha upasuaji wa kupandikiza vifaa vya usikivu nchini. Je, ni juhudi gani zimefanyika kuongeza vitengo vya *speech therapy* katika hospitali zetu, ili kuondosha tatizo la mabubu na viziwi nchini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja anaulizia ni kwa namna gani Serikali itajipanga kupeleka vifaa tiba kwenye *level* ya wilaya. Tunapokea ushauri wake na sio tu kwenye eneo la kupeleka vifaa kwa ajili ya kupima watu wenye matatizo hayo, lakini ni ku-*include* kwenye *package* ya

mama anayejifungua, wakati anajifungua basi mtoto aweze kuhakikishwa kwamba amechunguzwa vitu vyote kiasi kwamba, hata wakati anahudhuria *clinic* kuna uchunguzi kama huo ili kuwatambua mapema na kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kwamba, toka 2016 kulikuwa na *operation* za kuweka vipandikizi kwa wale watu ambao wana shida ya usikivu; tunapokea ushauri wake na bado tunasema hivyohivyo kama kwenye *issue* ya suala zima la watoto wadogo, vilevile tutapeleka kwa kuanzia kwenye *level* za mikoa kuhakikisha *operations* kama hizo zinaweza kufanyika na watu wao kupata huduma, lakini vilevile kwa watu ambao tayari wana tatizo hilo tunatengeneza utaratibu wa kuwasaidia hasa wanapokuja hospitali, watu wanaoweza kufafanua zile lugha za ishara na mambo mengine, ili waweze kupata huduma kama watu wengine. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Mayenga, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kituo cha Afya cha Kambarage kilichopo Manispaa ya Shinyanga Mjini ambacho ni tegemeo kubwa sana kwa wananchi na hasa akinamama kwa kuwa kinazalisha akinamama takribani 330 kwa mwezi, kinakabiliwa na tatizo kubwa sana la ukosefu wa *generator.* Kiasi cha shilingi milioni 290 ambayo ilitolewa katika mpango wa Serikali kuboresha vituo vya afya ilitolewa na ikakabidhiwa *MSD,* vifaa tiba vingi vimekuja kasoro *generator,* wananchi wanalalamika. Je, ni lini

*generator* litakuja kama sehemu ya vifaa-tiba katika Kituo hicho cha Afya cha Kambarage? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nimetembelea hicho kituo na nimekuta Mheshimiwa Mbunge alichangia milioni 18 kwa ajili ya ujenzi wa hicho kituo, lakini ninachoweza kusema ni tukishamaliza maswali hapa, tukutane mimi na yeye, tutashirikiana na mwenzangu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ili tuweze kuhakikisha kwamba, vifaa hivyo vinafika kwa sababu, kama fedha zimepelekwa, basi ni kupeleka kile ambacho kinatakiwa kufanyika. Tukae mimi na yeye tuhakikishe *generator* limeenda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Hassan Selemani Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 323

**Ujenzi wa Daraja la Mto Ruvuma**

**MHE. HASSAN S. MTENGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Daraja la Mto Ruvuma ili kufungua Shughuli za Kibiashara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. FREDY A. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Selemani Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali za Tanzania na Msumbiji zilijenga Daraja la Umoja (Mtambaswala) ili kufungua shughuli za kibiashara. Kwa sasa Serikali ya Tanzania inategemea kuanza kufanya mazungumzo na Serikali ya Msumbiji, ili kuanza taratibu za ujenzi wa Daraja la Kilambo, Mto Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Mtenga, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; naomba *commitment* ya Serikali, ni lini ujenzi huo wa daraja utaanza?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni lini Mheshimiwa Waziri tutaongozana nami ili twende kwenye eneo husika ambalo tunalizungumzia la kujenga daraja apate ufumbuzi zaidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. FREDY A. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hassan Selemani Mtenga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza anataka *commitment* ya Serikali kwamba, lini ujenzi huu hasa utaanza katika daraja hili la Mto Ruvuma, eneo la Kilambo. Nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia suala zima la daraja hili katika Mto huu Ruvuma, sababu tunatambua kwamba, daraja hili ni kiungo muhimu kati ya Nchi yetu ya Tanzania na Nchi ya Msumbiji. Kwa maana hiyo, mazungumzo ambayo tutayaanza hivi karibuni pamoja na Nchi ya Msumbiji kupitia Wizara yetu ya Mambo ya Nje, tutafanya *commitment* kupitia pia Wakala wetu wa Barabara Nchini *(TANROADS)* ili tuanze sasa mchakato mzima wa kuanza kujenga daraja hili, maana daraja hili lazima lijengwe na nchi mbili kati ya Tanzania na Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Kwenda naye kuona hili eneo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mara baada ya Bunge hili la Bajeti, mwezi Julai nitakuwa na ziara, hivyo nitakwenda kwa Mheshimiwa Mbunge kutembelea eneo hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mliosimama nimewaona, lakini kwa sababu, kanuni zetu zinataka majibu ya maswali yawe ni majibu kamili, kwa maana ya maswali yetu yajibiwe kikamilifu, huyu ni Naibu Waziri upande wa Uchukuzi kwa hivyo, hayo maswali yanamtosha.

Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 324

**Kuleta Sheria ya Uanzishaji wa Baraza la Taaluma ya Ustawi wa Jamii**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatunga Sheria ya Uanzishwaji wa Baraza la Taaluma kwa Kada ya Ustawi wa Jamii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na Uandaaji wa Sheria ya Taaluma ya Ustawi wa Jamii kwa kujumuisha maoni ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na ya wadau mbalimbali kwa kushirikiana na Chama cha Wataalam wa Ustawi wa Jamii Tanzania na itakapokamilika Muswada wa Sheria utawasilishwa Bungeni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini sambamba na hilo nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; naomba kupata *commitment* ya Serikali kuhusiana na kutunga sheria hii. Je, sheria hii itaweza kutungwa ndani ya uhai wa Bunge hili?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa, sheria imechukua muda mrefu kutungwa. Je, Serikali haioni sababu ya kutengeneza mkakati au mpango maalum wa kuona jinsi ya kuweza kuwaangalia hawa Maafisa Ustawi ambao wanakiuka taratibu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Toufiq, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, inaona umuhimu wa sheria hii. Kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi Serikali itasimamia sheria hii ili iweze kuwasilishwa mapema katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili kuhusu Maafisa Ustawi kuwa na maadili. Ushauri umepokelewa. Hata hivyo, Wizara inafuata kanuni za utumishi wa umma kwa wafanyakazi wote na wafanyakazi wote wanaokiuka maadili, hatua za kisheria zinachukuliwa pale wanapofanya makosa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimemwambia Naibu Waziri ningempa nafasi, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwenye swali Namba 316, ya kumjibu swali la nyongeza la kwanza alilokuwa ameliuliza Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, kuhusu kukamilika kwa wodi ya wanawake na wanaume kwenye kituo hicho cha afya.

Jibu la msingi linasema wodi hiyo ya wanawake na wanaume ipo na imekamilika, lakini Mheshimiwa Mbunge anasema haijakamilika. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri hajaleta bado huo ufafanuzi. Kwa hivyo, tutaliacha hapo kwa leo, aendelee kutafuta huo ufafanuzi, utakapokuja basi, Waheshimiwa Wabunge mtajulishwa, lakini pia mwenye swali lake Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, ufafanuzi huo utakapokuja ndio tutakapotoa hapa kama kuna maelekezo yoyote ya kutoa kuhusu majibu hayo ambayo yalitolewa, ambayo ni ya msingi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni humu ndani. Tutaanza na wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao wamewaalika hapa kwa ajili ya kuja kutazama shughuli za Bunge:-

Wageni wa Wabunge wote wasimame kwa pamoja. Karibuni sana wageni wetu, tunaamini mnawaona Wabunge wenu humu ndani. *(Makofi)*

Pia, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao wanafunzi 93 na Walimu sita wa Shule ya Msingi Mlimwa ya Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 70 na Walimu 10 kutoka Shule ya Sekondari Mvumi *Mission* iliyopo Mvumi, Mkoani Dodoma; hawa sidhani kama wameingia? Nadhani wataingia baadaye, watakapofika watatangazwa.

Waheshimiwa Wabunge hayo ndio matangazo niliyonayo hapa. Kwa hiyo, tutaendelea na ratiba yetu, Mwenyekiti wa Bunge ataingia sasa.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na wachangiaji wetu wa leo. Mchangiaji wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Catherine Magige, akifuatiwa na Mheshimiwa Joseph Musukuma, wakati huo Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama ajiandae.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Nishati. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na Wizara nzima kwa kazi kubwa wanazozifanya.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MBUNGE FULANI:** Waziri hayupo na Naibu hayupo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magige, Serikali ipo Bungeni.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Nilimwita Mheshimiwa Catherine Magige.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Wizara hii ya Nishati. Wanastahili pongezi sana, Waziri na timu yake nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Catherine Magige, hebu keti kwanza.

Waheshimiwa Wabunge tunaahirisha shughuli za Bunge kwa nusu saa, mpaka Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri watakapokuwa wameketi Bungeni.

*(Saa 3:58 Asubuhi Bunge Lilisitishwa kwa muda)*

*(Saa 4.30 Asubuhi Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishatikwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimuita Mheshimiwa Catherine Magige, Mheshimiwa Joseph Musukuma ajiandae, pamoja na Dkt. Joseph Mhagama.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze kwa kumpongeza Waziri kaka yangu January kwa kazi kubwa unayoifanya pamoja na timu yako nzima pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Rais hakukosea kukupa hii Wizara unaimudu na unaiweza chapa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuanzisha mpango wa kuwa na hifadhi ya kimkakati ya mafuta na kuhakikisha kwamba *TPDC* inawezeshwa kushiriki katika biashara ya mafuta kupitia kampuni yake tanzu ya *TAN OIL* ili kuwezesha upatikanaji wa mafuta

nchini. Ieleweke kwamba *TPDC* haifanyi biashara hii yenyewe inafanya usimamizi inayofanya biashara hii ni *TAN OIL*. Hii ni hatua nzuri sana niwapongeze, tumeona nchi za wenzetu kama Saudi Arabia, Algeria na Falme za Kiarabu wanatumia makampuni katika mataifa yao katika biashara hii. Niwapongeze sana Serikali niipongeze Wizara na Waziri na timu yako yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kutenga Shilingi Bilioni 500 kwa kuboresha *grid* ya Taifa, pesa hizi zitasaidia upatikanaji wa umeme na kupunguza tatizo la umeme. Tunajua umeme ni uchumi, umeme ni kila kitu tunajua Bilioni hizi 500 zitasaidia sana. Sambamba na kupongeza Serikali naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mtendaji Mkuu wa Tanesco Ndugu Maharage Chande anafanyakazi kubwa sana tunaiona na tupo pamoja naye tunamuomba endelea kufanyakazi kuhakikisha changamoto hii ya umeme kwa wananchi inapungua kama siyo kuisha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kutenga Shilingi Bilioni 140 kwa ajili ya kuendelea kusambaza miradi ya umeme vijijini na pia kwa ajili ya kuongeza kusambaza umeme katika vitongoji. Changamoto ya umeme katika vijiji bado ipo kwa baadhi, mimi mwenyewe katika Mkoa wangu wa Arusha katika vijiji vya Wilaya ya Longido, Karatu, Arusha Mjini, Ngorongoro, Arumeru, Meru, kote huko bado kuna changamoto ya baadhi ya vijiji kukosa umeme. Mheshimiwa Waziri nilikuletea *list* ya vijiji vyangu na uhakika kabisa uliniahidi vijiji vyangu vya katika Mkoa wa Arusha ambavyo havina umeme vyenye changamoto vitapata mpaka vitongoji. Kwa hiyo tunasubiri wananchi wa Arusha umeme huo uweze kutufikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kutenga Shilingi Bilioni Moja katika mradi wa kuhamasisha matumizi endelevu ya nishati safi. TUNAJUA 20% ya wagonjwa wanaosumbuliwa na mfumo wa upumuaji unatokana na matumizi ya kuni, tunaimani kabisa mradi huu utasaidia sana hasa akinamama ambao wengi ndiyo tunahangaika katika kupika kwa kutumia kuni. Tunajua Mheshimiwa Waziri wewe ni mdau mkubwa wa mazingira ulikuwa katika Wizara ya Mazingira, Tanzania tulikuwa tumeshazoea mifuko ya *plastic* uliacha alama ulihakikisha Tanzania sasa hivi mifuko ya *plastic* hakuna tumeisahau kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kukutia moyo Mheshimiwa Waziri najua wewe ni kijana mchapakazi, hakuna sehemu ambayo unapita huachi alama, kila sehemu unaacha alama na tunayo imani kabisa utaacha alama kubwa sana katika Wizara hii tuna imani na wewe, Watanzania tuna imani na wewe, chapa kazi tuna imani na Naibu wako pia Makatibu Wakuu na wote katika Wizara yako timu yako nzima tuna imani na ninyi chapeni kazi wananchi wana mategemeo makubwa sana na ninyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna imani sana na Mheshimiwa Waziri, Rais alimteua January hakufanya makosa kwa sababu tumeanza kuona, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, tumeona kazi kubwa inayofanywa na Wizara pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii, naunga mkono hoja ahsante sana.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Catherine Magige. Nilimuita Mheshimiwa Joseph Musukuma wakati huo Mheshimiwa Dkt Joseph Mhagama anajiandaa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inazofanya pamoja na mambo madogo madogo yanayoendelea kutokea lakini hizo ndizo changamoto lazima ukabiliane nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kuhusiana na suala la umeme, jana kuna mchangiaji nilimsikia anazungumza kuhusu *sub-station* ya Geita. Ni kweli tulimuona hata Mtendaji Mkuu wa *TANESCO* Ndugu Maharage kwenye vyombo vya habari anatangaza kufunga mkataba na *GGM* ambayo tunategemea kupata karibu Bilioni Tano kwa mwezi na utekelezaji wake ulitakiwa uwe umekamilika mwezi wa 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshauri Waziri kuwanyang'anya biashara ya mafuta ya *exemption GGM* siyo kazi ndogo, ubovu mwingine Serikali ukishajitangaza kwenye *tv* hamna ufuatiliaji, nilijaribu kufuatilia kule *GGM* hakuna kitu kinaendelea ndiyo kwanza wako kwenye manunuzi na wakati ujenzi wa *sub-station* ulitakiwa uwe umekamilika mwezi wa 12, kama leo ni mwezi wa Sita ndiyo kwanza wanaanza manunuzi, maana yake kuna miaka miwili ijayo.

Mheshmiwa Mwenyekiti, tunajua sisi tunaoishi pale kwamba wanatumia zaidi mafuta karibia zaidi ya lita Milioni Tatu kwa mwezi, siyo kazi ndogo na kuna *deal* za watu pale, siyo kazi ndogo ni lazima *TANESCO* muwe na mkakati mzuri maana ya kujenga ile *sub-station* ya Geita ilikuwa ni pamoja kulilenga lile soko la mgodi mkubwa wa *GGM* sasa naona kama tuna mizaha mizaha ambayo ninaimani wenzetu ndiyo wanatumia kama nafasi. Kwa hiyo, ni vizuri Mheshimiwa Waziri fanya ufuatiliaji uone

wamefikia wapi usikae kuletewa tu taarifa za makaratasi, naamini hazitakusaidia na sisi wengine tulioko kule tunaona hali siyo nzuri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili mimi kwenye Jimbo langu nimepata Ofisi ya *TANESCO* ambayo Meneja wetu pale anaenda mpaka kilometa 100 mpaka kilometa 90 kwenda kutoa huduma, tulikuwa hatuna gari anatumia pikipiki tena bodaboda, hapa amebeba viatu vya kukwea kwenye nguzo amebeba na vifaa vya kwenda kutengenezea. Nilipozungumza humu mmetuletea gari ambayo kiukweli ni kama dharau bora angebaki tu kwenye bodaboda. Gari inasukumwa kilomita moja ndiyo inawaka! Sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri mimi ni Mjumbe wako wa Kamati najua mipango uliyonayo, toka akiwa Waziri Kalemani mnasema mna magari 100 yamefikia wapi? Au yamekuja yameenda wapi? Huko Mjini watu wana vitendea kazi sehemu ambazo mmepeleka huduma vijijini pelekeni magari ili watu waweze kufurahia huduma ya Tanesco vizuri pale wanapokuwa wamepata matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu nazungumza kwenye suala la mafuta. Nilizungumza hapa tunaishukuru Serikali imechukua hatua kupunguza kuweka bei, kuweka ile Bilioni 100 imepunguza lakini imepunguza wapi? Mimi naiona tu kwenye karatasi mpaka leo, yaani imepunguza kwa mletaji imepunguza kwa watu wa Dar es Salaam mimi ninayetoka Nzela Vijijini na Wabunge wenzangu mafuta ya vituo vyetu almaarufu madumu bado bei ni ile ile na imeongezeka sehemu zingine. Sasa Mheshimiwa Waziri mtusaidie maana tukitoa ushauri saa nyingine huwa hamtusikii tunawaeleza kila siku legezeni masharti ya vituo vya vijijini ili watu wakafungue vituo. Unawekage sharti kituo cha kijijini kinachouza lita 200 unaweka

masharti sawa na kituo cha Kariakoo kinauza lita 15,000? Kwa hiyo, utakapokuwa umelegeza masharti nikuhakikishie kwamba madumu kule yatapungua na bei zitakuwa zinafuata utaratibu kwa sababu watu watakuwa na *reserve* ya kutosha. Kwa hiyo nikushauri narudia kushauri na kwenye Kamati nimezungumza ni vizuri tukabadilika mwaka wa pili hii tunazungumza karibia wa tatu tulegeze masharti ya kituo cha mafuta cha kijijini kisifanane na vituo vya mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Nne Mheshimiwa Waziri ni kuhusiana na suala la biashara kwenye hili naungana na Prof. Muhongo. Unajua biashara inataka vitu vingi sana, siyo tu *degree* kuipeleka *TPDC* kwenda kufanya biashara ya mafuta nakuambia ukweli mimi naungana na Mheshimiwa Profesa Muhongo hatutafika popote ni suala la muda tu. Tulikuwa na kampuni inaitwa *COPEC* iliingia kwenye hizi biashara ilienda wapi? Ilikufa sasa hivi tumeibuka tena na *TAN OIL* tunasema ni shirika, kampuni tanzu lakini bosi ni huyo huyo Mataragio na hii nawapa labda mwaka mmoja tu na yenyewe mnapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya mafuta ina akili nyingi, kwa mfano watu kama *MOIL* na wengine wenye vituo vya mafuta wanawakopesha wateja wakauze kwenye madumu walete haya huko kwenye *TANOIL* unamkopeshaje mteja? inaweza ikaharibika tu *pump* ya kutengeneza kwa 15,000, 20,000 unaanza *procurement* siku tatu mpaka mafuta yanakupandia bei. kwa hiyo niombe sana mimi nakubaliana na Muhongo *TPDC* ibaki kwenye kazi yake ya taaluma ya kutafuta mafuta na kutafuta gesi kwenye biashara tuwaachie *private sector* mimi nakuhakikishia Mheshimiwa Waziri hii pesa kwa mfano ungempa *private sector* akafanya na

huu mtaji baada ya miezi zita tungekuwa na faida kubwa sana lakini leo pamoja na kwamba ni Kampuni ya Serikali nakuhakikishia Mheshimiwa Waziri huko tuendako bado tuko Bungeni kuna mzinga ambao najua tu utakuja wala siyo muda mrefu tutakuja kuujadili tena humu. Tuziache *private sector* zifanye kazi za biashara sisi tufanye kazi ya taaluma kuwaonyesha watu wafanye kama walivyosomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kuhusu mafuta ninataka kumuuliza Waziri na wataalam wake mimi ni mfanyabiashara kama sifanyi biashara ya mafuta lakini nina biashara zingine zina-*attach* na mafuta. Katika hii biashara ya kushusha bei jana Tarehe Mosi nataka mnipe majibu kwenye ku-*wind up* aliyepata faida ni mwagizaji au muuzaji? Kwa sababu kuna watu wana vituo huko vijijini wamefumaniwa na lita 20,000 jana na wao wameshazinunua *cash* na hizi pesa tunakopa benki kwa asilimia 22, amekutwa na labda lita 100,000, 200,000 bei imeshuka hakuna utaratibu wa ku-*return* hela zao, sasa hiyo hasara inabebwa na nani? Kwa sababu mlikuwa mnafanya tathmini ya kushusha mafuta Tarehe Mosi mlifanya utafiti kwa Watanzania ambao wana vituo huko mijini na vijijini kwamba tutakaposhusha watakula hasara gani, kama ni hapana lazima tukae chini tuangalie tumewatia umaskini watu wetu hawa wanaouza vituo vya vijijini na Mikoani kwa sababu pengine hatukufanya utafiti mzuri na haya ndiyo mambo ambayo bado ninasema Mheshimiwa Waziri tuiache *TPDC* ifanye kazi ya taaluma, hii kazi ya biashara tuwaachie *private sector* hii zimamoto Mheshimiwa Waziri wewe bado ni wa kwetu tutakuja kukaa tena na wewe bajeti ijayo bahati nzuri watu wengine *computer* inawezekana hawatunzi vizuri vile vipaumbele vyako ulivyovigawa jana usubiri mwakani vinakuja kukusulubu tena humu ndani. Nakueleza ukweli

kwa sababu watu wametunza zile wanakusubiria mwakani, tunajua ni bajeti yako ya kwanza hii ya mkakati wako lakini mwakani tunakung'ang'ania tuko na wewe tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Waziri Mkoa wa Geita tumepata bahati mbaya sana, tumepata Mkandarasi ambaye wenzetu tayari miradi inaendelea akaonekana hana uwezo, tumepata mwingine nikuombe Mheshimiwa Waziri hakuna siasa nzuri Tanzania kwa wanasiasa kama umeme tukuombe hawa Wakandarasi uwasimamie vizuri na Mheshimiwa Waziri imetosha muda wa kukaa ofisini wa mipango, umemaliza karibia miezi sita zunguka! Watanzania tunataka kukuona huko kwenye nguzo huko tunakueleza nguzo zinaanguka unaona, tukizungumza nguzo zinatengenezwa ni fupi unaona zunguka usiletewe makaratasi, mimi nakukaribisha sana kwenye Mkoa wangu wa Geita lakini na Jimbo langu uje uone na hayo matatizo ninayo kuambia, tunayo ofisi lakini bado watu wakitaka kwenda kulipa labda bili au nini wanatakiwa watembee kilometa 57 na ofisi ya *TANESCO* iko pale, tunashindwa nini gharama ya kufunga mfumo na kufanya zile *correction* na kuwahudumia watu tatizo liko wapi Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri haya matatizo yako kila mahala kwa Wabunge ambako vimepelekwa vituo vidogo bado mtu anaona bango la ofisi ya *TANESCO* lakini unaambiwa tembea kilometa 100 kwenda kulipia bili au kutatuliwa tatizo la kimsingi. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri uwe makini na uzunguke kwa ajili ya kuona matatizo ambayo tuko nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine Mheshimiwa Waziri la bwawa la umeme, nazungumza tena ninakuomba Mheshimiwa Waziri

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma muda wako umekwisha.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimuita Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama wakati huo Mheshimiwa Hassan Kungu, Mheshimiwa George Malima wanajiandaa. Utaratibu wetu ni ule ule tunaanza na waliochangia mara chache zaidi ndiyo tunakuja wa mara mbili, mara tatu, mara nne mpaka mara tano. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi siku za karibuni dunia na Taifa letu kumekuwa na *shock* kubwa sana ambayo imepelekea upandaji mkubwa sana wa bei ya bidhaa muhimu kiasi ambacho Watanzania lakini na wananchi wengi duniani wamepata ugumu wa kukabiliana. Kama Taifa lakini kama Serikali ukilinganisha na Serikali zingine zote duniani moja katika majukumu yao muhimu katika eneo hili ni kuhakikisha kwamba inafanya *intervention* ambayo itasaidia kupunguza gharama za maisha itasaidia kupunguza upandaji wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu unaonyesha moja katika bidhaa ambazo zina madhara makubwa sana

kwenye upandaji wa bei ya bidhaa na huduma katika nchi yoyote ni mafuta ya *petrol, diesel* na kadhalika. Changamoto hii bado tunayo na kwa sehemu imepata utatuzi kulikuwa na sera za kifedha na za kikodi ambazo Serikali ilizifanyia kazi na tukapata ruzuku na sasa tumeona faida yake kwamba mafuta kwa sehemu kubwa yamepungua bei ukilinganisha na vile ambavyo ingekuwa kama Serikali isingechukua hatua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili naomba niipongeze sana Serikali imechukua hatua muhimu lakini niombe sana hatua hizi zisiishie kwenye ruzuku peke yake, mikakati mingine yote ambayo Serikali imeiweka ikiwemo pamoja na *Strategic Reserve* iendelee ili Watanzania waweze kupata nafuu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni ule ule kwamba gharama ya maisha imepanda duniani kote, bei ya nishati imepanda duniani kote kinachotofautisha kati ya Taifa moja na lingine ni hatua ambazo Serikali inazichukua ili kupunguza gharama hizo. Tanzania tumeongoza njia Mheshimiwa Rais ameongoza njia kwa kutoa hizo Bilioni 100 ambazo zimekuja kama ruzuku kwenye sekta ya mafuta ili Watanzania wapate unafuu. Unafuu huu utapatikana zaidi iwapo jitihada zingine ambazo Mheshimiwa Waziri umezisema utaendelea nazo na utaenda kuzikamilisha na mimi nitaunga mkono hoja ya bajeti hii kwa sababu naamini watakwenda kuitekeleza hii mikakati ambayo imewekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni kuhusu Jimboni kwangu. Naishukuru Serikali, kwa sehemu Madaba tumepiga hatua kwenye upatikanaji wa umeme vijijini, asilimia karibu 95 ya Vijiji vya Madaba na maanisha Madaba kama Halmashauri, vijiji vyote vimepata umeme

isipokuwa Kijiji kimoja cha Ifinga. Kwenye hili naipongeza sana Serikali. Kijiji kilichobaki ambacho ni Ifinga kipo kilometa 48, Mheshimiwa Waziri alituletea wataalam wa masuala ya umeme hapa na wakandarasi, tumezungumza nao na wametuhakikishia kwamba mwezi Desemba, Kijiji cha Ifinga kitakuwa kimepata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanaifinga wanasubiri Desemba waende kusherehekea Krismasi wakiwa na umeme kwenye nyumba zao. Pia pamoja na jitihada nzuri za Serikali, yapo baadhi ya maeneo ndani ya Madaba hayajafikiwa na umeme, nayo ni maeneo muhimu sana. Kwanza tunazo sekondari mbili, hizi naomba Mheshimiwa Waziri aziandike tafadhali, tunayo Sekondari Kongwe ya Lipupuma, ipo ndani ya Kata ya Mkongotema, Kijiji cha Mkongotema, sekondari hii ni ya muda mrefu wakati wana-*design* umeme sekondari ilikuwepo, wakati wanaleta nguzo sekondari ilikuwepo, wakati wanafunga nyaya sekondari ilikuwepo, lakini hadi leo haijapata umeme na mtaa mzima wa Lipupuma haujapata umeme. Watanzania wanaoishi maeneo yale wana imani na Mheshimiwa Waziri, tunaomba tupate umeme haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madaba pia kuna sekondari mpya inajengwa pale na sekondari hii amepewa heshima Mbunge wa Jimbo la Madaba, Joseph Kizito Mhagama na inaitwa kwa jina hili. Tunaomba tupewe umeme haraka sana kwa sababu mwezi Januari tunaanza masomo pale. Kwa hiyo tunaomba sana eneo hili lipate umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo eneo la sekondari mpya vile vile inayojengwa Maweso, ni pembezoni

kidogo cha kijiji, hatuna umeme. Watanzania wanaoishi eneo lile wanasubiri wapate umeme. Maeneo ambayo yamesambazwa umeme kwenye vijiji vyetu hayajasambazwa kwa ukamilifu. Tunaamini kwenye programu ya kujaziliza umeme na kupanua umeme, Madaba itapewa kipaumbele. Kijiji cha Mtepa mitaa yake mitatu Mtumbika, Makaraveti na Miembeni kote umeme haujafika. Wananchi hawa wanategemea Waziri awape kipaumbele

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Vitongoji vya Ngadinda, Lilondo na baadhi ya vitongoji vya Mahanje havijapata umeme. Hata Madaba Mjini pale pale katikati ya mji kuna vitongoji havijapata umeme, Kijiji cha Gumbilo, kijiji Kongwe kabisa nacho baadhi ya vitongoji havijapata umeme. Mimi binafsi sina mashaka juu ya *commitment* ya Serikali kwenye kupeleka umeme vijijini, naelewa jambo hili lina bajeti *implication,* lakini kwa sababu tulishawaahidi Watanzania na kwa sababu mama amedhamiria kufanya kazi hii kwa weledi mkubwa, naomba Wizara imsaidie mama kufikisha umeme vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kukuza uchumi kama hatutafikisha umeme vijijini ili vijana wa Kitanzania waweze kujiajiri kwenye shughuli ndogo ndogo za ufundi umeme, ufundi simu, ufundi redio, lakini wafanye masuala ya *welding. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maslahi ya muda, nakushukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Madaba na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa

Hassan Kingu, wakati huo Mheshimiwa George Malima na Mheshimiwa George Mwanisongole wanajiandaa.

Mheshimiwa Hassan Kungu nafikiri hayupo, haya Mheshimiwa George Malima.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie katika hotuba hii ya Wizara ya Nishati. Kwanza kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kufanya katika nchi yetu na hasa ile *subsidy* ambayo imetolewa kwenye bei ya mafuta na hata tumepunguziwa kidogo namshukuru sana. Pia niwapongeze Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo pia inaendelea kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri bado kuna changamoto katika Wizara hii na napenda kuzungumzia baadhi ya changamoto ambazo nimeziona. Changamoto ya kwanza ni huu Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini ambao unasimamiwa na *REA*. Umeme umesambaa katika vijiji vingi katika nchi hii, lakini ukienda katika hivyo vijiji utakuwa umeme umewekwa katika *center* ya kijiji, kijiji kimoja kinakuwa na nguzo 20 au chini ya 20, kwa hiyo unakuta sehemu kubwa ya kijiji hakuna umeme. Hii imesababisha malalamiko mengi sana kwa wananchi. Ningeshauri sana jambo hili walizingatie, haitakuwa na maana tukisema tumeweka umeme katika vijiji vyote katika nchi hii, wakati wanaonufaika katika vijiji ni asilimia ndogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni Mradi wa Kusambaza Gesi Majumbani. Mradi huu ni muhimu sana kwa maendeleo

ya nchi yetu, lakini usambazaji wake unasuasua sana. Hadi sasa gesi hii imesambazwa katika Mikoa mitatu Mtwara, Lindi na Dar es Salaam na katika viwanda ni viwanda 53 tu ambavyo vimesambaziwa gesi, lakini pia nyumba ambazo zimesambaziwa gesi ni 1,379, nadhani tunaweza kuona ambavyo *speed* yake ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya gesi kwenda majumbani ni kubwa sana, itatusaidia kutunza mazingira yetu. Watu wengi wakisambaziwa gesi majumbani wataepuka matumizi ya mkaa na kuni, hivyo tutalinda mazingira yetu. Kwa hiyo ningeomba sana Wizara hii iendelee kwa *speed* ile ambayo watu tulikuwa tunaitarajia, ikiwezekana miji yote au mikoa yote ya Tanzania ipate huduma hii ya gesi majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye Jimbo langu la Mpwapwa, bado usambazaji wa umeme sio wa kuridhisha sana. Mpaka sasa hivi kuna zaidi ya vitongoji 50 ambavyo havina umeme, lakini vijiji ni zaidi ya 15 bado havina umeme. Nimesikia wengine wanasema kimebaki kijiji kimoja, lakini mimi ni zaidi ya vijiji 15. Kwa hiyo ningeomba sana *speed* ya usambazaji pia iongezeke, vitongoji zaidi ya 50 ni vingi mno, hata tunashindwa kuelewa kama kweli katika Jimbo la Mpwapwa tuna katika umeme vijiji vyote. Kwa hiyo naomba sana Mheshimiwa Waziri na wenzake wazingatie sana jambo hili. Umeme ndio suluhisho la uchumi katika nchi yoyote duniani, kama nchi haina umeme maana yake hata uchumi wake utaendelea kudumaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ni muhimu katika viwanda na tumesema viwanda vikubwa au vidogo ndio vinavyotoa ajira kwa wananchi wengi, sasa kama hatuna umeme wa uhakika maana yake viwanda havitakuwepo

na hata tukiwa navyo havitafanya kazi kama inavyotakiwa. Kwa hiyo ni muhimu sana tukazingatia kwamba, tukiwa na umeme wa uhakika tutakuwa tumejitahidi kutoa ajira kwa vijana wetu na viwanda vitakuwepo, lakini vijana wa vijijini ambako pia hakuna viwanda watafungua viwanda vidogo vidogo. Watafungua viwanda vya kuchomelea vyuma, wengine watafungua *saloon*, kuna kazi nyingi sana ambazo zinategemea umeme. Kwa hiyo, Wizara hii ni muhimu inatakiwa iangalie sana na izingatie jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la bei ya kuunganisha umeme, jambo hili bado halijaeleweka vizuri, utasema kijijini ni Sh.27,000, lakini bado wananchi hatujaelewa vizuri au hawajaelewa vizuri wapi ni mjini na wapi ni kijijini. Kwa hiyo unakuta kamji kapo nje ya mkoa lakini kwa sababu kuna ka-*centre* kidogo, basi gharama ya kuunganisha umeme inakuwa ni kubwa. Nadhani jambo hili kama Wizara ingeweza kuli-*address* vizuri ili wananchi waelewe ni maeneo gani ambayo gharama ya kuunganisha umeme inatakiwa iwe Sh.27,000 na maeneo gani yanayotakiwa kuunganisha umeme kwa bei ya Sh.300,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila hivyo kumekuwa na migongano mingi sana, wananchi wa vijijni wakiambiwa hiyo bei ya Sh.300,000 hawawezi ku-*afford,* matokeo yake hawa watu wanaamua kuacha, kwa hiyo hakuna umeme vijijini. Kwa hiyo naomba hilo nalo liwekwe vizuri ili tuelewe ni maeneo gani yanaunganishwa kwa Sh.27,000 na maeneo gani yataunganshwa kwa bei ya Sh.300,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine au changamoto ambayo ipo kwenye Wizara hii ni kukatika katika kwa umeme hovyo na hii nadhani inasababishwa

na uchakavu wa miundombinu. Wizara ingejikita sana kuboresha miundombinu kwasababu kukatika katika kwa umeme katika maeneo yetu kumesababisha hasara kubwa sana kwa wananchi, vifaa vyao vinavyotumia umeme vimeungua na taratibu za kupata *compensation* ni ngumu, kwa hiyo watu wamekutana na tatizo hili, umeme unakatikakatika kila wakati. Kwa hiyo tunaamini kwamba jambo hili wanalijua na watajitahidi sana kuimarisha miundombinu. Miundombinu iliyopo sasa katika maeneo mengi ya nchi yetu imechakaa sana na ndio maana umeme hauwezi ku-*flow* vizuri. Hivyo, tunawaomba sana kama Wizara wazingatie hili na ikiwezekana ule mradi wa kusambaza nguzo za zege uendelee katika maeneo yote ili umeme uwe *stable*, nchi iwe na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa George Malima. Nilimwita Mheshimiwa George Mwenisongole, wakati huo Mheshimiwa Mariam Ditopile, Mheshimiwa Maimuna Mtanda na Mheshimiwa Isack Francis Mtinga, wanajiandaa.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa hii nafasi muhimu sana ya kuchangia bajeti hii muhimu kwa Watanzania. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa fedha shilingi 100,000,000,000 alizotoa, imeonesha kabisa kwamba Rais wetu anajali maisha ya Watanzania.

*Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa mara ya kwanza*

*tangu niwe Mbunge nimeshuhudia Waziri anawasilisha hotuba yake ya Bajeti bila kumleta mke wake humu ndani, badala yake Mheshimiwa Waziri ametuletea hivi vipaumbele vya bajeti imeonesha kabisa huu Waziri yupo serious. Mambo ya kuja kuuza sura hapa yeye hana, yeye yupo serious na kazi. (Kicheko/Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, nimesoma hotuba yake ya bajeti yote, jamani Wabunge naomba mnisikilize. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenisongole wewe ndiye unayechangia, endelea kuchangia kiti kinakufuatilia.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay*, ahsante.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa, karibu.

**T A A R I F A**

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji, akinamama wanaoletwa hapa Bungeni wanakuja kwa heshima zote, ni walezi wa familia, wanajaliwa na hawa waume na hawa wanawake na ndio maana wanaletwa hapa, hawaji hapa na wala hawaletwi hapa kwa ajili ya kuuza sura. Haya ni matusi makubwa sana kwa wanawake,

naomba arekebishe maneno yake, maneno ya hovyo kabisa haya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Mayenga, ni taarifa au unataka afute maneno yake.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, afute.

**MWENYEKITI:** Nazungumza na Mheshimiwa Lucy Mayenga, kiti kikizungumza unanyamaza.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, arekebishe maneno yake *Hansard* ikae sawa, haiwezekani wanawake wanaokuja hapa Bungeni, ikaonekana wanakuja kuuza sura.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Mayenga ulitumia taarifa, kwa hiyo Mheshimiwa Mwenisongole taarifa unapokea?

**GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona Mheshimiwa Lucy Mayenga hajanielewa, mimi nimempongeza January Makamba, yeye alichokisia…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kufuatia kauli aliyotoa mchangiaji ambayo ni ya maudhi, wakati anachangia amempongeza Waziri

wa Nishati, lakini ameenda mbele zaidi akadhihaki kwa kusema kwamba Mawaziri ambao wanawaleta wenza wao hapa wanawaleta kuja kuuza sura na hawapo *serious.* Sasa kanuni zetu zinakataza lugha za kuudhi kwa hiyo ningependa mzungumzaji afute kauli, hiyo kauli aliyotoa ambayo inaudhi na inakera. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko amesimama kwa kifungu cha Kuhusu Utaratibu, Kanuni ya 75 bila shaka inayotaka kufahamu ni kanuni gani ambayo imevunjwa maana ndio msingi wa kifungu hiki. Labda nikusomee: "Mbunge yeyote anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno "kuhusu utaratibu" ambapo Mbunge yeyote ambaye wakati huo atakuwa anasema atanyamaza na kukaa chini na Spika atamkata Mbunge aliyedai utaratibu ataje Kanuni au sehemu ya Kanuni iliyokiukwa".

Mheshimiwa Esther Matiko ni kanuni gani imekiukwa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 71(1)(j).

**MWENYEKITI:** Kanuni ya 71(1)(j) inayosema lugha za kuudhi ni pamoja na hatatoa lugha ya matusi au ishara inayoashiria matusi au kumsema vibaya Mbunge au mtu mwingine. hatotumia lugha ya kuuzi au inayodhalilisha watu wengine.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes,* 71(1) (j).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Mwenisongole amesimama Mheshimiwa Matiko hapa kukutaka ufute maneno uliyotumia ya kutambulisha kwa sababu tunao

utaratibu Bungeni hapa wa kuruhusu wageni mbalimbali kuja wakiwemo viongozi pamoja na wanaoambatana na viongozi wenzetu. Kwa hiyo kuwaita waanauza sura ni maneno yasiyofaa, kwa hiyo futa maneno yako hapa ili uendelee kuzungumza. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafuta kauli ya kuuza sura, lakini nabaki na msimamo wangu wa kumpongeza Mheshimiwa Waziri…

**MWENYEKITI:** Sasa sikiliza Mheshimiwa Mwenisongole, ukifuta ukasema lakini nitakukalisha usiendelee kuzungumza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa nafuta kauli. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, endelea kuchangia.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

La pili nampongeza Mheshimiwa Waziri, nimesoma hotuba yake yote ya bajeti, katika hotuba yake ya bajeti kwa mara ya kwanza tangu nimekuwa Mbunge asilimia 99 ya fedha anazoomba zote zinakwenda kwenye miradi ya maendeleo, sijawahi kuona hiki kitu, ni asilimia moja tu ya bajeti yote ya Wizara ya Nishati inakwenda kwenye matumizi ya kawaida. Hiki ndicho ambacho sisi na Watanzania tunataka kukiona, hiki ndio kilio cha Watanzania kuona fedha za wananchi nyingi zinakwenda kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kaka yangu January, Mheshimiwa Waziri nina mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Serikali ili ilisaini mkataba wa *REA* na wakandarasi mwezi Juni, mkataba wa miezi 18 na sisi kama Wabunge na wananchi wote tulifurahi tukiamini kwamba vijiji 3,448 vilivyobaki kwenye mpango wa *REA* vinakwenda kumalizika na kwa mara ya kwanza umeme utafika katika vijiji vyote Tanzania. Hata hivyo, cha kusikitisha hawa wakandarasi hawa ambao kwa kweli sijui wamepata wapi hiyo jeuri, waliposaini mkataba wa miezi 18 walipewa miezi sita, hiki kipindi kinaitwa *mobilization period* na walilipwa 25 *percent* ya gharama yao, wakaambiwa *mobilization period* ni kipindi ambacho mkandarasi anatakiwa afikishe vifaa vyote *site* au ahakikishe vifaa na taratibu zote zimefika *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo vifaa ambavyo mkandarasi wa *REA* anavihitaji ni nguzo, *transformer*, LUKU na nyaya ambavyo vyote vinazalishwa hapa nchini. Kwa mshangao hawa wakandarasi mwaka huu mwezi Machi wanatuambia vifaa vimepanda, kwamba umeme wa *REA* hauwezi kuendelea kwa sababu gharama za vifaa zimepanda, lakini cha kushangaza hata Waziri naye anakubaliana na sababu hizi ambazo hazina mashiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walikuwa wapi katika kipindi cha *mobilization period* kupeleka vifaa kwanini wasiseme kipindi hicho, Miezi sita wao kupeleka vifaa *site* imefika, leo hawawezi kuja wakatuambia umeme wa *REA* umeshindwa kufika kwa sababu vifaa vimepanda, hivyo vifaa vimepanda mwaka huu. Kwa hiyo, ni kwamba maamuzi ya Waziri kukubaliana na hizi hoja za Wakandarasi si sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ya CCM imeahidi umeme utafika vijijini kufikia Disemba, vilevile Mheshimiwa Waziri katika hotuba yako hujatuambia sasa umeme huu wa *REA* utaisha lini na hawa Wakandarasi wanadai kiasi gani sasa za kupanda. Pia katika majadiliano na Wakandarasi si kuna kitu kinaitwa *variation* ambayo mnaweza mkakaa na Wakandarasi mkajadiliana *variation* ambayo imepanda, hata ukiangalia bidhaa zote za hawa Wakandarasi wanazozihitaji zinazalishwa hapa nchini! Sasa *transformer* zipi, nyaya zipi, *LUKU* zipi au nguzo zipi zimepanda kiasi cha kusababisha huu mradi wa *REA* usiendelee? Kwa kweli ni jambo ambalo inabidi tuwe makini sana na Wakandarasi *otherwise* watatuletea historia ya mtu na Ngamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngamia alikwenda kwa mtu mmoja akamuomba aingize mguu, yule mtu akamkubalia baadaye akasema naomba niingize na kichwa yule mtu akamkubalia, mwisho wake ngamia akaingia nyumba nzima akatoa! Tukiendelea kuwakubalia Wakandarasi kwa kila hoja wanayokuja hatutaweza kufanikisha kufikisha umeme vijijini, huu ni udhaifu ambao unataka kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine cha mwisho wananchi tunaotoka maeneo ya mpakani tunayo *advantage* ya kufaidika na bidhaa zinazouzwa bei ya chini upande wa pili wa mpaka. Kwa mfano, sukari imepanda Tanzania lakini ukienda Zambia ipo chini, mafuta ya kula yamepanda huku ukienda Zambia yapo chini na vitu vya namna hiyo, lakini cha kushangaza sasa gharama hizi za mafuta ambazo zimepanda Mkuu wangu wa Mkoa yeye ameunda *taskforce* kupambana na wananchi wanaokwenda Zambia kuchukua vitu kwa

bei nafuu wanasema hao ni walanguzi, sasa mimi nilitegemea angeunda *taskforce* kupambana na wafanyabiashara wasiowaaminifu ambao wanapandisha vitu ambavyo havihusiani hata na bei ya mafuta. Mimi niiombe Serikali itoe kauli kwa Wakuu wa Mikoa wote ambao maeneo yao yanapakana na nchi za Jirani, wananchi wana-*advantage* ya kuishi maeneo ya mpakani waruhusiwe kwenda kufuata bidhaa nje kwa bei nafuu, hawa siyo walanguzi! Mtu akienda akichukua kilo kumi kwa sababu anachukua kilo kumi au ishirini kwa sababu hataki kwenda kila siku kununua sukari, kwa hiyo anachukua nyingi ili haifadhi na anamchukulia na jirani yake, lakini sasa tukisema kila mtu anayekwenda kufuata vitu vya bei nafuu ni walanguzi hii tutakuwa hatuwatendei sawa wananchi wanaoishi mipakani. Naomba Mheshimiwa Waziri uliangalie kwa sababu Nishati ya Mafuta imepanda na imesababisha vitu vingi kupanda. Kwa hiyo, niombe hili suala ambalo jingine ambalo wananchi tunaoishi maeneo ya mpakani tunahitaji kuwa na hiyo *advantage*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo Mheshimiwa Waziri mimi nitaunga mkono hoja pale nitakapopata maelezo ya kutosha kwa nini tunawapa kichwa hawa Wakandarasi na sababu zao ambazo hazina msingi za kutuambia kwamba vifaa vya *REA* vimepanda wakati havijapanda na vyote vinapatikana hapa nchini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nafikiri ulikuwa unamaanisha ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti siyo Mheshimiwa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, nilimuita Mheshimiwa Ditopile huyu atachangia jioni, Mheshimiwa Maimuna

Mtanda wakati huo Mheshimiwa Isack Francis Mtinga pamoja na Mheshimiwa Hassan Kungu, anajiandaa.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii nami niweze kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan kwa kutoa ruzuku kwenye mafuta, fedha zile ambazo amezitoa ambazo angalau zimeshusha kidogo bei ya mafuta hapa nchini tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati pamoja na timu yake kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya ninawaomba wazidi kuongeza nguvu ili tuweze kuyaona manufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia suala la gesi asilia. Mtwara *Gas Plant* ina jumla ya visima 11 ambavyo vinauwezo wa kuzalisha *megawatt* 22 za umeme kwa siku. Lakini kati ya visima hivyo visima Tisa ni vya muda mrefu ni vya kati ya 2006 na 2007 na *life span* ya mashine hizo ni miaka 10. Kwa hiyo, utaona kwamba muda wa mashine hizo umeshapita kiasi kwamba uzalishaji wa umeme umekuwa ni wa chini sana. Tunaomba Wizara ijipange kutafuta *replacement* ya vile visima Tisa ambavyo ni vya muda mrefu ambavyo pia vinaiingizia Serikali gharama kwa sababu ya matengenezo yasiyoisha kwa sababu muda wake pia umeshapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka kupata *commitment* ya Serikali ni lini mradi wa *megawatt* 300 ambao unatakiwa kwenda kujengwa kule Mtwara

utaanza? Nimeona kwenye hotuba ya Waziri imewekwa lakini hii si mara ya kwanza inawekwa, imewekwa muda mrefu sana kila wakati inawekwa lakini haitekelezwi. Kwa hiyo, tunaomba Waziri atakapokuja kuhitimisha atuambie ni lini hasa ujenzi wa *megawatt* 300 Mtwara utaenda kuanza kwasababu unafaida kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa Mtwara haujatulia, umeme unaofika Mtwara ni mdogo, pamoja na Mtwara tunazalisha gesi lakini umeme wetu unaoingia pale ni mdogo sana unakatika kila wakati. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri atuambie ujenzi halisi wa *megawatt* 300 utaanza lini Mtwara? Anapokuja kuhitimisha hotuba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane pia na mzungumzaji aliyepita aliyezungumzia suala la *REA* katika maeneo yetu. Ni kweli kabisa Wakandarasi wa *REA* walipewa kazi ile mwaka jana kati ya Agosti na Septemba, kipindi kile mfumuko wa bei haukuwa mkubwa kama ulivyo sasa hivi, mfumuko umeanza karibuni, sasa wanakuja na kisingizio cha kwamba vifaa vimepanda bei, walikuwa wanafanya nini kipindi chote ambacho kimepita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Jimbo la Newala Vijijini kwa mfano, ambako mkandarasi anayeitwa *Central Electrical International Limited* amepewa kazi ya kuweka umeme katika Jimbo la Newala Vijijini, Newala Mjini, Tandahimba, Newala lakini Mkandarasi yule kwakweli tumechoka kwa sababu ufanyaji wake wa kazi haueleweki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Jimbo la Newala Vijijini, Vijiji 107 ndivyo ambavyo vipo kwenye Jimbo lile

lakini ni vijiji 33 tu ndivyo vyenye umeme, Mkandarasi amepewa *scope* ya kazi anaifahamu lakini ninavyoongea sasa hivi amefika Kata mbili tu ambazo zina vijiji 11 hali ambayo inatia wasiwasi kwamba je, ikifika Desemba 2022 kweli atakuwa amemaliza vijiji vyote 74 ambavyo havina umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri nakuomba Kaka yangu msimamie Mkandarasi aliyepewa kazi Mtwara, Tandahimba, Nanyamba na Newala afanye kazi kwa juhudi ikiwezekana usiku na mchana, kwa sababu watu tupo gizani, lakini umeme huu unamanufaa makubwa sana kama utawafikia wananchi wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanashindwa kujiajiri kwa sababu hawana umeme, kungekuwa na umeme wangeuza *ice-cream,* wangechomea ma-*gate* wangefanya kazi mbalimbali lakini wanashindwa kwa sababu umeme haupo. Nasi tumeahidi katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi kwamba tutaongeza ajira zipatazo zaidi ya 8,000 kufikia 2025 lakini ajira hizi zingine zinatokana na sekta binafasi ikiwemo hii ya umeme kwamba vijana wangeweza kujiajiri wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba sana Waziri wetu asimamie umeme ufike kwenye vijiji kupitia *REA* ili wananchi wale nao waweze kunufaika waone matunda yanayotokana na kazi ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo maeneo niliyotaja ambayo yapo gizani yanapakana sana na nchi jirani nchi ambayo hali yake tunaifahamu, nimeshaongea hapa umeme huu si *luxury* umeme ni ulinzi ukiondoa suala zima

la kazi lakini umeme ni ulinzi utatulinda kwa kuwepo kwake. Kwa hiyo, tunavyofanya hawa Wakandarasi waliopewa kazi wanaenda polepole wanahatarisha usalama wa raia wa maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo umeme unaofika maeneo ya Mtwara na Lindi ni mdogo sana, kule tunafahamu kabisa kwamba ndiko gesi asilia inakotoka kwa wingi kutoka kule Msimbati, Songosongo gesi hii inaenda kuchakatwa Kinyerezi inarudishwa kule. Kwa hiyo, umeme taunaopata ni mdogo sana. Tulitaraji miradi hii wananchi wanaotoka katika maeneo yale wai-*own* wao wenyewe kwa maana ya kwamba waone manufaa yanawafikia moja kwa moja. Tuliambiwa kwamba watapata umeme wa majumbani lakini kiasi ambacho kimefika cha matumizi ya umeme majumbani ni kidogo sana, ni kidogo mno na sijui mradi ule umeishia wapi kwa sababu ulikuja mara moja tumeona kimya mpaka leo. Naomba sana Serikali kupitia Waziri mjipange muhakikishe umeme huu unawafikia wananchi wa Lindi na Mtwara, waone manufaa ili wawe walinzi wazuri wa miradi hii kwa sababu inatoka kule kwao watusaidie kulinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni gridi yetu ya Taifa umeme huu ukienda unaishia Tunduru Gridi ya Taifa kule ipo Tunduru, kwa hiyo, umeme unaofika Masasi kupitia gridi ya Taifa hauna nguvu. Niombe sana Serikali ione uwezekano wa kujenga *sub-station* maeneo yale ya Masasi ili wananchi waweze kupata umeme wa uhakika kwa sababu kuna kukatika katika sana kwa umeme kutokana na umbali unakotoka umeme hadi kuwafikia walaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja lakini Mheshimiwa Waziri anapokuja aje na majibu ambayo nimeyaomba niyasikie anatujibuje. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maimuna Mtanda kwa mchango wako. Nilimuita Mheshimiwa Isack Francis Mtinga ili aweze kuchangia.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuchangia Wizara hii ambayo ni *engine* ya maendeleo ya nchi yetu. Kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri na Naibu wake vijana hawa, ukisikiliza hata hotuba yao imesheheni na imeshiba mambo ambayo wananchi yakifanyika hakika tutafika mbali katika sekta hii ambayo ni *engine* ya maendeleo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nianze mchango wangu kwanza na Jimbo langu la Iramba Mashariki Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama. Katika suala zima la bei za kuvuta umeme kwa mara ya kwanza. Wilaya zetu hizi ni mpya kwa mfano, Wilaya yangu ya Mkalama ni Wilaya mpya. Wilaya kama Wilaya inapotamkwa kwamba ni Wilaya mpya ni kwa sababu tu ya utawala lakini maisha ya wananchi ni maisha ambayo bado ni ya kijijini na uwezo wao ni mdogo, sasa hili suala la kwamba kwa sababu ni Makao Makuu ya Wilaya lakini vilevile kuna Miji Midogo tu iliyochangamka tu kwa mfano, Mji wa Iguguno. Iguguno ni Mji mdogo sana ambao haujawa Mji rasmi lakini kwa sababu tu pamechangamka tayari *TANESCO* wanasema kwamba eneo kama hili watavuta umeme kwa 320,000 sasa lengo la Serikali la kufikisha umeme kwa wananchi katika maeneo kama haya kwa bei hizi linakuwa si rahisi kulifikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri Wizara iangalie namna nyingine yakufanya *assessment* nani avute umeme kwa 320,000 na nani avute umeme kwa Shilingi 27,000 tusitumie maeneo tu kwamba kwa sababu ni Wilaya kwa sababu ni Mji lakini wananchi wanaoishi katika mazingira haya katika maeneo haya, maisha yao ni ya chini sana, ni maisha ya kijijini. Kwa hivyo suala la kusema kwa sababu pamechangamka tu kwa mfano pale Iguguno watu wavute umeme kwa 320,000 wananchi wengi wataendelea kuishi bila umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye Wilaya hizi mpya kama Wilaya ya Mkalama ukifika pale Nduguti Makao Makuu ya Wilaya, kwa sababu tu kuna jengo la halmashauri nanini lakini maisha ya wananchi wa kawaida ni maisha ya kijijini kabisa. Kwa hivyo, mimi ningeomba kabisa suala hili la kuvuta umeme kwa 320,000 na hii 27,000 Wizara iangalie namna nyingine ya kufanya *assessment* nani avute umeme kwa njia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika suala zima la hizi *tariff* za umeme kuna hii *tariff* ya D1 ambayo ni kwa ajili ya wananchi wa chini unalipa Shilingi 10,150 unapata *unit 75*, *TANESCO* wamekuwa hawatoi elimu vizuri kuhusu hii *tariff* inakuwa kama vile inawategea tegea wananchi, kwamba ukinunua huu umeme wote unapata *unit* 75 unatumia kwa mwezi mzima, hasa haitoi elimu matokeo yake wale wananchi wananunua umeme kidogo kidogo mwisho unaisha kabla ya mwezi inabidi anunue tena, sasa anakuja anatolewa na *system* kwenye hii *tariff* na akitolea anakwenda kwenye gharama kubwa zaidi. Kwa hiyo, mimi ningeiomba *TANESCO* watoe elimu kwa wananchi kuhusu hii D1 ya malipo ya umeme ili wananchi waweze kujua masharti yake waweze kufaidika nayo,

kwa sababu lengo la kuiweka hii nikuwasaidia wananchi wa chini waweze kutumia umeme vizuri na waweze kupata umeme na waweze kulipa *bill* zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nataka pia niupeleke kwenye bomba la gesi. Bomba hili limetumia fedha nyingi sana mpaka kufika pale Dar es Salaam, mpaka sasa asilimia karibu 50 ya matumizi ya bomba hili ni matumizi ya kuzalisha umeme na tunakuja na miradi mikubwa kama Nyerere *Hydro Power* na mingine mingi Waziri ameisema kwenye hotuba yake, kwamba tutakuwa na umeme mwingi sana wa maji ambao ni umeme *cheap*. Kwa hiyo, nina hakika baada ya muda fulani *TANESCO* haita-*opt* kutumia gesi kuzalisha umeme kwa sababu watakwenda kwenye umeme wa maji ambayo ni rahisi. Sasa naamini kabisa baadaye hili bomba litakuja kuwa *white elephant* kwa sababu litakuwa limekaa pale na matumizi makubwa ni kuzalisha umeme na sasa tunakwenda kwenye umeme wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu Waziri amesema miradi mingi sana mikubwa ya mabilioni ya fedha lakini sijaona akigusia suala la kusambaza bomba hili kutoka Dar es Salaam kuelekea Mwanza ili lipite kwenye miji hii na bomba hili likipita maana yake likitoka Dar es Salaam kwenda Mwanza, maana yake litapita Pwani, litapita Morogoro, litapita Dodoma, litapita Singida, litapita Shinyanga mpaka kufika Mwanza na litakapopita huku, sasa litasambazwa kwenye nyumba kuweza kutumia gesi kwenye nyumba zetu na hapo sasa tutakuwa tumetumia vizuri fedha nyingi ambazo zimetumika katika kutengeneza bomba hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakoelekea bomba hili halitatumika kwa sababu umeme tutakwenda kwenye

maji na huo umeme wa maji ni mwepesi. Kwa hiyo, ningeshauri wizara katika miradi yake mikubwa ya mabilioni iliyoiweka suala la kutoa bomba hili Dar es Salaam na kulipeleka Mwanza liwekwe kama kipaumbele ili gesi hii iweze kutumika. Nimesikia kwenye hotuba yake amesema kutakuwa kuna vituo vile vya kupeleka gesi huku kwa kutumia vile vituo ambavyo gesi tutajaza kwenye magari na nini, najua imeenda kwenye *private sector* lakini itakuwa na gharama ikianza hivyo si mbaya, lakini Serikali iangalie jinsi ya kulitoa hili bomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile walaji wakubwa wa mkaa ni watu wa mijini kwa hiyo, bomba hili likipita hata mazingira yetu yatakuwa salama kwa sababau wananchi watatumia gesi hii kwenye nyumba zao na hivyo mazingira yatakuwa salama na tutaokoa gharama kubwa sana ambayo inatumika kulinda mazingira ya nchi yetu. Kwa hiyo, ningeomba Wizara ya Serikali kwa ujumla iangalie suala la kulitoa hili bomba Dar es Salaam na kulipeleka Mwanza kwa maana lipite kwenye mikoa mingi ili tuweze kutumia vizuri hii gesi ambayo Mungu ametujalia na Serikali imetumia fedha nyingi kuitoa huko iliko mpaka kufikisha Dar es Salaam, sasa iende kwenye matumizi ya wanatanzia ili iweze kuokoa maisha ya Watanzania iweze kuokoa mazingira yetu na hakika kama tukifanya hivi maisha yetu yatakuwa bora sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilipenda niseme katika mambo haya lakini nikupongeze sana Waziri, hotuba yako ni nzuri tuombe tu kwamba fedha zifike ili haya ambayo yameanza kutekelezwa yatekelezwe na ili nchi yetu iweze kufika mahala pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimuita Mheshimiwa Hassan Kungu wakati huo wafuatao wanajiandaa; Kwanza ni Mheshimiwa Daktari Jasson Samson Rweikiza, Pili Mheshimiwa Phillipo Mulugo na watatu ni Mheshimiwa Daktari Florence Samizi.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye hotuba hii ya Nishati. Kwanza kabisa nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoweza kufanya kazi iliyo bora na iliyotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa sababu ametupunguzia maswali mengi na ametufanya tuelewe vitu vingi kwa wakati mmoja. Kile kitendo alichokifanya cha yeye kuwaleta wataalam hapa, pamoja na Mameneja wa Wilaya zote, maana yake ni kwamba pale ametupunguzia muda wa kwenda kuwafikia hawa watu wote, lakini pia naamini wazi kuwa imepunguza maswali mengi na hata vilevile michango haitakuwa mingi sana kutokana na jambo lile alilolifanya. Kwa hiyo, ni pongezi kubwa kwake na natamani hata Wizara nyingine zingefanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja niende kwenye mchango wangu, kwenye Jimbo langu ama Wilaya ya Tunduru. Wilaya ya Tunduru tunapokea msongo wa umeme wa kilovoti 33 kutokea Songea Mjini na umeme ule unasafiri kwa kilomita 260. Kama unasafiri kwa

kilomita 260 maana yake ni kwamba huku njiani kote umeme huo unatumika na tunautumia kwa Wilaya mbili, kwa maana ya Wilaya ya Namtumbo na Wilaya ya Tunduru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inapotokea hitilafu Namtumbo maana yake ni kwamba Namtumbo wanakosa umeme na sisi Tunduru tunakosa umeme pia vilevile. Kwa hiyo, jambo hili limepelekea umeme wa Tunduru kukatikakatika mara nyingi sana na tunapata adha kubwa mno. Ulifikia wakati kwa siku umeme unakatika mara 12 mpaka mara 17. Wakati mwingine unaweza ukakatika siku nzima umeme usipatikane. Wakati mwingine tunalala na giza usiku kucha. Lakini ukiuliza ni kwamba unakuta hitilafu imetokea Namtumbo, kwa hiyo, mpaka wenzetu wa Namtumbo washughulikie hitilafu hiyo ya umeme ndipo na sisi Tunduru tuweze kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya adha hiyo kubwa, tarehe 4 Septemba mwaka jana niliweza kuuliza swali la msingi hapa ambalo Wizara kama inaweza kutujengea *substation* ya kilowati 132 pale Tunduru. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hii aliweza kujibu kwamba watatuletea ama watatujengea mradi huo wa kilowati 132 pale Tunduru na alisema ataingiza kwenye mpango huu ili sasa Tunduru tuweze kupata hiyo *substation* na tuondokane na tatizo hili la kukatikakatika kwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa nimepitia mpango huu mara mbili, mara tatu, sijaona kabisa hilo jambo kama limeingizwa kwenye huu mpango. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, anipe *commitment* ama aseme na wananchi wangu wa

Tunduru kule wasikie kama ni kweli huu mradi upo ama haupo, kwa sababu tuliambiwa utaingizwa kwenye huu mradi lakini sijaona kama umeingizwa kwenye huu mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aniambie ni kweli huu mradi utatekelezwa kwa kipindi hiki? Kama utatekelezwa je, ni lini utaanza huu mradi? Naomba pia utakapotekelezwa huu mradi ama utakapoanza kujengwa huu mradi, niombe sana utakapokuwa unatoka Songea kuja pale Tunduru Mjini, basi zijengwe njia tatu za usambazaji. Njia ya kwanza irudi Hulia, njia ya pili iende Nanyumbu Masasi na njia ya tatu itumike palepale Tunduru Mjini. Hapo Waziri atakuwa ametusaidia sana na tatizo hili litaenda kwisha kabisa na Mheshimiwa Waziri tutampongeza mno na tutamwombea aendelee kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kutokana na ukubwa wa Wilaya ya Tunduru ilivyo, tunahitaji angalau tupate *sub office* nne ambazo hizi zinaweza kufanya kazi kwa urahisi, kuwafikia wadau wa umeme kwa urahisi kutokana na eneo lenyewe namna lilivyokuwa kubwa. Kwa hiyo, *sub office* hizi zipatikane nne ambazo zitakuwa na ikama za kiofisi zilizokamilika. *Sub office* moja ijengwe Milonde, ya pili iwe Nakapanya *sub office* na ya tatu iwe Nalasi *sub office* na ya nne iwe Lukumbule *sub office*. Kwa kufanya hivyo maana yake ni kwamba tutakwenda kusaidia kwa haraka matatizo haya ya umeme kwisha katika Wilaya ya Tunduru kutokana na kwamba jiografia ya Tunduru ni kubwa mno. Kwa kutumia ofisi moja tu na wana gari moja tu, kukitokea changamoto tatu kwa siku moja maana yake ni kwamba wanawafikia wananchi kwa ugumu mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, nataka nishauri kwamba hizi transfoma zinazojengwa kwenye vijiji lazima tuziangalie kwa umakini ama tuangalie namna ya kufanya, kwa sababu zile transfoma zinazidiwa haraka sana na wateja wa umeme kwa sababu zina *KVA* 50. Kwa hiyo, kama zina *KVA* 50 maana yake ni kwamba kama zina wateja wengi inazidiwa kwa haraka na kunatokea tatizo tena la kukatika kwa umeme. Kwa hiyo, nashauri badala ya kufunga transfoma za *KV* 50 basi zifungwe transfoma za *KV* 100 na kama siyo hivyo basi kwenye kijiji kimoja zifungwe transfoma mbili, tatu na kuendelea kulingana na ukubwa wa kijiji chenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Hassan Kungu kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Dkt. Jasson Rweikiza aweze kuchangia.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie Wizara hii muhimu ya Nishati. Nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri January Makamba, Mheshimiwa Naibu Waziri Stephen Byabato na watumishi wote wa Wizara, viongozi na watumishi wa taasisi mbalimbali chini ya Wizara, *REA* na nyinginezo kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru pia kabla sijasahau, jambo la juzi la kutuletea wataalam hapa Bungeni wa *TANESCO, REA* na mashirika mengine lilikuwa ni jambo muhimu sana na zuri sana. Ahsanteni sana.

Tumezungumza na wale watu, wametusaidia matatizo yetu kwenye majimbo na kasi imeongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka nizungumzie umeme na nizungumzie umeme Bukoba Vijijini. Kama walivyosema wenzangu umeme ni suala la maendeleo siyo suala la anasa, ni tija ya maendeleo, ni uchumi, umeme ni siasa kwa sisi ambao tuko kwenye siasa, unatusaidia mambo mengi yanakwenda, yanasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pale Bukoba nishukuru kwanza kwamba kasi ya maendeleo ya umeme ni kubwa ni nzuri lakini kuna tatizo kubwa sana. Bukoba na Kagera nzima kama walivyoongea wengine hapa wachache, umeme unazimika sana, ukiamka asubuhi ukakuta umeme unawaka, utakuwa na bahati kama utafika saa nne haujazimika. Saa sita utazimika tena, kwa siku unazimika mara nane, mara 10 au mara 20. Kwa hiyo, inakuwa ni matatizo makubwa na kama una kiwanda kidogo hutaona tija yoyote, itakuwa ni hasara kubwa kuwa na umeme kwenye kiwanda chako. Kama una taa zako zitaungua, kama ni *fridge* itaungua na vitu vingine vya umeme, unakuwa huna tija na umeme huo kwa sababu umeme unazimikazimika mara nyingi sana kwa kutwa moja usiku na mchana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu inafahamika, sababu ni kwamba umeme wa Bukoba unatoka Uganda tunaununua nchi jirani ya Uganda. Uganda wenyewe wana shida ya umeme, wana mgao. Kwa hiyo, wanapoleta umeme Bukoba ni umeme kidogo kuliko mahitaji yaliyopo na Kagera kwa ujumla. Kwa hiyo, wakipunguza kidogo, basi umeme unazimika kwenye maeneo yetu. Sasa mfumo, ile gridi ya Taifa imekaribia

kufika kwenye maungio kule Bukoba, umeshaingia mkoani nafikiri uko sehemu za Muleba au nyuma kidogo pale. Naomba Wizara ifanye kazi kubwa ya kuongeza kasi kusudi mfumo huu, gridi ya Taifa iunganishwe na Mkoa wa Kagera tuondokane na umeme wa kutoka nchi jirani ambao hautoshi, matokeo yake ni kuzimika umeme mara kwa mara, hivyo, inakuwa shida kubwa sana kwa watumiaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nashukuru kwanza, kwamba kasi kama nilivyosema ya kufunga umeme kwenye vijiji mbalimbali ipo. Pale kwangu kuna vijiji vingi ambavyo havijapata umeme, Kijiji cha Buzi, Kijiji cha Buguluka, Kijiji cha Musira, Kijiji cha Butakya, Bituntu, Sheshe, Lukoma na vingine vingi, lakini kasi ipo, machimbo yamechimbwa na tunaanza kuwa na matumaini kwamba umeme utafungwa, nashukuru kwa hilo. Hata hivyo, tusifikiri kwamba kwa kufunga umeme kwenye vijiji hivi na vile ambavyo vimeshafungwa tayari, tumepiga hatua kubwa sana, bado kabisa, bado kabisa, vitongoji vingi vingi havina umeme, watu wengi sana hawana umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta kijiji kizima nitakusomea mifano hapa michacho ya kata mbili. Kuna Kata moja inaitwa Kyamulaile. Kata ya Kyamulaile ina vijiji vinne, kijiji Omkihisi kina kaya 490 ni kaya 10 tu zenye umeme. Kijiji cha Kyamulaile yenyewe ina kaya 863, kaya zenye umeme ni 38. Nina Kijiji Mashule, kina kaya 1,085, kaya zenye umeme ni sifuri, hata moja yenye umeme hakuna, lakini kwenye mtandao wa *TANESCO* na *REA* wanahesabu na hiki kijiji kina umeme wamekimaliza. Kaya yenye umeme sifuri, walifunga umeme kwenye chanzo cha maji pale wakaondoka. Wananchi wote, kaya zote hazina umeme. Kata ya Nyakibimbili, Kijiji cha Bundasa

kina kaya 610, kaya zenye umeme 19. Kijiji cha Bugengele, tuna kaya 368, kaya zenye umeme 28. Kijiji cha Kitaya kuna kaya 330, zenye umeme kaya 27.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo inaonesha kazi ya kufunga umeme bado ni kubwa sana, tunahitaji msukumo mkubwa wa *REA* wa *TANESCO* kuongeza kasi. Tusifikiri kwamba kufunga vijiji vyote kama tunavyoambiwa Desemba walikuwa wanafunga vijiji vyote kazi imeisha, kazi bado ni mbichi kabisa, ni kubwa. Mbaya zaidi kule Bukoba wanapokwenda kufunga umeme kwenye kijiji kingine au kitongoji fulani wanapita juu ya nyumba za watu. Juu kuna waya za umeme, chini nyumba hazina umeme, sasa nafikiri kwamba ni rahisi ukishafika pale wateremshie watu umeme ambao wamepitiwa na zile waya ili nao wapate matunda ya kupitishiwa pale waya hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia unafyeka mazao yao, sisi kule mazao yetu ni kahawa na migomba, wanafyeka, yote wanatoa, mtu ana nusu heka, yote inafyekwa, lakini hapati umeme. Sasa unashangaa huyu mtu kwa nini wanamuadhibu na umeme hawampi. Kwa hiyo, nafikiri kwamba ingekuwa bora sana hawa nao wafikishiwe huduma ya umeme kama ambavyo wanapelekewa wale wengine ambao wanapitishiwa pale juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Jasson Rweikiza kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Phillipo Mulugo wakati huo Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi anajiandaa.

Haya tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi wakati huo Mheshimiwa Halima Mdee anajiandaa. *(Makofi)*

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu sana. Nami nianze kwa kumpongeza Rais wetu, Mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anaendelea kujali maisha ya Watanzania na kipekee kwa jinsi ambavyo ametoa pesa kwa ajili ya kupunguza makali ya bei ya mafuta. Niwaombe watendaji bei hii iwanufaishe watu wote na siyo wa mijini tu. Kwa sababu tayari kumeshakuwa na malalamiko kwamba huko kwetu vijijini imepungua Sh.150. Naomba taasisi husika tulifuatilie kwa sisi tunaotoka vijijini ili keki hii basi wote tuweze kufaidika sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Waziri wa Nishati na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii. Kipekee pia nimpongeze Mkurugenzi wa *REA* kwa kazi nzuri anayofanya, lakini na Mkurugenzi wa *TANESCO,* ndugu yetu Maharage Chande ameanza vizuri, amekuja na mikakati mizuri tunaiona, Nikonekt, Mita Janja tunaamini zitaenda kuondoa changamoto kubwa tulizokuwa nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama katika Bunge hili mwaka jana kama sasa ambapo Jimbo langu la Muhambwe lilikuwa lina vijiji sita tu vilivyowekewa umeme, lakini leo nisimame kuishukuru Serikali na kuipongeza kwamba kwa sasa nina vijiji 25 ambavyo vimefikiwa na umeme. Hii ni kazi nzuri inayofanywa na Shirika letu la *REA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ninavyo vijiji 15 ambavyo hivi vinatakiwa kuwekewa umeme kwa sababu vimeshapelekwa nguzo lakini vimekumbwa na hii changamoto ya nyaya, *MV* na *LV* imekuwa ni changamoto. Tunaambiwa *low voltage* na *medium voltage* imepanda bei. Niombe Wizara, niombe Serikali iingilie kati hili suala la wakandarasi kukosa hizi nyaya. Vijiji vyangu hivi 15 ukivipa hizi nyaya vinaenda kuwashwa umeme, nitakuwa na vijiji 40, hii ni *quick win.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jitihada za makusudi zichukuliwe kabisa kuhakikisha tunapata hizi nyaya kwa wananchi wangu ambao katika Jimbo la Muhambwe ambao wamesubiri umeme kwa muda mrefu sana. Maana vijiji hivi ni utekelezaji wa *REA* awamu ya III, mzunguko wa kwanza, maana tulipitia changamoto kubwa, naomba jitihada hizi zifanyike kwa haraka ili wananchi waliosubiri umeme kwa muda mrefu wa Muhambwe, Kukinana, Kumsenga, Kwakijina, Lukaya, Magarama, Kumkubwa wanasubiri umeme kwa muda mrefu. Naomba Serikali ichukulie kwa uzito wake ili tuweze kupata umeme katika jimbo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niungane na wenzangu kuhusiana na bei ya kuunganisha umeme. Sisi wananchi wa Muhambwe mradi wetu mzunguko wa kwanza ulichelewa sana, kwa hiyo, hatukufaidika na hiyo shilingi 27,000. Nimpongeze Waziri ameliona hili na amesema ndani ya miezi sita atakuja na jibu zuri. Niombe Jimbo la Muhambwe lipewe upendeleo wa kipekee kwa sababu hatujafaidika na hiyo bei ya shilingi 27,000 ili wananchi wangu waendelee kulipa shilingi 27,000 ili waweze kuunganisha huu umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuiomba Serikali, pamoja na jitihada hizi nzuri bado umeme haujawafikia wananchi. Kipekee niwasemee wananchi ambao wanatumia hizi taasisi mbalimbali ikiwemo taasisi za afya;-mahospitali na zahanati, lakini taasisi za elimu; mashuleni, taasisi za dini; makanisani na misikitini bado ni changamoto kubwa. Naomba *REA* wachukue jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba taasisi hizi zinapata umeme, kwa sababu tunapozipatia taasisi hizi tutakuwa tumewagusa watu wengi kwa wakati mmoja na vilevile tutakusanya mapato zaidi kwa hizi taasisi kwa sababu zina uhakika wa kulipa zaidi. Naomba zipewe kipaumbele cha makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kilio chetu Mkoa wa Kigoma kuunganishwa kwenye gridi ya Taifa. Niipongeze Serikali na kumshukuru Waziri, nimeona kwenye vipaumbele ni kipaumbele cha kwanza kuunganisha Mkoa wa Kigoma kwenye gridi ya Taifa. Namwomba Mheshimiwa Waziri kama walivyotuahidi kwamba mwezi Oktoba, Mkoa wa Kigoma tunakwenda kuunganishwa kwenye gridi ya Taifa, basi bajeti i-*reflect* kile walichotuahidi kwamba kwa bajeti ambayo wametuwekea basi iweze kuunganishwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tutengewe bajeti ya kutosha ili tuweze kuunganishwa kwenye gridi ya Taifa kama walivyotuahidi mwezi Oktoba ili na sisi wananchi wa Mkoa wa Kigoma basi tuanze hizo biashara wenzetu wanazofanya kama za vinyozi, vijana wanasubiri kwa hamu, basi na sisi tuuze soda baridi, tuuze maji baridi, maana yake tumesubiri kwa muda mrefu, naomba lizingatiwe, kama tulivyopewa kipaumbele cha kwanza, basi na pesa pia tupewe mgao wa kutosha kama kipaumbele cha kwanza kinavyoonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali vile vile, mwaka jana tulikuwa na mradi wa kupata umeme kutoka maporomoko ya Mto Malagarasi, megawati 49.5. Nimeona safari hii tumetengewa Bilioni 13. Nichukue nafasi hii kuipongeza na kuishukuru Serikali kwa sababu kupata umeme katika maporomoko ya Mto Malagarasi itakuwa ni suluhisho la kudumu. Naomba tulichukue kwa umuhimu wake ili wananchi wa Muhambwe waweze kupata umeme kutoka katika Mto Malagarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi zote hizi niendelee pia kuipongeza *TANESCO*. Mkurugenzi amekuja na mikakati mizuri, lakini nimepitia taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali. Ili tuweze kulisaidia hili shirika na tuweze kulikwamua hapo lilipo, lazima tulisaidie hili shirika. Shirika hili la *TANESCO* ni kati ya mashirika ya Serikali ambayo yana deni kubwa kuliko mtaji. Hii imeoneshwa kwenye ukurasa wa 36 wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirika hili linadaiwa Tritioni 13.4 na huku likiwa na mtaji wa Trilioni 3.0. Hii ni uwiano wa takribani asilimia 356. Hii ina maana gani? Shirika hili haliko himilivu, shirika hili halijasimama kibiashara. Kwa hiyo, naiomba Serikali iisaidie shirika hili. Tunafahamu katika deni hili liko *principle* na kuko na *interest*. Pia yapo na madeni mengine kama hapa Wabunge wengi wamesema jinsi ambavyo wanadaiwa kwenye gesi, basi Serikali ichukue jitihada za makusudi kulisaidia hili shirika ili tuweze kulipima kwa sababu madeni yao wameyarithi, ni madeni ya miaka mingi, mengine ni ya makaratasi lakini mengine ni kama hayo nimesema ni *interest*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lisaidiwe hili shirika kuweza kulipa hili deni, aidha Serikali ilichukue hili deni au iligeuzwe hili deni liwe mtaji au iipe ruzuku *TANESCO* hasa kwenye hii gesi ambayo matumizi ya gesi ni makubwa takribani Bilioni 40 mpaka Bilioni 50 tumeona *TPDC* wanawadai Bilioni 400 shirika hili haliwezi kwa nini nasema haliwezi, nimepitia mahesabu ya mapato ghafi ya shirika hili, hawa wanakusanya takribani Bilioni 120 hadi Bilioni 150 kwa mwezi ina maana kwa mapato yao hata tukiwaambia wasitumie hizi pesa kwa jambo lolote hili deni watalilipa ndani ya miaka Nane mpaka Tisa, hawawezi kulilipa, Serikali ichukuwe jitihada za maksudi kuisaidia *TANESCO* ili ilipe hili deni au ilichukue hili deni ili *TANESCO* iwe na mtaji mkubwa kwa ajili ya uhimilivu wa shirika hili kuweza kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu umeme ni uchumi, umeme ni siasa na wananchi wanahitaji umeme, wanahitaji kuona siyo kuwaambia na Ilani yetu imewaambia tunakwenda kumaliza kupeleka umeme, sasa tukiwa bado shirika haliko imara hivi basi itakuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao viongozi wazuri wamewekwa pale katika Wizara Waziri, Naibu Waziri na Wakurugenzi wote, kwa hiyo Serikali itawasaidia waweze kufanya kazi zao vizuri na hii itakuwa kipimo kwamba tutaona matokeo chanya haraka kwa ajili ya ufanisi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache naomba kuunga mkono hoja asilimia 100 nikitegemea yale yote niyoyashauri yataenda kutekelezwa kwa ajili ya maslahi mapana ya Jimbo la Muhambwe, ahasante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi. Nilimwita Mheshimiwa Halima Mdee wakati huo Mheshimiwa Anastazia James Wambura pamoja na Mheshimiwa Hamida Abdallah wanajiandaa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi nianzie hapa ambapo ameishia Mheshimiwa Dkt. Samizi kuhusiana na *TANESCO*. *CAG* amesema ni miongoni mwa mashirika yanayoendeshwa kwa madeni, ina madeni zaidi ya mtaji kama ambavyo mwezangu aliyetangulia amesema na katika mashirika 16, shirika la *TANESCO* ni Namba Mbili, deni Trilioni 13, mtaji Trilioni Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jana Mheshimiwa Waziri umesema kwamba haya madeni ya *TANESCO* ni ya makaratasi, sasa ni muhimu kwa sababu hili ni shirika letu muhimu na tunapenda lifanyiwe *reform,* utuchambulie kinagaubaga kiwango kipi ni madeni ya makaratasi, kiwango kipi ni uzembe wa baadhi ya watu na kukosa kuwajibika. Ninasema hivi kwa sababu ukisikia deni linalozungumzwa na *TANESCO* sana ni lile Bilioni 500 la *TPDC*, lakini madai ya *TANESCO* kwa watu wengine nadhani ni kama zaidi ya Bilioni 400. Sasa hapa katikati kuna nini, na anayejua huo mzizi siyo mwingine ni wewe, lakini pili tumeambiwa hivi karibuni na nilikuwa napitiapitia hapa kwenye Mafungu yako nikifikiria kwamba nitaona sijaona, kwamba tunatakiwa kuilipa *Symbion* Shilingi Bilioni 355, kwa sababu gani, kuna jamaa mmoja tu pale *TANESCO* baada ya mkataba wa *Symbion* wakati 2011 na 2013 ulipoisha, yeye mwaka 2015 alisaini mkataba lakini 2016, Tarehe 24, Mei Serikali ikasitisha mkataba. 2017 wenzetu wakaenda Mahakama za Kimataifa, 2019 wakaendelea kwenda Mahakama za Kimataifa 2021

hatimaye Serikali mkakubaliana na *TANESCO* mkaingia mkataba na *symbion* kuilipa Bilioni 325. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tu kuna watu wamefanya maamuzi, ya kuingia mkataba *whether* ilikuwa ni kwa dili ama siyo kwa dili lakini Serikali hiyohiyo na baada ya miezi kadhaa ikasitisha mkataba, halafu Serikali hiyohiyo inakuja inaingia makubaliano na *symbion* kulipa kodi za wananchi Bilioni 355. Sasa unajua kuna wakati unakaa unafikiri hivi hizi hela za Watanzania, hizi pesa za walipa kodi hizi hivi tuna uchungu nazo kweli kama tunavyosema?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali nnamshukuru Mwanasheria Mkuu yuko hapa, majuzi rafiki yangu Mheshimiwa Reuben wa Muheza alisema hivi kwa nini Mawakili wetu Wanasheria wetu hawapelekwi kwenye mafunzo ya kuwa wabobezi kwenye mikataba? Yaani kwenye mambo muhimu pesa hatutengi leo tunaambiwa nchi yetu eti tukamlipe *symbion* Bilioni 355 kwa kuvunja mkataba wa kizembe! Wanasheria wa nchi wako wapi Mwanasheria Mkuu tunaomba majibu haya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo watu wanalia umeme hapa hivi tujiulize tu….

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ndiyo Mheshimiwa wa Mbunge wa Tabora, taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Halima Mdee anapouliza wanasheria wa nchi wako wapi sijui, yeye mwenyewe ni Mwanasheria ameuvua lini uanasheria? *(Kicheko/Makofi)*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee unapokea taarifa?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijatumika tu rafiki yangu, tatizo mkiona tunafunguka mnafikiria sisi ni *enemies* hapana sisi ni Watanzania tunapigania Tanzania hii, kwa hiyo, Wanasheria ninaowazungumzia hapa na waliopewa dhamana na nchi hii kwa kusomeshwa kwa kodi za nchi hii, kusimamia mikataba ya nchi hii, kwamba leo tunaenda kuilipa *Symbion* Bilioni 355. Sasa naamini Mheshimiwa January utakuja kunijibu vizuri kwanza huo mpunga huko wapi maana hapa siuoni kwenye bajeti yako siuoni na kwenye bajeti iliyopita hatukuona.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee kwa hiyo taarifa umeipokea au umeikataa?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeikataa taarifa kwa mantiki niliyoieleza hilo la kwanza. Pili, ningependa kujua vilevile hawa watu wote walioshiriki katika mnyororo hadi Taifa limefika hapa, wanawajibika kiasi gani, wameshachukuliwa hatua, kama hawajachukuliwa hatua, mna mpango gani wa kuchukuwa hatua? Haiwezekani watu 'wanavijikesi' vya hovyo hovyo huko wako ndani, wakati kuna watu wenye kesi makubwa ya uhujumu uchumi tumekaa nao tu

haiwezekani! Huwezi kutofautisha hili jambo uhujumu uchumi, kwa hiyo naomba nipata majibu sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muhtadha huohuo Bwawa la Julius Nyerere, katika mradi ambao Serikali imewekeza asilimia 100 kwa pesa za ndani ni mradi huu kutokana na maandiko yenu, 6.5 *trilion*. Mradi huu ulitakiwa ukamilike tarehe 14 Juni, kwa mujibu wa mkataba wa awali. Leo tunaambiwa umefikia asilimia 57, tunajua kwenye mkataba kuna sura mbili, Mwanasheria Mkuu yuko hapa, kwamba upande mmoja ukiwa na uzembe upande mwingine lazima ufidiwe, ninaomba Waziri ukija kutujibu hapa utuambie hasara ambayo Tanzania imeipata kwa Mkandarasi huyu kutokumaliza Tarehe 14 Juni, tunalipwa kiwango gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya nimesoma taarifa ya Kamati, taarifa ya Kamati ya sasa na taarifa ya Kamati ya Mwezi wa Pili vinatofautiana. Mwezi wa Pili Kamati ya Nishati na Madini imeeleza sababu Tisa za msingi, hizo sababu Tisa ni uzembe wa Mkandarasi. Eti leo wanatuambia UVIKO wakati Mheshimiwa Naibu Waziri unakumbuka ulikuja Kamati ya Bajeti ukatuambia Mkandarasi anasema UVIKO, ninyi kama Serikali mmegundua tatizo siyo UVIKO ila Mkandarasi alikosea, alitakiwa ajenge matuta mawili, kajenga tuta moja wakati wa mafuriko mchezo mzima ukavurugika ninyi mlisema! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nataka leo haiwezekani kila siku sisi tunapigwa haiwezekani! Sasa leo tunampa mtu kazi tena tunamlipa vizuri, yaani kama kuna mtu analipwa kiroho safi ni huyu jamaa, yaani hana hata *stress!* Sasa nataka hivi, huyu mtu anayekula pesa zetu bila *stress,s* hajamalliza ujenzi kama mkataba unavyotaka,

sababu zake alizozitoa ni za uwongo, sababu za Kamati ya Bunge zilikuja hapa zikabaini, Waziri ulikuja ukatuambia kabisa tena hamkutaka kuzikubali tena, tukakuambia subiri mwezi wa Sita si bado? Hasa mwezi wa Sita ndiyo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Taifa lipate majibu kiroho safi, mimi sina bifu na ninyi, wote tunajenga nyumba moja kiroho safi. 6.5 *Trillion* ambazo tunampa huyu kwa heshima kubwa, nchi inapata nini kutokana na uzembe ili tujue kumbe bado tunashida mikataba, ili tujue Wanasheria wetu bado hatujajifunza kutokana na makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sina mengi sana leo hayo mawili tu, naomba nipate majibu kwa nia njema na nisipojibiwa tutakamata Shilingi tu ili tuweze kujiachia zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimuita Mheshimiwa Anastazia James Wambura wakati huo Mheshimiwa Hamida Abdallah anajiandaa na nimeambiwa Mheshimiwa Mulugo karejea kwa hiyo ajiandae pia kuchangia.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kupewa tuzo ya kipekee kabisa kwa uendelezaji wa miundombinu, ambapo ninaamini kabisa kwamba miundombinu hii ni pamoja na ile ya sekta ya nishati, kwa hiyo nampongeza

sana. Vilevile ninaipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo inaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina masuala makubwa mawili katika eneo hili la nishati. Nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kutenga shilingi bilioni 1.48 kwa ajili ya kusambaza gesi asilia majumbani katika viwanda na katika taasisi mbalimbali. Kwa kweli ni jambo moja la muhimu sana, na niseme kwamba usambazaji huu wa gesi asilia hasa kwa ajili ya kupikia utasaidia sana kupunguza matatizo ya uharibifu wa mazingira unaotokana na matumizi ya kuni na mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile itasaidia kupunguza matatizo ya kiafya kama yale ya maradhi ya mapafu na maradhi ya macho wenzetu katika nchi za wenzetu wameshafanya utafiti na kuonyesha kwamba matumizi hasa ya muda mrefu ya kuni na mkaa yana athari kubwa sana kiafya kwa akina mama na watoto na hasa kwa upande wa mapafu na upande wa macho, nasi wenyewe tumekuwa ni mashahidi, wakati mwingine Bibi zetu wanauawa kutokana kuonekana na macho mekundu wanakuwa na imani za kishirikina, wanawaua kwa sababu hizo lakini kumbe tatizo kubwa ni matumizi ya kuni na mkaa kwa muda mrefu, kwa hiyo ninaipongeza Serikali lakini niiombe iongeze fedha kwenye eneo hili kwa sababu kazi inayofanyika kwa kweli inakwenda taratibu sana tunaomba kasi iongezeke ili kusudi kuweza kuwanusuru hawa akina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongeze tena faida nyingine kubwa ambayo inatokana na matumizi ya gesi asili kwa kupikia ni ile ya kusaidia kupunguza matatizo ya lishe kwa katika kaya hasa kwa upande wa Watoto. Wenzetu wa *FAO* mwaka 2018 waliweka mkakati

kuongeza upatikanaji wa nishati mbadala kama vile gesi na umeme kutasaidia sana kuimarisha lishe majumbani. Hii inatokana na kwamba akina mama wale watapata muda mwingi wa kuwahudumia watoto vilevile wanaweza wakapika vyakula vya aina mbalimbali. Kwa mfano unga wa dona kupika ugali unahitaji nishati ya uhakika lakini hata uji ambao tunashauri watoto watumie uji wa dona unahitaji muda mrefu, kwa hiyo niombe sana wizara iliangalie hili iongeze fedha ili kusudi wenzetu kule vijijini waweze kupata nishati ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili ni kuhusiana na zile uzalishaji wa *megawatt* 300 kule Mtwara, naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba uwezo wa kituo cha kuzalisha umeme kule Mtwara ni *megawatt* 30 tu, lakini kwa sasa kuna mashine tatu ambazo ziko nje, kwa hiyo wanazalisha umeme *megawatt* 24, lakini matumizi ya umeme Mtwara la Lindi ni *megawatt* 22 kwa hiyo utaona kitu kinachobaki ni kidogo sana ni takribani *megawatt* Mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana hizi *megawatt* 300 ambazo wizara imesema kwamba itatoa kipaumbele kwenye huu mradi ifanya hivyo kweli. Kwa nini ninasema hivyo, nimeangalia kwenye randama nimeona hakuna bajeti katika miradi mingine ambayo Wizara imewekea kipaumbele kwenye mradi huu wa *megawatt* 300 wa Mtwara hakuna bajeti hata Shilingi Moja! Kwa hiyo niombe sana wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri atuambie Wizara ina mpango gani kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho ningependa Bunge lako Tukufu litambue ni kwamba, wakati wastani wa Kitaifa wa usambazaji wa umeme vijijini imezidi

asilimia 80 kule Mtwara bado asilimia 51 ya vijiji havijafikiwa na umeme. Hata hivyo, bado tunayo mahitaji makubwa ya umeme ukiangalia sasa hivi tunahimiza sana viwanda vya uchakataji korosho, vipo viwanda 20 ambavyo havifanyi kazi hatujui tatizo ni nini, hata hivyo tunaendelea kuhimiza uanzishwaji wa viwanda vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo eneo la *EPZ* kule Mtwara maeneo ya bandari lile eneo wakienda wawekezaji pale tutahitaji umeme mwingi sana wa kutumia, kuna miradi mingine ya maji mikubwa kama vile miradi ya Makonde, mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma, miradi hii itahitaji umeme mkubwa, sasa Wizara iniambie hizi *megawatt* Mbili sasa hivi tukikamilisha hiyo miradi itatosha kweli kuzalisha kutumika katika pampu kubwa za kuzalisha maji? Kwa kweli niseme Mtwara hatujatendewa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kiwanda cha Dangote pekee chenyewe kinahitaji zaidi ya *megawatt* 30 lakini wenyewe wanazalisha umeme wao, kwa maneno mengine tunataka kusema kwamba kwa umeme huu tulionao, kama tuta-*neglect* hizi *megawatt* 300 ina maana hakuna fursa za uwekezaji zaidi katika Mikoa ya Mtwara na Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Serikali ituangalie watu wa Mtwara na Lindi ituanzishie huu mradi wa uzalishaji umeme ili kusudi nasi tuweze kuwa na fursa za uwekezaji, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana sasa namwita Mheshimiwa Hamida Abdallah.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamida Abdallah na baadae Mheshimiwa Phillipo Mulugo. Mheshimiwa Phillipo Mulugo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii ya Nishati. Nianze na mgogoro uliyopo kule Songwe, Mheshimiwa Waziri naomba anisikilize vizuri. Ni kweli Waziri ni mgeni katika Wizara hii lakini Maafisa wa Serikali wako pale na hasa *TPDC*. *TPDC* wametugonganisha kule Songwe, wametoa eneo moja linaitwa South Tanzania kule Kijiji cha Maleza, Jimbo la Songwe, kwamba wanakwenda kutafiti mafuta na gesi. Pale ukifika hata Mheshimiwa Kalemani wakati ule alishafika, wakaona ule uwanja na wakaanza kuona viashiria vya gesi na mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo watu wa kutafiti *helium* nao wakaenda, wakakuta kuna dalili hizo. Kwa hiyo wakawa wamepata *certificate* ya kwenda kufanya utafiti kwa ajili ya *helium* Wizara ya Madini, lakini vilevile *TPDC* wakatoa tena *certificate* ya wale wa *heritage* Tanzania wakafanye utafiti wa mafuta na gesi kwenye kitalu hichocho, kinaitwa South Tanzania. Sasa tunajiuliza Serikali ni moja hiyohiyo kwa nini mambo hayo yanatokea na hivi ninavyosema wananchi pale wanasubiri walishafidiwa mashamba, mahindi, kila kitu. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri alichukue hili akaongee na watu wa *TPDC* waweze kuona jambo hili linakwendaje kwa sababu tunazo rasilimali tayari kule Ziwa Rukwa na mafuta yapo, kumbe gesi ipo, *helium* ipo, lakini ni *just* utafiti tu, mambo yamegongana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu Miradi ya *REA* kwenye Jimbo la Songwe. Miradi ya *REA* Jimbo la Songwe nashukuru Mungu kwa asilimia 30 bado kidogo vijiji vyote kuweza kutimia angalau asilimia 70 tayari, lakini hivi Vijiji vya Ngwara, Itiziro, Itindi, Maleza, Namkukwe, Manda, Isanzu, Muheza, Mpona, Ilea, Iyovyo na Kijiji cha Somi, vijiji 13 bado umeme, lakini tayari Mkandarasi ameshapatikana, ameshamwaga na nguzo, amechimba mashimo halafu akakimbia akaondoka, toka mwaka jana mwezi Septemba, mpaka hivi ninavyoongea Mkandarasi haonekani. Juzi nilikuwa Jimboni, nimetembelea Vijiji hivyo Mkandarasi haonekani kabisa, sasa sijajua Mkandarasi amepotelea wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna vijana ambao walikuwa wamechimba mashimo, wanadai fedha mpaka sasa hivi, wanamkimbilia Mbunge, Mbunge Serikali imetudhulumu, unajua wale kule hawajui masuala ya ukandarasi, hawajui masuala ya *tender*, sijui *private company, no,* wao wanachoangalia kwamba tunachimba shimo ili umeme uje, ni Serikali ndiyo imeleta umeme, ndivyo ilivyo. Kwa hiyo Mbunge akienda kufanya ziara pale, kwenye mkutano wa hadhara nimekutana na maswali sana Mheshimiwa Waziri, kwamba hawajalipwa fedha walizofanya kazi kwa ajili ya yale mashimo. Kwa hiyo naomba Mkandarasi aliyeshika *tender* kwenye Mkoa wa Songwe atafutwe haraka popote alipo akamalizie kazi kule ili umeme uweze kufika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo nilikuwa na hayo tu kwenye Wizara hii, *otherwise fine* Waziri anafanya vizuri, hongera sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Cecil Mwambe wakati huo Mheshimiwa Felix Kavejuru na Mheshimiwa

Issa Ally Mchungahela wanajiandaa. Mheshimiwa Mwambe, hayupo, haya Mheshimiwa Felix Kavejura.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa fursa hii. Kigoma tuna kilio cha umeme tangu nchi yetu ipate uhuru miaka 60 iliyopita, Kigoma na Katavi hatujaunganishwa kwenye *grid* ya Taifa. Viongozi wa Taifa wa ngazi za Kitaifa wamekuwa wakifanya ziara mbalimbali katika Mikoa ya Katavi na Kigoma na kutoa ahadi ya kuunganisha mikoa hiyo katika *grid* ya Taifa kwa muda mrefu, lakini mpaka sasa hivi miradi hiyo haijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri mwaka 2019 tarehe 25 Machi, 2019, Serikali iliahidi ifikapo mwezi Aprili, 2020 Kigoma itakuwa imeungwa na umeme wa *grid* ya Taifa na ilisema tayari bilioni 87 zipo tayari kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo, leo tuko mwaka 2022 mradi huo haujakamilika, hizo bilioni 87 zilienda wapi? Haitoshi tu, mwaka jana tarehe 26 Novemba, 2021, Serikali ilitangaza kwamba itaunganisha umeme wa *grid* ya Taifa kwa Mikoa ya Katavi na Kigoma kwa mwaka 2022, wananchi wa Kigoma na Katavi wanasubiria kwamba je, ni kweli ifikapo Desemba 31 mwaka huu mikoa hiyo itakuwa imepata umeme wa *grid* ya Taifa? Tuna kilio cha muda mrefu, umeme ndiyo kila kitu, huwezi kupata uchumi wa viwanda bila umeme, umaskini wa Mkoa wa Kigoma na Katavi umesababishwa na ukosefu wa miundombinu ikiwa ni pamoja na umeme. Mikoa hii inazalisha sana, lakini imekosa umeme, kwa hiyo haiwezi kuvutia wawekezaji wa viwanda pasipo na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Waziri kwenye vipaumbele vyake 12 ambavyo amevileta hapa Bungeni,

amesema kipaumbele namba moja ni kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme ikiwepo kupeleka umeme wa *grid* ya Taifa kwenye Mikoa ya Katavi na Kigoma. Najiuliza nimeona vyanzo vya Kigoma kuunganishwa na umeme wa *grid* wa Taifa ni kutoka Nyakanazi kuja Kigoma, kutoka Urambo kuja Kigoma, kutoka Sumbawanga kwenda Kigoma na maporomoko ya Mto Malagarasi. Inanichanganya kwamba hivi vyanzo vyote vinatokea kwa wakati mmoja? Naomba Waziri atakapokuja kutoa hitimisho lake awaeleze wananchi wa Kigoma, katika hizo njia zote nne ni njia ipi hasa ambayo ameipa kipaumbele cha haraka sana ifikapo Desemba tuwe tumepata umeme wa *grid* ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa tunatakiwa tujiulize gharama ya kuendesha umeme ule wa *generator* Kigoma kila mwezi, Shirika linapata hasara ya zaidi ya milioni 700, ukizidisha kwa mwaka Shirika la *TANESCO* linapata hasara zaidi ya bilioni 8.4, kwa miaka kumi ni bilioni 84 kulikoni? Ukiangalia gharama ya kuunganisha umeme wa *grid* ya Taifa kutoka kituo cha Urambo kwenda Kigoma ni bilioni 69, kwa nini huu mradi hautekelezeki wakati Taifa linaendelea kupata hasara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kuangalia, kutakuwepo na watu wanaofaidika na ununuzi wa mafuta, kutakuwepo na maslahi ya *supplier* anaye-*supply* mafuta ya kuendesha hii mitambo ya *generator*. Tunaomba sana wananchi wa Kigoma na Katavi wanalalamika, wana maombi makubwa sana, wana imani kubwa sana na Mheshimiwa Waziri, ana muda mfupi tu lakini ameweka kipaumbele kwa mikoa yetu. Nilikuwa nimejiandaa kukamata shilingi ya Waziri, tunasubiri, endapo itafika mwaka kesho, mikoa yetu

haijaunganishwa na *grid* ya Taifa tutakuja kukamata shilingi ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Felix Kavejura. Nilimwita Mheshimiwa Issa Mchungahela, aweze kuchangia.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona na kunipa fursa hii. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunipa fursa hii pia ya kuongea na nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nahutubia Taifa hapa. Kwa makofi haya naona kwamba Wabunge tuko tayari kusikiliza Hotuba ya Taifa ambayo itatufanya tuitekeleze kikamilifu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo jambo la kulizungumzia ambalo kama sitalisema naona nitakuwa sitaitendea haki nchi hii. Sisi Watanzania, lakini sisi Wabunge ambao tumepewa dhamana hii kubwa ya kutengeneza maono na kutengeneza mwenendo wa nchi hii kwa maana ya uchumi wake, lakini na mahusiano yetu na nchi zingine na ustawi wa nchi hii, kwa kweli tunalo jukumu la kusimamia sana haya tunayoongea na siyo kusema tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia jukumu tulilokuwa nalo, kumekuwa na manung'uniko mengi sana yakijitokeza kwamba hatuna usimamizi mzuri katika bajeti zetu na hiyo inapelekea utekelezaji wa maeneo mengi sana, siyo bajeti hii lakini takribani bajeti zote unasuasua.

Sasa ndugu zangu nataka nikwambieni kwamba pesa tunazozitenga hapa, ni nyingi sana, ukichukulia mfano kwenye bajeti hii peke yake kuna takribani bilioni 2.7, hii ni pesa kubwa sana. Ukiangalia kwenye bajeti nzima ni zaidi ya asilimia tano ya bajeti, ni pesa nyingi sana. Kwa hiyo tunayo kila sababu ya kuisimamia pesa hii kuhakikisha kwamba inafanya kazi inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu haya tunayo Wabunge, Wabunge ndiyo tumepewa dhamana ya kusimamia pesa hii, wale ndugu zetu wengine kwa maana ya wananchi wa kawaida, hawana nafasi hata kama watataka kufanya hivyo, lakini wanaona kwamba sisi ndiyo watu thabiti ambao tunatakiwa tuifanye hii kazi kikamilifu. Kwa hiyo nawaomba ndugu zangu Wabunge kwa pamoja kabisa na ndugu zangu Mawaziri ambao ndiyo watekelezaji wa haya majukumu ya Wizara zao, tusimamie kikamilifu kabisa hizi bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano kwenye bajeti iliyotengwa mwaka jana, mwaka jana kwa ujumla tulitengewa takribani trioni 2.3 za bajeti hii ya Nishati. Katika kiasi hicho cha pesa kumekuwa na changamoto katika maeneo fulani ya utekelezaji, kwa mfano, Mradi wa Kinyerezi wa kufua umeme ulitengewa takribani bilioni 88.5, lakini katika kiasi hiki cha pesa kiasi kilichopokelewa ni sifuri. Mnaweza mkaona hapo, sasa hatujui ni kwa nini kiasi hiki hakikupokelewa, wakati kuna umuhimu sana wa kupata huu umeme ambao ungetakiwa kufuliwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *REA* pia tulitengea bilioni 363, lakini katika kiasi hicho kilichotengwa mwaka jana ni asilimia 59 pekee ndicho kilichopokelewa, lakini utekelezaji wake sasa katika hizo

pesa zilizopokelewa ni mdogo sana. Ukiangalia kwa mfano, Kamati inayohusika na masuala ya Nishati ilivyokwenda kutembelea baadhi ya miradi, ilikwenda ikakuta eneo la Pwani ambako kulikuwa kumetekelezwa mradi mmojawapo wa *REA* ulitekelezwa kwa asilimia 20 tu. Sasa kama utekelezaji ni asilimia 20 kwenye *REA,* hivi mnafikiria kwamba tunaweza tukaendelea kwa kiasi gani. Hapa tunaweza tukasema kwamba utekelezaji umekuwa ni finyu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukulie katika Mkoa wangu wa Mtwara, Mkoa huu umekuwa na changamoto kubwa sana ya umeme, ni katika Mikoa ambayo tunaweza tukasema ina shida kubwa ya umeme ukiondoa Mkoa wa Tabora. Utekelezaji wake ni mdogo kabisa, kumekuwa na shida ya kubwa sana ya kukatikatika kwa umeme kwa mfano Masasi ukatikaji wa umeme umekuwa takribani mara nne kwa siku. Jambo hili hatuwezi kulivumilia kama kweli tunataka maendeleo ya kweli katika masuala ya kiuchumi. Bajeti iliyopangwa katika Jimbo la Lindi kulikuwa na takribani vijiji 30 ambavyo vilitakiwa kufikiwa na Mradi huu wa *REA,* kitu cha kushangaza mpaka hivi ninavyosema hata kijiji kimoja hakijafanyiwa utekelezaji wa Mradi wa *REA*. Sasa ndugu zangu tunaweza kufika kwa mtindo huu kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kuna baadhi yetu tumekuja hapa tumepongeza sana katika hii Wizara. Siyo vibaya kupongeza, lakini je, tukienda katika uhalisia hizi pongezi hii Wizara inastahili kweli, kwa sababu nikiangalia ni katika Wizara ambazo *performance* yake iko chini kabisa chini ya kiwango. Tukiangalia kama kweli tunahitaji kuendelea na hii Wizara ina-*perform* chini kiasi hiki katika bajeti zake, nashindwa kuelewa kwa kiasi gani

hii bajeti iliyoko sasa hivi itaweza kutekelezwa. Ndipo pale niliposema ndugu zangu Wabunge kwa pamoja, kwa umoja wetu, naomba sana tuisimamie hii Wizara kikamilifu kwa sababu hii Wizara imepewa pesa nyingi sana hatuwezi kuziacha hizi pesa zikapotea kwa mtindo kama huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mradi wa Julius Nyerere kwa mfano, kuna pesa nyingi pale zimewekwa kwa ajili ya utekelezaji, lakini mpaka sasa hivi kitu cha kushangaza ni kwamba mradi huu haujakamilika wakati ulitakiwa *at least* kwa asilimia 98 uwe umekamilika. Sasa hivi uko kwa takribani kwa asilimia kwa kama 56 hivi, yaani takribani asilimia kama 40 hivi na kitu uko nyuma. Kwa hiyo tunaweza kuona ni kwa jinsi gani najaribu kuzungumza kwamba *performance* ya Wizara hii siyo nzuri japo kama sisi baadhi yetu tunasifia. Sina nia kuvutana na mtu yoyote, nisije nikaeleweka vibaya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naam.

**MWENYEKITI:** Nilikuongeza dakika moja, nikifikiri ndiyo unahitimisha lakini naona bado unataka kuendelea kuhutubia Taifa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekushukuru sana. Naomba sasa baada ya shukrani hiyo, niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mchangiaji wetu anayefuata ni Mheshimiwa Almas Maige, wakati huo Mheshimiwa Kunambi Godwin ajiandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniruhusu nichangie hoja hii ya Wizara ya Nishati kuhusu bajeti yao kwa mwaka 2022/2023. Kwanza nijiunge na Wabunge wote wanaotoa pongezi kwa Wizara hii. Nimefurahi sana Mheshimiwa Rais kumteua mwanangu Makamba kwa sababu baba January tunajuana sana mimi na yeye, ni marafiki. Wamefanya kazi nzuri sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vipaumbele hivi walivyoviweka hapa vikitekelezwa nchi hii haitaingia tena gizani, tuwapongeze sana. Unajua ukisema juu juu bila kuzama chini huwezi kufanikiwa, ukitaka kuijua Wizara hii, uende ukaone mitambo yao, ukaone *station* zao, ukaone wanakozalisha umeme na kazi ngumu. Wizara hii peke yake ndiyo umeme ukikatika unarudi baada ya muda mfupi. Zamani tulikuwa na simu unaripoti simu mbovu, wiki nne, wiki tano haijatengenezwa. Umeme unaripoti na mjue Waheshimiwa Wabunge kila mtu anayewasha umeme haukuja kwa rimoti kama *microwave*, umeungwa na waya mpaka Kidatu mpaka unaposindikwa umeme huu, ni jambo gumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusema katika Jimbo langu tulipoingia madarakani Awamu hii ya Sita na Awamu ya Tano kulikuwa hamna hata kijiji kimoja chenye umeme leo nina Vijiji 41 vina umeme na unawake. Hata juzi wamewasha umeme katika vijiji vyangu vinne Kinyamwe, Ibelamirundi, Ikongolo, Utemini na Ndono na kule ni msituni, sisi Tabora tuna misitu, lakini wanapitisha umeme katikati ya msitu na unakwenda katika vijiji. Hili si

jambo la kubeza, ni jambo la kuwapongeza sana, hongereni sana Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mama Samia Suluhu Hassan kurithi mradi ule mkubwa wa umeme wa bwawa la Mwalimu Nyerere, ni fedha nyingi sana linajengwa lile bwawa, amejikita na Mawaziri wake Waziri Makamba na mwenzie Naibu Waziri kumalizia mradi huu, siyo jambo rahisi tumpongeze Mama Samia Suluhu Hassan sana. Ni moja ya miradi waliyosema itatelekezwa mbona inaenda sana! lakini panapokwenda meli Zanzibar na mawimbi yapo tutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa mpango wa kuwa na miradi mingi ya kuzalisha umeme nchini, inalenga kutatua matatizo ya umeme kabisa. Zamani tulikuwa na mradi mmoja na mashine za kukodisha, lakini leo kuna mkakati wa kujenga mitambo yetu wenyewe ya kufua umeme. Mimi nina hofu ndogo sana, nina hofu ambayo sijui naogopa nini? Kituo cha Umeme cha Msamvu *(Vital Installation)* kimeungua mara mbili, unajua kwa nini naogopa? Kituo hiki kinaunganisha umeme unaotumika kujenga Bwawa la Mwalimu Nyerere na kila kinapoungua mradi kule unasimama, ni moja ya sababu ya kuchelewesha mradi ndiyo maana naogopa hii *Vital Installation* itaunguaje mara mbili pale pale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kujiuliza ni hujuma au ni uzembe, ni nini sasa? Mheshimiwa Makamba tafadhali sana, naomba sana muweke kitengo cha uchunguzi, hii *Vital Installation* kuungua mara mbili kwa muda mfupi isiungue tena mara ya tatu inatuchelewesha. Nashauri sana hebu fungueni macho

muangalie kuna nini huko? Zamani *TANESCO* walikuwa na kitengo kile cha *Business Intelligence* na kulikuwa na watu kutoka *TISS* wanafanya kazi huko, Mheshimiwa marehemu Kasanzu na Mheshimiwa Kiza walitoka *TISS* kwenda kusimamia ulinzi na usalama wa vituo *Vital Installation* ya *TANESCO*. Sijui kama imerithiwa au inaendelea sina hakika, naomba sana Mheshimiwa Makamba usimamie ulinzi wa vituo vyako vya umeme *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utafutaji wa mafuta, mimi sijui kwa nini Tanzania hatujapata mafuta, sina sababu inayoniweza nikawaza nikajua kwa nini hatuna mafuta Tanzania? Kwa sababu wenzetu walivyopata mafuta ni ushoroba ule ule wa Bonde la Ufa na sisi linaanzia kwetu hapa kwanini sisi hatuna mafuta? Najiuliza ni teknolojia tu tunayotumia kutafuta mafuta au utaalam ni mdogo au uwekezaji mdogo au hakuna utashi ni hujuma ni ukosefu wa uzalendo na nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Makamba hili mimi nitakukamata wewe, kwa sababu wewe ni kijana unayejua sana mambo haya, hivi kweli kwa nini hatupati mafuta? Huko Uwembele Tabora huko kuna mahali wanasema hapo panafaa mafuta yapo, uchunguzi ni mdogo sana unaokwenda kufanya kazi kule, wataalam wanaokwenda kule hatuwaoni wakabeba vitu vikubwa vya kutafutia mafuta, hamtaki kupata mafuta hapa? Kipaumbele cha kutafuta mafuta na gesi mmekiweka Namba 11 kwa nini kisiwekwe cha kwanza? Maana yake mafuta tunahangaika hovyo hata hatujui tufanye nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia gesi kule wenzetu Ruvuma kule wale watu wa *Mozambique* kwenye Jimbo

lao wanaloungana na Ruvuma ndiyo wamepata gesi, *trillion* na *trillions* za *cubic,* sisi bahati mbaya hata hatujaanza kutafuta kule. Tafuteni gesi kule la sivyo gesi inatembea kama mkondo kule chini wakitoboa kule gesi itahamia kule yote, naombeni sana jaribuni kutafuta mafuta Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kuniruhusu nichangie hoja ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Almas Maige kwa mchango wako. Nilimuita Mheshimiwa Godwin Kunambi wakati huo Mheshimiwa Vedastus Manyinyi anajiandaa.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nianze kwanza kwa namna ya pekee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu wa kupeleka fedha takribani Shilingi Bilioni 100 kwa ajili ya kunusuru suala hili la upandaji wa bei ya bidhaa hii ya mafuta. Nimpongeze Waziri na Wizara yake na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi ambazo ziko chini ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nianze kuishauri Serikali kupitia Wizara hii muhimu. Tunachangamoto kubwa hasa kwenye suala la gharama za kuunganishwa na huduma ya umeme kwa mwananchi mmoja mmoja lakini pia na taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri leo hii kwa nini Serikali isije na mpango huu kwamba mwananchi anapotaka kuunganishwa na huduma ya umeme, asilipe chochote aunganishiwe gharama halafu aje kutozwa hiyo gharama kwenye bili yake ya kulipia umeme kama

huduma zingine. Kwamba unaunganishiwa umeme bure, ukishaunganishiwa umeme unapotaka kuingiza umeme kwa maana ya *LUKU*, basi unalipa gharama yenu mnakata humo kidogo kidogo, hii niwaambie mkiweza kutekeleza hili litasaidia, kwanza mtaongeza wigo ya wateja wengi wataunganishiwa umeme watu wote wenye mahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia upande wa pili mwananchi ataona unafuu kwamba anaunganishiwa umeme bila gharama yoyote. Sasa hivi tunaombwa sijui Shilingi 27,000, sijui Shilingi ngapi inatupa shida tu. Lakini Mheshimiwa Waziri wewe ni Kaka yangu najua wewe ni *fresh minded* na unafikra nzuri, nikuombe katika hili jambo hili ukilifanya kwa kweli kama Wizara yako inakwenda kupata *credit*, kubwa zaidi na Serikali inakwenda kuongeza wigo wa mapato kwamba kundi kubwa la wananchi, wataunganishiwa umeme, pia ulipaji utakuwa kwenye gharama zake kwa maana ya bili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la pili ninashauri kwamba tumeona wengi tunatumia *television* kuna ving'amuzi mbalimbali, *Azam* sasa hivi nikiunganisha tu huduma ya *Azam* moja kwa moja napata huduma na napata huduma ile ya *television*, leo hii *LUKU* kwa kutumia hizi *LUKU* zetu za *TANESCO* kwanza unanunua umeme halafu unakwenda unaanza kubofya tena kuunganisha umeme, hii teknolojia imepitwa na wakati kwa kweli, jambo hili mimi nadhani halileti afya. Kama kwenye ving'amuzi tunaweza kwa mfano mimi leo hii niko Jimboni, mlinzi ameniambia umeme umekatika na nimefunga nyumba yangu LUKU iko ndani, maana yake nini, ninaweza kuunganisha umeme nikiwa Jimboni Morogoro hapa Dodoma nyumba yangu ikawaka, jambo hili linafanyika na ni jambo la kawaida tu *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe kushauri Serikali ni vyema ikaja na mpango huu hii ndiyo teknolojia ya kisasa na naamini Wizara ikienda kufanya jambo hili itasaidia na sisi wananchi kupata unafuu wa huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niguse eneo lingine la mradi wa *REA* mimi Jimboni kwangu ninaishukuru Serikali mradi huu unatekelezwa kwenye vijiji 11, lakini changamoto kubwa ambayo tunaipata wananchi wa Mlimba ni Mkandarasi. Kwa mfano, kuna Kijiji cha Lugala na Kaka yangu Mheshimiwa Waziri mpaka leo huyu Mkandarasi hata kuchimba mashimo hajachimba hata nguzo wananchi wa Lugala hawazioni pale Uchindile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa muda bado na mnasema Disemba mradi unakamilika, lakini kama hajaanza kazi hofu yangu anaweza akaomba tena *extension*. Kwa hiyo, jambo hili mimi niombe kwamba kwa Wizara ni muhimu sasa likachukua hatua kwenye eneo hilo, hali kadhalika Kijiji cha Tanganyika pale Masagati kuna hiyo changamoto. Kama haitoshi nimesikia sikia kama ni kweli au la na kama ni kweli Mheshimiwa Waziri nikuombe unapokwenda kufanya majumuisho, nimesikiasikia mnataka kutuongezea ile *Low Voltage (LV)* kwenye vijiji vyote ambavyo viko kwenye hii miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna huo mpango Serikalini kwenye Wizara yako kwamba, mnatuongezea kilomita nyingine katika hili nianze kukupongeza kabla hujasema. Kwa kuwa, imekuwa ni changamoto kubwa sana kule kwenye vijiji vyetu, *LV* umeme mdogo unakuwa na kilomita moja haufiki maeneo muhimu, lakini kama

mnakwenda kutuongezea ushauri wangu mwingine ni muhimu sasa umeme huu uguse kwenye maeneo muhimu ya huduma za jamii. Kwa mfano, vituo vya afya, zahanati na shule zetu, hii itatusaidia wananchi hawa kupata huduma, kwa hiyo kama kuna jambo la namna hiyo Mheshimiwa Waziri kwetu sisi wana Mlimba tunasema ukiweza kutuongezea hiyo kilomita moja, unapokwenda kuhitimisha hapa sisi tutashangilia na kwa kweli utakuwa umeupiga mwingi sana Kaka yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ni eneo la suala la utafiti wa mafuta na gesi nchini. Nchi yetu ni tajiri sana isingefaa tuendelee na changamoto za mafuta, isingefaa tuendelee na changamoto za umeme. Mimi nishauri jambo hili inawezekana na niliwahi kusema hapa huko nyuma nchi yetu ina kila kitu, hatuna changamoto ya rasilimali fedha wala rasilimali watu changamoto tulizonazo ni tatu tu kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza ni uzalendo, Mtanzania yeyote mwenye mapenzi mema na nchi yake anaweza kufanya jambo kubwa sana. Pili, ni *mindset* kwamba *it can be done,* inawezekana! Watanzania wengi hatuna jambo hili. Jambo la Tatu, ni *commitment.* Mtu yeyote kwenye Taasisi yoyote akiwa na mambo haya matatu anafanya miujiza. Tumekuwa tukizungumza fedha fedha fedha jambo moja, lakini uzalendo, tukiweka mbele *mindset* kwa maana ya *positive attitude* na mwisho *commitment* inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niseme tu na nishauri Wizara hii na ninaamini naendelea kusema *my brother* naamini uwezo wako naujua, nafahamu pia na uwezo wa Naibu Waziri wako, katika hili nadhani mnayo

nafasi bado. Mnayo nafasi Watanzania tunayo imani na ninyi kwa kutumia hayo mambo matatu naamini, mnakwenda kufanya miujiza kwenye Wizara hii na sisi wote Watanzania tukafurahia huduma ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimuita Mheshimiwa Vedastus Manyinyi aweze kuchangia.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Nishati. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ya kisayansi, vilevile na timu yake yote kwa ujumla katika Wizara hii. Mimi nimemsikiliza kwa makini sana, kutokana na hii hotuba yake labda nichangie tu kwenye maeneo mawili. Eneo la kwanza ni eneo la huu umeme wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba huu umeme vijijini kwa maana ya *REA* ni umeme ambao umesaidia sana watu wetu wengi na umekuza uchumi wa nchi hii kwa *speed* kubwa. Ndiyo maana hata Serikali ikafika mahali ikasema umeme huu uende hata kwenye yale maeneo ya pembezoni mwa Miji ambapo kati ya Miji ni pamoja na Musoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niseme kwamba Mji wangu wa Musoma ulibahatika kuwa miongoni mwa Miji ambayo ilianza kupata umeme huu katika zile mitaa za pembezoni, kwa hiyo nashukuru kwa hilo, katikati hapa ukawa umesimama lakini jana Mheshimiwa Waziri nakushukuru kwamba umesema kwamba unatoa ndani

ya miezi Sita kwa ajili ya kufanya tathmini. Sasa mimi ombi langu ni moja tu kwamba pale kwangu Musoma Mjini kama ni tathmini ilishakamilika na baada ya kuwa imekamilika tulianza kupata umeme wa *REA* katika ile mitaa ya pembezoni. Mfano, kwa pale Musoma Mjini kuna mtaa kama Morembe, mtaa kama Songambele, mtaa wa Bweri, Nyabisare, Mwisenge Mtakuja, Zanzibar pamoja na kule Makoko - Bukanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule tumepata umeme wa shilingi 27,000 lakini sasa bahati mbaya moja tu ni kwamba, ule umeme wamekuwa wakipewa watu mita 60 yaani pale ambapo nguzo inapita. Katika hiyo mitaa zaidi ya mitaa 15 unakuta mtaa mmoja ni nyumba tano ndiyo zimepata umeme wengine hawana. Kwa hiyo, mimi ombi langu kwako kwa heshima zote hebu basi hapa Musoma Mjini kwa sababu, tayari hili zoezi lilishafanyika na watu wameshapata umeme, kumbe ni kwamba hatuna sababu ya kufanya tathmini tena. Maana leo tukisema kwamba twende kufanya tathmini maana yake ni kwamba, kwa mwaka huu watu wetu hawawezi kupata umeme wa Shilingi 27,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu suala la umeme linasaidia sana watu wetu kupata ajira na kusema kweli katika nchi hii kati ya eneo ambalo nadhani Serikali inahitaji kuweka nguvu sana ni kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata ajira, maana vijana wetu wengi wanamaliza vyuo, wanamaliza shule lakini wakifika mahali hawana kazi ni imani yangu kwamba, ule umeme ukisambaa, umeme wa shilingi 27,000 anayetaka kufanya kazi ya *welding* atafanya, anayetaka kutengeneza *kiosk* cha chake soda baridi zinapatikana ataendelea, biashara ya *saloon* itaendelea, na ukiangalia leo mahali popote ambapo umeme

umepita tayari vijana wengi wanapata ajira kwa sababu wanaweza kujiajiri. Kwa hiyo, mimi niseme tu kwamba pamoja na ahadi uliyoisema ya kufanya tathmini lakini kumbe yako maeneo ambayo huhitaji kufanya tathmini isipokuwa tu unahitaji kuelekeza ni suala tu la nguzo kuongezeka pamoja na nyaya basi na kwa kufanya hivyo watu wengi wataendelea kujipatia umeme na maisha yao yatakuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo mimi nishauri kwamba leo katika bahati tuliyonayo tayari mpaka sasa kwa mujibu wa hotuba yako, tunazalisha karibu *megawatt* 1,694 lakini matumizi yetu ni chini ya *megawatt* 1,400. Kwa hiyo, kwa maneno mengine tunazo *megawatt* zisizopungua 400 lakini inaonekana ndani ya miaka miwili, tutakuwa na *megawatt* zingine siyo chini ya 2,000 ambazo hazitakuwa na matumizi. Sasa mimi niseme tu kwamba Watanzania wengi wangependa kuweka umeme lakini ni kwamba ule uwezo wa Shilingi 300,000 kwenda juu, maana leo tunazungumza Shilingi 320,000 lakini unapokuja kwenye hali halisi kwamba hata yule mtu wa mjini mwingine ni zaidi ya nguzo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kumbe mahitaji yake ni zaidi ya shilingi 300,000, tunakwenda shilingi 500,000 mpaka shilingi 1,000,000. Sasa mimi ombi langu ambalo linawezekana kabisa hasa kutokana na *projection* ya umeme ambao tunatarajia kuupata, hivi kwa nini tusiendelee na zoezi la shilingi 27,000 lakini kwa utaratibu wa kuwakopesha. Yaani leo mimi ni vigumu nikapata shilingi 500,000 ya kuweka umeme au shilingi 1,000,000 ya kuweka umeme lakini ni rahisi sana ukaniwekea umeme kwa gharama nafuu, lakini kwenye *charge* ile ya kila mwezi labda badala ya kulipa shilingi

20,000 kwa mwezi basi nikawa nalipa shilingi 30,000 au shilingi 50,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba tukifanya hivyo watu wengi zaidi wataweza kuweka umeme na wakiweka umeme kwa sababu, tunatarajia kuwa na umeme mwingi basi kumbe ni kwamba na mauzo yetu nayo yatakuwepo. Hata kama ungetafuta *Financial Institution* kama benki wakatoa mkopo tukawawekea watu wengi umeme, maana yake ni kwamba Shirika lingeweza likapata fedha zaidi. Kwa hiyo, mimi nikuombe kwamba Mheshimiwa Waziri ikikupendeza basi ni vizuri Mji kama wa Musoma ungekuwa *pilot study* ya kuona kwamba namna gani tunaweza *tukawa-finance* watu wetu wakapata umeme kwa gharama nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa sababu pale Musoma Mjini tulikuwa na tatizo la maji kwa sababu watu wetu hawakuwa na uwezo wa kuweza kulipa maji kwa pamoja. Tulipoweka utaratibu wa kuwakopesha mabomba na vifaa vya maji, leo karibu Mji wa Musoma kote sasa tunadhani ndani ya kuja kufikia bajeti hii watu wote wa Musoma watakuwa wamepata maji zaidi ya asilimia 95. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba kumbe tukienda hivyo kwenye umeme na katika maeneo mengine basi watu wetu watapata huduma bora ambayo itawasaidia sana, katika kuondoa hasa tatizo la ajira ambalo ndilo tatizo kubwa linalowasumbua watu wetu wa Musoma lakini na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilidhani tu kwamba niweze kutoa huo mchango kule kwingine kwenye mafuta kwa leo kwa sababu na mimi naye nina-

*interest* huko, nadhani sitachangia sana kwa sababu ya muda, zaidi ya hapo naendelea kusema nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Vedatus Manyinyi, mchangiaji wetu wa mwisho katika *session* hii atakuwa ni Mheshimiwa Mohamed Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwisho.

Kwanza kabisa na mimi nichukue fursa hii ya kuwapongeza Waziri na wenzake kwa hotuba nzuri sana. Kiukweli katika hotuba za safari hii zilizokuja vizuri kama ikitekelezwa inaweza kutusogeza sana. Hotuba hii inajibu maswali mengi, changamoto nyingi za kisera na mimi naamini watu waliopo kwenye Wizara hii wanatosha kutekeleza mambo waliyoandika wenyewe, kwa sababu hizo, mimi naomba nieleze zaidi mambo ya Chemba. Naomba nieleze changamoto tulizonazo hasa za umeme kwenye Jimbo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza, wenzangu wameongea juu ya Wakandarasi, sisi kwenye awamu hii *REA round* ya tatu awamu ya pili *ina-cover* vijiji 50, sasa hivi Mkandarasi yuko *site* mwaka mzima lakini kwenye vijiji hivi 50 amewasha kijiji kimoja tu ndani ya mwaka mmoja, tafsiri yake kumaliza atatumia miaka 50 vijiji vingine vilivyopo. Wenzangu wameiongelea changamoto hii sasa mimi sipati majawabu kwa nini changamoto hii ipo hivyo. Nafahamu kabla ya kuomba kazi walifanya *survey* walitafuta majawabu namna gani watapita kuweka kazi hii, lakini hiyo changamoto imeonekana kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri katika hili, zipo Wilaya au Majimbo jiografia yake ni ngumu sana kumpa mwaka mmoja, mwaka mmoja na nusu au miaka miwili kumaliza vijiji vyote 50, mimi hapa maeneo yangu kutoka kijiji kimoja hadi kijiji kingine ni kilomita 50 mpaka 70, unaweza ukaona kabisa jinsi gani kazi hii ilivyokuwa ngumu. Mimi ninawashauri kama wanataka kazi hii itekelezwe kwa wakati, zipo Wilaya ambazo ni lazima waweke Wakandarasi wawili *otherwise* tutaendelea kugombana leo kwenye mkutano, unaeleza ndugu zangu Serikali hii tiifu imeleta fedha kwa ajili ya vijiji vyote na ndani ya miaka miwili vijiji vyote vitakuwa na umeme lakini inachukua miaka minne. Mimi nimuombe Waziri muangalie uwezekano kwenye Wilaya ambayo jiografia zimekaa vibaya, tuangalie kama tunaweza kuongeza Wakandarasi ili kazi hii ifanyike kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia zipo changamoto nafikiri changamoto zingine ni za kiutawala huko huko. Kwa mfano, mimi ninavyo vijiji ambavyo miundombinu yote imemalizika tangu miezi sita iliyopita lakini hawajawasha umeme. Kila ukienda ukiuliza vipi unaambiwa tunakuja kesho kuwasha, sasa changamoto hii nafikiri ni ya kiutawala zaidi, mimi niwaombe watu wanaohusika hebu tusaidieni yale maeneo ambayo tayari miundombinu ya umeme iko tayari wawashe. Wamesema wenzangu umeme huu una fursa nyingi kwamba tukiwasha umeme, zipo faida za kiuchumi zinapatikana kule sasa kwa nini tunawachelewesha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilipata simu ya mteja mmoja ana kiwanda kidogo cha kukamua alizeti, yeye anakimbizana na alizeti inayotoka shambani sasa hivi, amekamilisha lakini amefika pale wanamuambia kesho,

kesho kutwa, kesho kutwa sasa hii ni changamoto kubwa sana. Mimi niwaombeni sana umeme huu unafaida kwetu sisi kule Chemba kwa sababu vijana wengi sasa watapata ajira huko. Niombe sasa hawa watu wanaohusika hebu mjitahidi, pale ambapo maeneo yale miundombinu imekamilika waende kuwasha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vipo vijiji kama Magandi, Machiga tangu mwaka jana miundombinu iko tayari, mpaka imefika mahali wanagombana na Meneja wa *TANESCO* kwa sababu wanamuambia kesho, kesho kutwa mtu anafika mahali anachoka. Mimi niwaombeni sana kwamba tunawajibu wa msingi sasa wa kuhakikisha hili zoezi la kuwasha umeme, miundombinu ikikamilika mfanye kwa haraka ili watu hawa wanufaike na huo umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni muhimu sana na wenzangu wameliongelea, Wilaya yangu tunaposema Chemba ni Wilaya mpya hakuna mjini kote ni vijijini, sasa tunashindwa kutafsiri ni nani anapaswa kulipa shilingi 300,000 ni nani anapaswa kulipa shilingi 27,000? Ninaiomba Wizara hebu waje na mfumo sahihi ambao sasa utatofautisha kwa sababu nyie wenyewe mnapita Chemba ni barabarani hapo, Chemba ni kijijini bado na nina uhakika watu wenye uwezo wa kulipa hiyo shilingi 300,000 ni wachache sana, hebu tuangalie namna bora ambayo tunaweza kuwasaidia hao watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, kuna jambo ambalo halijafanyika, tunafahamu umeme utasaidia sana kupunguza shida za maji huko vijijini. Sasa hizi *projects* za umeme hazikuweka bajeti ya kuweka umeme maeneo yenye taasisi, kama shule za msingi ukiona shule ya msingi ina umeme labda imejengwa kijijini

pale pale, lakini ni ukweli usiopingika visima vingi vya maji viko pembezoni kidogo ya kijiji, sasa nafikiri tuangalie upya namna gani ambavyo tunaweza tukasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maeneo yangu mimi, yapo maeneo ambayo maji yanauzwa shilingi 400, shilingi 300 kwa dumu, kwa sababu tu wanatumia dizeli *ku-pump* zile mashine ili maji yapatikane. Mimi niwaombe sana ndugu zangu nami nakuamini sana Waziri, namuamini sana Naibu Waziri na Viongozi wote mlioko huko jambo hili liko ndani ya uwezo. Nawaombeni mtusaidie, naombeni muangalie namna bora umeme ambao unaweza ukafika kwenye visima hivyo vya maji shule za msingi na zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema siku moja hapa kwamba nina Kituo cha Afya cha Makorongo, ninakumbuka siku Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alivyokuja kukifungua aliwaambia leteni umeme nikasema mpaka leo umeme haujafika. Sasa unaanza kujiuliza alikuja Waziri, alikuja Mkuu wa Mkoa akasema maneno hayo, alikuja Waziri Kalemani akasema maneno kesho kutwa umeme uwe umefika hapa, sasa wewe ndugu yangu haujafika pale, najua wewe ukifika mambo yatakuwa sawa, ndugu zangu nawaombeni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa *session* yetu ya asubuhi nawashukuru wachangiaji waliopata nafasi ya kuweza kuchangia. Mchana watakaoanza kuchangia ni Mheshimiwa

*Engineer* Stella Manyanya atakuwa wa kwanza akifuatiwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mheshimiwa Emmanuel Kingu na baadae wataendelea wachangiaji wengine.

Waheshimiwa Wabunge, ninasitisha shughuli za Bunge mpaka 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

**HOJA ZA SERIKALI**
**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na uchangiaji. Nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe, wakati huo Mheshimiwa Emmanuel Kingu anajiandaa.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, lakini pia nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kuwa hapa tukiwa salama. Kwa namna ya pekee kabisa naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoendelea kufanya, hususan katika eneo hili la Wizara ya Nishati, hasa katika kuhakikisha kwamba, miundombinu inaendelea kuimarishwa, lakini pia

kupeleka fedha katika miradi ya kimkakati tuliyokwishaianza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Waziri wa Nishati pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Makamba na Mheshimiwa Stephen, lakini pia Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi watendaji wote ambao wako chini ya Wizara hii, Wenyeviti wa Bodi pamoja na watumishi wote ambao wako katika Wizara hii. Kwa kuwa, sio rahisi kumtaja kila mmoja, basi niseme tu kwamba, nawapongeza na hasa ikizingatiwa kwamba, Wizara hii wafanyakazi wengi ni wahandisi wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema kwamba, ulimi ni kitu ambacho wakati mwingine kinaponza na ukiangalia Wizara hii tulivyoichukulia wakati inapokea madaraka, yaani wakati Mawaziri hawa wapya wanapokea madaraka, ilikuwa kidogo tuna hali ya wasiwasi itakuwaje? Mambo yataendaje? Kwa hiyo, kukawa kunatokea maneno ya hapa na pale, lakini kusema kweli utulivu ulioendelea na pia viongozi hawa jinsi ambavyo wameendelea kupokea wajibu wao na kuutendea haki, tunaona sasa haya mabadiliko makubwa ambayo yanaendelea. Vilevile tunaona hata Waheshimiwa Wabunge ambao walikuwa wakali sana kwa kipindi cha nyuma, sasa wanaiunga mkono bajeti ya Wizara hii bila kusita na wala sio kwa unafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa semina mbalimbali zilizotolewa kwa ajili ya kuelimisha zaidi. Semina hizi zilikuwa na lengo la kujenga uelewa zaidi na sio kwa ajili ya kuwapofusha Wabunge, Wabunge wa Bunge hili ni Wabunge makini sana, huwezi kuwapofusha. Ni watu ambao wakisimamia jambo lao

wamelisimamia, lakini wakielewa watakuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kidogo kuhusiana na Bwawa la Mwalimu Nyerere. Napenda kuipongeza sana Wizara kwa kazi hii na hapa namkumbuka Mwenyekiti wake wa Bodi ambaye katika Shirika la *TANESCO* ambaye amekuwa ni muasisi wa masuala ya Matokeo Makubwa Sasa. Hapo ni kwamba, unachagua jambo moja zito na unalifanyia kazi kwa nguvu zako zote ili liweze kuzaa matunda mengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hili kwa mtu yeyote ambaye ni dereva mzuri anapoachiwa gari lililokuwa lime-*park* mahali au linaendelea kutembea, hawezi kuchukua tu akaliendesha bila kuangalia lina maji, lina *oil*, lina kitu gani ili liweze kwenda vizuri. Hilo ndilo lililofanyika, baada ya mabadiliko ya kiuongozi kulikuwa na muda kidogo wa kutathmini mradi huu uende vipi, changamoto ni zipi na mahali labda pengine tuboreshe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mradi mkubwa kama wa Mwalimu Nyerere, jamani ule mradi tusiuchukulie sawa na kujenga nyumba yako au kufanya tu ni mradi wa kawaida ambao unaufikiria, unahitaji umakini wa hali ya juu. Mabadiiliklo yoyote ambayo yanafanyika au marekebisho yoyote yanayofanyika hapo si kwamba, wale wa mwanzo hawakuwa na maana au hawa wa mbele ndio wanajua zaidi, ni katika kuufanya mradi huu ambao unatumia trilioni za Watanzania zaidi ya sita, uweze kuwa imara, uweze kuwa utakaokuwa na tija na utakaoweza kudumu kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkumbuke kwamba, hata zile mashine nyingine zinaenda kuwekwa chini huko

kwenye maji. Kwa hiyo, lazima vitu vingine viwekwe vizuri kiasi kwamba, hata zikishafungwa zile mashine kama *turbines* hutegemei kwamba, kesho tena utaanza kusema kwamba, ngoja niangalie, sijui tuangalie ilikaa vibaya, sijui kitu gani, lazima uende kwa mahesabu yote na usije ukapotea. Kwa hiyo, nawapongeza sana na nazidi kusisitiza waendelee kuwa watu makini, pale ambapo wanaona kuna dosari wasisite kusema na kufanyia kazi hata kama itatugharimu kuongeza muda kidogo au pesa kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba, wamefanya jitihada ya kupeleka wataalam wetu kwenda kufuatilia utengenezaji wa zile mashine umba na *turbines* ambazo ziko kule, hilo ni jambo jema sana. Niseme tu kwamba, ndugu zetu wote ambao tuko humu na walioko nje sisi Kamati yenu ya Nishati na Madini tuko makini, ndio maana hatupigi kelele nje, tunapigia kelele ndani. Tunapokuwa kule kwenye Kamati kule ni patashika nguo kuchanika, kila jambo lazima tulione na tunatembelea hiyo miradi na tumetembelea, tumeona Mradi wa Mwalimu Nyerere unaenda vizuri. Sasa hivi *power house* yaani nyumba ya umeme inajengwa inaendelea vizuri, hizo mashine zinaendelea kutengenezwa, sehemu ya *station* ya kituo cha umeme inatengenezwa, *line* ya umeme kutoka kule kwa Bwawa la Mwalimu Nyerere mpaka Chalinze na yenyewe inajengwa, lakini pia tumesisitiza kwamba, hata tukizalisha huu umeme mega wati 2,115 kama hakuna viungo vya kupeleka umeme kwa hawa watumiaji itakuwa ni hakuna maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jinsi ambavyo mfumo huu unafanya kazi hakuna tofauti na mwili wa binadamu. Unaweza ukawa na kichwa, huna shingo, wewe ni

*hopeless,* unaweza ukawa na shingo na mikono huna kichwa, haisaidii. Kwa hiyo, ni lazima mfumo mzima uangaliwe. Nashukuru sana bajeti ya safari hii imeendelea kuwa vilevile nzuri, lakini kubwa zaidi ni kuhakikisha kwamba, sasa ile mifumo mingine ya usambazaji umeme, usafirishaji umeme wa *KV* 400 na yenyewe inakamilika kwa pamoja, iendelee kufanyiwa kwazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimefurahi ni kuona ni kwa namna gani tulipokuwa tunalalamika umeme unakatikakatika, Serikali imetoa fedha ya kutosha kwa ajili ya kufanya matengenezo na marekebisho muhimu ili umeme uendelee kuwafikia wananchi. Sasa hivi naomba Waheshimiwa Wabunge, ukisema umeme unakatikakatika, malizia kusema ni eneo gani ili tukashughulikie, kwa sababu, ukisema kwa ujumla yawezekana utakuwa hutendi haki, sema kwamba, eneo fulani ili liende likashughulikiwe na mambo yazidi kuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo mwaka huu ni mwaka wetu wa sensa. Mwaka wa sensa tutaangalia takwimu za aina mbalimbali, moja ya takwimu itakuwa ni namna gani Watanzania wameweza kunufaika katika nishati za aina mbalimbali. Kwa hiyo, niwaombe, wenzetu watu wa *REA* ambao wamefanya kazi kubwa sana waendelee kuhakikisha katika hii miezi miwili tuliyonayo umeme usambazwe kwenye majumba ya watu ili itakapofikia kujua ni watu wangapi wana umeme, basi idadi yetu iongezeke na izidi kuonesha nchi hii ni nchi yenye nguvu na yenye dhamira katika kuleta maendeleo ya wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo napenda nisisitize kuhusiana na hizi mita janja ambazo tutaanza kuzitumia. Niwaombe sana kwamba, mita janja kimsingi ni ghali kidogo na kama ni ghali hatutegemei wote watapewa kwa mara moja. Kwa hiyo, nafikiria kwamba, mita janja waanze kupata wale ambao watakuwa na uwezo wao wa kuchangia, kwa sababu zile zitakuwa na bei kubwa zaidi pengine takribani mara tatu ya mita za kawaida. Sisi wa maeneo ya vijijini acha tupate hata kama ni mita hizi za kawaida, lakini la msingi tupate umeme kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye upande wa mafuta; napenda kuipongeza sana Wizara kwa jinsi ambavyo imechukua hatua ya kujaribu kupoza makali ya mafuta. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ile shilingi bilioni 100 ambayo ameitoa kwa ajili ya kusaidia marekebisho hayo. Sasa naona kuna mpishano kidogo, wafanyabisahara wanasema kwamba, ile bei ilivyowekwa sasa mafuta yamepungua wao wanapata hasara kwa sababu, walinunua mafuta mengi. Wafanyabiashara tusameheni, acheni ujanja, wakati ule bei ilipotangazwa ikaongezeka mlikuwa pia na madumu mengi mmeyahifadhi, mbona hamkusema kwamba, ngojeni kwanza tuuze kwa bei ndogo haya madumu mengi tuliyoyahifadhi, halafu badaye tutapandisha bei? Acheni ujanja, *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema hivi hata kama hiyo bahati mbaya ipo, ndio hivyohivyo hata wananchi iliwakuta bahati mbaya kupanda bei kubwa sana. Sasa hivi na ninyi bebeni mzigo kidogo, lakini mwisho wa yote tutaenda wote vizuri. Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba, kimsingi nia ni njema, kusiwe huyu anasema hili, anasema

hili, huko ni kuyumbisha, hakuna suala la kuyumbisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niombe kuendelea kusisitiza, najua pengine sitapata tena nafasi ya kuchangia. Bajeti inayokuja ya Serikali ipunguze kama ni kodi wapi kokote itakakojua, lakini katika miradi ya umeme, maji na afya, katika maeneo yale muhimu ambayo tunapeleka fedha za tozo, jamani acha tujifunge mkanda. Kwenye *corona* tulisema tusijifungie tukavuka na hivyohivyo kwenye masuala haya ya kupanda bei mafuta na nini acha tujifunge mkanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule vijijini tunahitaji maendeleo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya kwa mchango wako.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge unapochangia una-*face* Kiti na unaangalia ishara. Nikishika *mic* maana yake lazima uanze ku-*wind up* kwa sababu, kengele inakuwa imeshapiga kama hukusikia.

Nilimwita Mheshimiwa Cecil Mwambe. Wakati huo Mheshimiwa Emmanuel Kingu na Mheshimiwa Mariam Ditopile wanajiandaa.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii kwenye Wizara hii muhimu sana na hotuba ya Waziri wa Nishati. Mwanzo kabisa kwanza ni-*appreciate* mchango wa Mheshimiwa Festo Sanga ambao aliutoa jana, wakati anachangia alikuwa anaeleza vizuri sana kuhusiana na uwezo wa wawekezaji wa ndani kwenye kuzalisha umeme. Alitoa mfano wa Kiwanda cha *Kagera Sugar* ambao wanatumia malighafi zinazobakia za sukari, yale mabaki ili kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya ziara hapo karibuni na kwenye ziara ile walituonesha mitambo anayosimika sasa hivi yenye uwezo wa kuzalisha megawati 20 za umeme wakati mahitaji ya Mkoa wa Kagera tuseme kama megawati 10 hivi ukitoa yeye mahitaji yake, lakini mpaka kufikia miaka mitatu, minne ijayo, atakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 60. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri azingatie ule mchango wake na aone namna ya kuondoa hii sheria kandamizi inayowazuia watu wenye uwezo wa kuzalisha umeme kwenye baadhi ya maeneo kuingiza kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, pamoja na pongezi zangu kwao Mheshimiwa Waziri kwa namna anavyofanya kazi zake na weledi wake kwa kulisaidia Taifa hili na naamini Mheshimiwa Rais, Mama, anamwamini sana kwenye kazi hii. Nafahamu Waziri sasa hivi ndio kiongozi wa majadiliano yanayoendelea kuhusu kukamilika kwa Mradi wa Gesi ya Lindi kwa maana ya *LNG* wenye thamani ya zaidi ya dola bilioni 30. Nimwombe sana, mradi huu ni mkubwa na wenye manufaa makubwa sana kwa watu wa Mikoa ya Kusini

kwa maana ya Mtwara na Lindi, lakini kwa Taifa lote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutegemei mradi huu ni wa muda mfupi, uwekezaji unaofanyika ni wa muda mrefu, utasaidia vizazi na vizazi. Sasa nimwombe Waziri, katika kukamilisha majadiliano ya mkataba huu ahakikishe wanaweka kule ndani *clause* inayowataka wawekezaji wawe na ulazima wa kutumia Bandari ya Mtwara kwa maana ya kuleta vifaa vitakavyosaidia kwenye uboreshaji wa mradi, lakini pia kutumia Uwanja wa Ndege wa Mtwara pia ambao sasa hivi ni mkubwa sana, umeboreshwa kwa maana ya *run way,* ina urefu zaidi kidogo ukilinganisha na Uwanja wa Ndege wa Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sasa hivi pale kuna uwezo wa kutua *Antonov* yenye uwezo wa kubeba tani nyingi tu ya vifaa. Kwa hiyo, hebu tuwalazimishe hawa watu watumie Uwanja wa Ndege wa Mtwara, watumie pia na Bandari ya Mtwara ili iweze kuchakachua, kuchenjua uchumi wa maeneo haya kwa ajili ya wananchi wa Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nishukuru sana kwa namna wanavyofanya kazi zao na nilimfuata nikamweleza na tulikwenda ofisini kwa Mheshimiwa Waziri mara nyingi tu, Miradi ya *REA* inatekelezwa kwenye maeneo yetu, lakini kwa bahati mbaya sana *scope* inakuwa ni ndogo, kwa hiyo, niliomba hapo nyuma katika miaka miwili, mitatu iliyopita, nilikuwa naongea sana kuhusu kata mbili kwa maana ya Kata ya Mpanyani pamoja na Kata ya Msikisi; wakandarasi, mkandarasi wetu *Namis Corporate* yuko pale na anashirikiana vizuri sana na Meneja wa Wilaya na yeye tumpongeze kwa

kazi nzuri anayoifanya, lakini sasa niombe kwa makusudi kabisa kuongeza *scope*. Watakapokuwa wanatoka kwenye hizi kata wahakikishe vitongoji vyote vya kata hizi vimepata umeme ndipo twende maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu kuna tatizo, sasa hivi ukienda Kata ya Ndanda tunaambiwa kuna umeme, lakini umeme huo haujafika zahanati ya Ndanda na sisi tunasema kwamba, umeme lazima ufike kwenye vituo vya kutolea huduma za kijamii. Umeme pia, haujafika zahanati ya Nasindi, zahanati ya Chihoro, zahanti ya Ngalole, Kituo cha Afya cha Mpanyani, Kituo cha Afya cha Lukuledi, Kituo cha Afya cha Namatutwe, Kanisa Katoliki la Nanganga, pamoja na Kanisa la Chikunja, maeneo haya yote hayajapatiwa umeme, lakini ukisikiliza wanakwambia kata hizi zina umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ndefu kidogo. Kuna kitongoji kimoja kinaitwa Ndolo, kiko kwenye Kata ya Ndanda. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, atuongezee nguvu kwenye eneo hili, watu hapa wanapata shida sana kwa sababu, miaka mitano, sita iliyopita walikuwa na umeme; walikuwa wanapata umeme kutoka kwa wamisionari wa Ndanda kama msaada, lakini baada ya kuzidiwa mitambo inayozalisha umeme kwenye hiki kitongoji, kwa hiyo, watu wa Ndanda wameamua kuchukua umeme wao, sasa wale watu wamefanya *wiring* kwenye nyumba zao. Ni kipande kama cha mita 200 tu. Ni suala sasa la kufanya uamuzi ili kuweza kupeleka umeme kwenye kitongoji hicho kwa sababu, watu wale sasa wako gizani wakati miaka mitano iliyopita walikuwa na umeme wa kutosha. Kwa hiyo, niombe sana Waziri tusisitize tufanye kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tulifanya ziara kama nilivyosema kwenye Mkoa wa Kagera, tuliweza kufika kwenye Kiwanda cha Minza wanaozalisha kahawa, lakini kule kwetu Mtwara pia, kuna viwanda vinavyozalisha korosho, kuna viwanda vinavyozalisha pamba. Kuna sheria moja kandamizi inayolazimisha viwanda hivi wakati hawafanyi uzalishaji wachajiwe kitu kinaitwa *capacity charge*. *Capacity charge* inachajiwa asilimia 75 ya matumizi ya mwezi uliopita, kwa maana ya *previous*. Kwa mfano, kama huu ni mwezi Juni nimesimamisha kiwanda kuzalisha, nalazimika kulipa asilimia 75 ya *invoice* yangu ya umeme ya mwezi uliopita, nisipoendelea kuzalisha bado nitakuwa naendelea kulipa hivyohivyo kwa kuonesha kama ni *capacity charge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii ni kandamizi. Sheria ya *capacity charge* ilitungwa wakati huo ili kuweza kupunguza matumizi ya umeme kwenye viwanda. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya *review* ahakikishe sheria hii anaileta tubadilishe ili tuweze kuwasaidia wawekezaji, tuweze kuwavutia wawekezaji. Hata sisi kwenye Kamati yetu ya Viwanda na Biashara na ukiangalia iko mpaka kwenye *blue print,* haijafikiwa kwenye utekelezaji wake, lakini tunaomba sana *capacity charge* iondolewe ili wawekezaji wawe na uhuru, asipotumia umeme asiulipie, haina maana ya kumchaji *invoice* ya umeme na hivi ndio vitu ambavyo tunasema vinaongeza *inflation. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kwenye masuala ya gesi haya ambayo niliyasema pale mwanzoni. Tunaomba sana sisi watu wa kusini mijadala hii inayohusiana na masuala ya gesi kwa sababu, sasa hivi wanasema wanaelekea kwenye hatua ya kuwekeana saini, basi baada ya kuwekeana saini mara moja

mijadala yote inayohusu masuala ya gesi, matumizi yake na mengine tuyaone yanaletwa kwenye Mikoa ya Mtwara, Lindi na mikoa mingine ya kusini ili iweze kuwachangamsha watu na kuwafanya waone kuna kitu pale kinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia kuchangamsha biashara, lakini pia, itawafanya watu wawe *aware* kwa sababu, wao ndio walinzi wa miundombinu hii. Tusipofanya hivyo kwa sababu kwa miaka karibu takribani kumi, kumi na tano nyuma, shughuli za gesi Mkoa wa Mtwara zilisimama ndio zilizosababisha uchumi wa mkoa wetu sisi kuyumba. Bandari haifanyi kazi vizuri wakati ile bandari ilikuwa inakusudiwa kupeleka vifaa vya gesi pia baada ya Serikali kuongeza kwenye ile *berth* moja walikuwa wanakusudia pale kutulia vifaa kwa ajili ya kupeleka Mozambique kwenye miradi ya gesi. Sasa miradi ya gesi ya Mozambique haiendi vizuri kutokana na hali ya kiusalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa bahati hii imerudi kwetu, kutoka Bandari ya Mtwara mpaka Lindi ni karibu kilometa 125. Kwa hiyo, tuombe kabisa mizigo itakayokuwa inatakiwa ifike kwa ajili ya uboreshaji wa huu Mradi wa *LNG* ishuke moja kwa moja Bandari ya Mtwara iweze kupelekwa pale. Ndugu zetu wa Mtwara watachangamka, uchumi wa mkoa wetu utachangamka na utaanza kuona manufaa ya gesi mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri asisahau kabisa kuangalia hilo jambo na nimshukuru sana kwa kazi kubwa anazozifanya, sasa hivi Kijiji cha Mumburu kilichopo Jimbo la Ndanda wakandarasi wa *REA* wako pale. Kijiji cha

Nanganga, tunaomba sasa akaongeze nguvu kwa maana ya kupeleka umeme katika Kijiji cha Nanganga A, Kijiji cha Mkwera, Kijiji cha Mumburu kama nilivyosema A na B, isipokuwa baadhi ya vitongoji vinakosa. Tuangalie pia, uwezekano wa kupeleka umeme Kijiji cha Tungani, kuna baadhi ya maeneo yanakosa, lakini pia Kijiji cha Mwongozo pamoja na Mkangu kwenye maeneo yote ya Jimbo la Ndanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri., kama ambavyo nilisema awali kwamba, kazi hizi zinakwenda na tulikutana wakati ule na Mheshimiwa hapa Mkurugenzi wetu wa *REA*. Yale tuliyoyaongea basi Waziri ataendelea kuyafanyia kazi, lakini kimsingi kazi za umeme Jimbo la Ndanda zinakwenda na naamini hivi karibuni tu watakwenda kuwasha. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na naunga mkono bajeti yake, nimtakie kila la heri katika kutekeleza yale yote aliyoyakusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimuita Mheshimiwa Mariam Ditopile.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia kwenye bajeti ya Wizara yetu ya Nishati. Kwa kuanza kabisa bila ya unafiki napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa maana ameonekana kuwa mwepesi sana kujibu hoja na kufanya maamuzi mazito na magumu kuhusu masuala ya nishati. Tumemuona Mheshimiwa Rais tangu Oktoba - Novemba aliruhusu baadhi ya tozo ziweze kutolewa kwenye mafuta ili kuleta unafuu katika bei ya mafuta ambayo imekuwa ikipanda kila mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeona namna gani baada ya Bunge kuomba unafuu wa bei kwa ajili ya kuweka maisha mazuri kwa wananchi wetu ameweza kutoa kwa kujibana matumizi yake Serikalini Bilioni 100 kama ruzuku na tumeona matokeo yake mwezi huu bei zimeshuka lakini pia tumeona akitoa maelekezo kwa Wizara ya Fedha na ninaamini Waziri wa Fedha yuko hapa na punde si punde atakuja kutuletea Bajeti Kuu pamoja na marekebisho ya Sheria za Forodha kwa kuleta upungufu kwenye baadhi ya tozo ambazo zitaweza kutolewa kwa ajili ya nishati hii ya mafuta. Kwa hiyo, ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwa mwepesi kutoa maamuzi ambayo yanaleta unafuu kwenye bei za mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeona namna gani anaguswa na sekta hii na anataka mapinduzi makubwa katika sekta hii ndiyo maana Mheshimiwa Rais ametulia sana kwenye teuzi zake za wataalam na Mawaziri kwenye Wizara hii. Mimi nilipata ukakasi mkubwa sana kwa baadhi ya watu walipobeza uteuzi wa Mheshimiwa Rais kumteua January Yusuf Makamba kuongoza Wizara hii. January namfahamu vizuri tangu naanza ufahamu wa akili ni Kiongozi Kijana ambaye ni kielelezo kwa vijana wengi ambao tuko nyuma katika siasa.  Kama hamumjui January Yusuf Makamba ndiye kijana aliyehusika kuandika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015/2020 ambayo Ilani hiyo ndiyo imetuletea ushindi mkubwa wa kihistoria kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2020.

Mheshimiwa Spika, nitasema alama yake kubwa mbili tu alizoziacha kwenye baadhi ya Wizara alizoziongoza, alipata nafasi ya kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, waswahili wanasema mzigo mzito apewe Mnyamwezi lakini mzigo mzito

alipewa Msambaa na akauvusha, alipewa kwenda kufuta mifuko ya *plastic* ili kunusuru mazingira yetu January aliweza na alama ameiweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili alipewa mzigo mzito wa kufuta viroba kwenye nchi yetu, viroba havipo na tunaona afya za vijana wetu zikiimarika baada ya viroba hivi kuondoka. Kwa hiyo sina mashaka na weledi…

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kumpa taarifa mchangiaji anayeendelea kutoa mchango wake ni mzuri sana hasa Bilioni 100 zilizotolewa kwa ajili ya kupunguza makali kwa wananchi wale wadogo lakini cha kushangaa bado nauli hazijashuka bei kwa hiyo tuendelee kuishauri Serikali ili kusudi wananchi waweze kufikia ile hatima ya Mheshimiwa Rais aliyokusudia. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Ditopile unapokea taarifa?

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea taarifa nia yake ni njema. Kwa hiyo, nilikuwa namalizia kusema kwamba Mheshimiwa January Yusuf Makamba nimefuatilia mjadala tangu jana ulipowasilisha bajeti yako, kila Mbunge anayeinuka anakusifia na tayari wamekuelewa na wameahidi kwamba wanaenda kupitisha bajeti hii kama kipimo, basi mimi nakwambia Mheshimiwa Waziri tunakukopesha imani sisi kama

Wabunge wenzako, kailinde hii imani na ukawatendee haki wananchi wa Tanzania katika sekta ya nishati na sina mashaka kwa sababu unae msaidizi mzuri, kijana mwenzako, Wakili Msomi na umemkuta hapa kwenye Wizara hiyo, kwa hiyo naona kwa umoja wenu mtashirikiana vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye teuzi hizi za Mheshimiwa Rais amemleta Katibu Mkuu ambaye anaijua hii Wizara, nani asiyemjua Mramba katika sekta ya nishati? Pia amemsindikiza Mramba na Msaidizi wake kaleta kijana mdogo Maimbali yuko vizuri amekulia kwenye mfumo kwa hiyo ninaimani kwamba katika Wizara kwa kweli huko chini mjipange mna uongozi wa juu ambao wana dhamira njema na wanaielewa hii sekta vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais hakuishia hapo tumeona teuzi zake za wenyeviti wa Bodi kuanzia *TANESCO*, *REA* analeta watu ambao wanaelewa nini wanaenda kukifanya. Hakuishia hapo pamoja na Wakurugenzi, leo hii Ndugu Maharage tumeona namna gani ameiwakilisha nchi kwenda kufanya makubwa nje ya Tanzania kwenye mashirika makubwa ambayo yapo *significant* ndani ya dunia hii, kwa hiyo amekuja nyumbani kuja kuvusha Shirika letu la *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitachangia kwenye maeneo machache sana, Mheshimiwa Waziri umetuletea bajeti yako ambayo mimi naichukulia kama ni *action road map* katika kufikia maono ya Wizara. Kiukweli umetupa mpaka vipaumbele vyako lakini umekuja na *ideas* mpya kusema kwamba namna gani utaihusisha *private sector* ili kujipunguzia mzigo lakini namna gani utapata fedha nje ya fedha kutoka Serikali

Kuu ili uweze kuendesha mashirika na kuweza kuleta maendeleo katika Wizara yako. Kwa hiyo, mimi nakutakia kila la kheri na tumeona kabisa namna gani unaenda kutekeleza mambo yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TANESCO* ninakupongeza sana Mheshimiwa Mkurugenzi Mkuu tangu uingie umeanza kuonyesha kile ulichokuwa unakifanya namna gani unataka kuki-*impact* ndani ya *TANESCO* kwa mambo mawili tu ya mabadiliko ya haraka, ni-*connect* umeianza kwa muda mfupi lakini tayari wananchi wameishaipokea *very positively*. Kuna hizi mita janja kwa sababu ilikuwa ni kitu cha ajabu unachukua simu unaigiza mita unanunua umeme tena uende ukatafute pa kuweka zile mita lakini yote ina-*portray* ni namna gani una maono makubwa ya kuja kubadilisha Shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Shirika ni kubwa lina na sehemu tatu kuu ambazo ni kubwa sana lakini nina uhakika kwa timu uliyonayo mtaweza kutekeleza yale ambayo mmeyakusudia na mwisho wa siku kweli mkasadifu ile kauli ya kuliangaza Taifa. Tumeona shida kubwa ambayo inatutatiza ndani ya *TANESCO* ni kukatika kwa umeme. Mimi naomba nitoe ushauri wangu msichukulie kukatika kwa umeme kwamba ni kadhia tu kwa wananchi na watumiaji wa umeme. Pamoja na huduma mnazotoa *TANESCO* mnafanyabiashara ya umeme. Mtu anatumia umeme *regardless* ni wa *TANESCO* ama ni wa *generator* sasa kile kipindi ambacho umeme umekatika yule mtu anaenda kutafuta *source* nyingine ya kutumia umeme, ina maana nyie mnapoteza mapato. Hata hapa Mheshimiwa Waziri wa Fedha upo *CAG* anapoenda kufanya ukaguzi kwenye mahesabu ya Shirika hili, aende akaangalie ule muda ambao *TANESCO*

umeme umekatika mapato wanayopoteza. Kwa hiyo, nimeona dhamira nzuri ambayo mmeionyesha kutaka kwa mara ya kwanza mnataka kwenda kubadilisha kwenda kufanya marekebisho kwenye mfumo wa *grid* na tayari tumeona inahitajika zaidi ya Trilioni Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Rais ndiyo maana nimesema anaenda kufanya maamuzi magumu ya kimapinduzi tayari kwenye bajeti hii mmetenga *500 billion, that's not small money!* Niliwahi kuongea hapa lazima *TANESCO* muende na teknolojia kwa sababu mnapoenda kubadilisha sijui *transformer* kupitia hizi *500 billion,* mtapoenda kubadilisha nguzo na nyaya itabidi mkate umeme ili mfanye hayo marekebisho lakini duniani ipo teknolojia ya kufanya haya na umeme uendelee kuwepo, ipo *live line technology* tunaomba muitumie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Dar es Salaam mnabadilisha nguzo kutoka za miti kwenda za zege inabidi mzime umeme mnapoteza mapato, wakati mnaweza mkaichukua *live line* mukaiweka kwenye hilo zoezi lenu mkaendelea kupata hela za umeme na mkabadilisha mifumo yenu. Kwa hiyo, naomba kwa kweli Wizara ichukulie kwa umakini sana suala la kutumia *live line*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaenda kuweka *transformers* kupitia kwenye miradi ya *REA, TANESCO* kama hivi, maana yake hapa mna bajeti kuweka *transformer* zaidi ya 6,000, tunajua kuna baadhi ya maeneo kama kwa Babu zangu huko Usukumani, Rukwa kuna radi nyingi sana, kuna sehemu unaweza ukapoteza kwa mwaka *transformer* tatu, yaani *transformer* hiyo moja inaharibika mara tatu kuna vifa vinaitwa *combi units,* vile

vifaa vinaenda kuzuia ile *transformer* isiungue kutokana na radi hii itasaidia pia kuokoa kwa sababu tayari Shirika letu lina madeni mengi. Kwa hiyo, kupunguza gharama ambazo zinaweza zikaepukika naomba pia mkaangalie hiyo teknolojia ya *combi unit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *REA* ninawapongeza sana Wizara kwa sababu wote tulikuwa tushaweka kwenye *mindset* kwamba *Rural Energy Electrification Agency* kwamba ni wakala wa kupeleka umeme vijijini. Lakini mmebadilisha kwa sababu siku umeme ukishafika nchi nzima *REA* ife, mmeenda kusema kwamba sasa hivi ni wakala wa kupeleka nishati vijijini, *that's the way to go!* Hayo ndiyo mambo ambayo tunataka kuyaona, mkimaliza kuweka umeme nchi nzima mnaenda sasa kupeleka nishati mbadala na nishati zingine kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimependa kuunga mkono mpango wenu wa vitongoji, kwa sababu kuna Mheshimiwa Mbunge aliwahi kusema hapa, kadri unavyozidi kutanua unazidi kutamani. Sasa umeme umefika vijijini haujafika vitongojini, kwa hiyo mpango huu wa kupeleka umeme vitongojini ni mzuri sana lakini kabla ya kuendelea nao kuna baadhi ya Waheshimiwa walishauri tuangalie yale maeneo ambayo umeme umefika lakini baadhi ya nyumba hazijapata umeme ili tunapoenda kwenye hili la vitongoji hili la vijiji liwe limekaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri sasa nakuja kwenye jambo kubwa ambalo nina imani kwa utulivu wako, kwa akili zako, kwa uweledi wako, ukitulia kwenye mradi wa *LNG* unaenda kuacha historia ya kudumu katika Taifa hili, kwa kweli vizazi na vizazi vitakukumbuka, mfupa huu

umeshindikana zaidi ya miaka 10 leo hii umetutolea kauli baada ya Tarehe 09 Juni tunaenda kusaini *HGA* kwa hiyo nikupongeze kwa hilo. Naomba uangalie sana vitu viwili, tunaye jirani yetu Msumbiji ameanza hili tumeona anavyosumbuka kwenye suala la usalama nasema kwa sauti ndogo kwa sababu tunajua, naomba tujipange vizuri neema lazima inaambatana na hofu ya usalama.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariam Ditopile kwa mchango wako mzuri.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Nilimuita Mheshimiwa Immanuel Kingu wakati huo Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, Mheshimiwa Hamida Abdallah na Mheshimiwa Daktari Charles Kimei wanajiandaa.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kiongozi wangu kwa kunipa nafasi na kwa kweli kimsingi kabisa mimi niungane na Wabunge wenzangu kuendelea kuipongeza na kuiunga mkono Serikali yetu. Mimi kwa leo nina mada kama tatu chache kwa kifupi kwa ajili ya kuishauri Serikali yangu Serikali ya Chama changu iliyoko madarakani, kuwashauri Mawaziri wake pamoja na Watendaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza utafiti wa kidunia unaonesha kwamba *Global Oil and Gas Companies* ni *state owned enterprise* ambazo zinaendeshwa na Serikali husika duniani kote. Ili Taifa lolote liweze kufanikiwa katika *exploration, exploitation* kwenye mambo ya *refinery*, uuzaji na usambazaji wa *oil and gas* Taifa lolote duniani Waheshimiwa Wabunge na

Mheshimiwa Mwenyekiti lazima lifanye uwekezaji wa kutosha katika taasisi zake za nchi kwanza, kwa sababu za kiusalama za nchi, lakini pili; kwa sababu za kibiashara za kupunguza makali ya maisha katika nchi yoyote ambayo imebarikiwa kuwa na *resources* ya mafuta na gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia baadhi ya michango ya Wabunge humu na kidogo nimekuwa *frustrated a little bit,* katika dunia ya sasa hivi Waheshimiwa Wabunge itakuwa ni hatari kubwa sana, tukija hapa Bungeni tukatoa ushauri wa kui-*discourage TPDC* katika uwekezaji wa mafuta na gesi tutakuwa tunafanya kosa kubwa sana katika Taifa hili. Mataifa makubwa duniani yanayozalisha gesi na mafuta nenda nchi kama za Saudi Arabia angalia akina Saudi Aramco yale makampuni, nenda Venezuela, nenda Kuwait wameyawezesha mashirika yao ya ndani ya nchi kistratejia yameweza kuwa na mchango mkubwa wa kufanya biashara kubwa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali, Kaka yangu Mheshimiwa January ninakuomba mimi sihitaji kusema sifa zako, uwezo wako wa kiutendaji *brother* hakuna mtu ana mashaka nao, uzalendo wako kwa nchi yetu Brother January na Naibu wako hakuna mtu ana mashaka nao, *good enough* umepewa timu ya Katibu Mkuu mchapakazi sana, Kaka yangu Mramba na mimi sifa moja January ambayo kwa kweli inakupa uziada, wewe ni *humble* sana *Brother* utasemwa utatukanwa mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. *Brother* umepewa *spirit* ya ku-*hold* na kuvumilia mambo, *keep that spirit* lengo letu ni kumsaidia Rais na Serikali ya Chama chake kilichoko madarakani kufanya *transformation*. Hoja yangu ya msingi ninaomba

Mheshimiwa January tengeneza mikakati, tunahitaji kuiona *TPDC* ya ushindani ndani ya miaka 10 tuweze kuwa na Shirika lenye uwezo wa ku-*compete* na akina Saudi Aramco tuweze kujenga heshima ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninaloishauri Serikali yangu ndugu zangu tusitake kuishauri Serikali kuja kuangamia, wote tunajua gharama ya kupanda kwa mafuta duniani kumeathiri vitu vingi, leo tunazungumza hapa mimi January nakuambia hili usingekuja nalo kwenye mkakati, *I swear* mbele za Mungu wangu nilikuwa nakwenda kukamata Shilingi lakini *brother* mimi nasema kwamba mimi nimenyanyua *salute* kwako umefanya jambo la *diversification* ya umeme na umetuambia unakwenda kuongeza kilomita mbili kila kijiji hivi jamani kwa *strategy* hizo atajitokeza Mbunge hapa aseme mama Samia hafanyi kazi? Au akisimama mtu kusifia mnasema eti wengine wanatumika? Unatumikaje kwa mambo mazito kama haya Rais anayoyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie wala msidanganywe Rais asidanganywe Wabunge wote humu ndani wanampenda Rais na wanamuunga mkono, watu wasiende kutaka kuwachongea Wabunge na Rais waonekane kwamba kuna baadhi ya watu wazuri baadhi ya watu wabaya, Mama Samia kwa kazi anazozifanya wewe Mbunge kama huungi mkono wewe ni kichaa. Leo tunazungumza hapa hii bajeti Mheshimiwa January umeleta hapa kwa *diversification* unakwenda kuifanya ya umeme ina maana Mama ameweka bajeti amekwenda kui-*triple* mara mbili, vijiji tunaongezwa kila kijiji kilomita mbili nani kama mama Samia jamani! Kweli na hili nikisema mje mseme kwamba Kingu anazungumza ili ajipendekeze hivi, mimi ni kijana msomi jambo la kwanza, halafu siyo msomi mimi hapa kichwani niko vizuri.

Nikija kujenga hoja hapa ninajenga hoja kwa sababu walipa kodi waliotutuma wamepata matumaini makubwa ya kazi zinazofanywa na Serikali Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu January kaka yangu ninawashauri ni kweli bei imepanda msije mkajidanganya hapa tukataka sifa hapa ooh! Wakandarasi wanaiba bei zimepanda msiwaumize Wakandarasi bei zimepanda za vitu fanyeni utafiti tumieni wataalam wakaangalie *quoted BOQ* zilikuwa ngapi? Waende kwenye *market* ya sasa hivi, waangalie bei inasoma ngapi, nendeni mkawaongeze wakandarasi pesa miradi ya mama iishe miradi ya Mama iishe, lengo letu ni kuhakikisha ya kwamba kwa hali Mama anavyoupiga mwingi *coming* 2025 Rais ajichukulie kura kutoka kwa Wabunge hawa ambao ndiyo wasemaji na wawakilishi wake huko kwenye Majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho tulizungumza hapa Bunge lililopita *and I was one of the MPs* ambao tulishauri ile kampuni mliipa kazi ya kuweka vinasaba kwenye mafuta *we spoke of this,* ilikuwa ina-*charge* Shilingi 14 kwa lita watu wakapiga kelele hapa mbona tunaibiwa, Rais ameingia madarakani Mama Samia ametoa maelekezo tangazeni *tender*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *tender* imetengazwa huyo ambaye yupo sasa *SISPA* ameomba na makampuni mengine, mchakato umeenda, kampuni imeshinda inatuambia itatuwekea vinasaba kwa shilingi 5.8 kwa lita hao *SIPSA* nasikia sijui wametenda shilingi nane, wameshinda kampuni *lowest* mmefuta *tender* hivi mnafanya kwa maslahi ya nchi au kwa maslahi ya nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunapozungumza hapa *projection* zinaonesha Serikali inapokea *loss* ya shilingi bilioni 4.5 kila mwezi, hivi jamani hatuionei huruma hii nchi, hizi bilioni 4.5 kila mwezi tunazopata *loss,* sitaki kusema mengi. Ushauri wangu kwa Serikali…

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Elibariki Kingu hasa kwenye ile jambo analolizungumzia la ufutwaji wa *tender.* Sheria ya Manunuzi ambayo tulitunga wenyewe ndani ya Bunge hili kifungu cha 19(1), (2) na (3) kinataka utaratibu wa kufuta *tender* Bodi ya Zabuni waende kuomba *PPPRA* na baada ya kuomba uchunguzi ufanyike na waitwe wale walioathirika baada ya kufuta *tender* ile lazima waitwe ili waweze kutoa *concern* zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama utaratibu wa ufutwaji wa hiyo *tender* ambayo wote humu ndani tulikubaliana kwamba wakapewe ile kampuni nyingine badala ya hii inayotia Taifa hasara, kama utaratibu haukufuatwa Mheshimiwa Waziri huu ni uendelezwaji wa uvunjwaji wa Sheria ya Manunuzi ambao unafanywa na Serikali katika idara mbalimbali za nchi hii naomba nikupe hiyo taarifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kingu unapokea taarifa.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa taarifa ninaipokea kwa unyenyekevu mkubwa sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya endelea.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndiyo maana haya mambo tunasema, unajua hili taifa tunalipenda wote, ikiwa Rais aliona kuna mahali kuna shida, mama yetu akaagiza haya yafanyike, hayo yaliyofanyika ya kufuta *tender* na ninakwambia hapa leo nina kwa mambo haya *I have statistics* zinaonesha wale watu wa *TBS* wanapoteza shilingi 11,000,000 kila siku; shilingi milioni mita tatu karibia na sabini kwa mwezi ukiangalia hata *trend* nzima kwenye nchi ndio nimekuja kufanya *compilation* nimepata fedha zinazopotea *4.5 billion* kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge mpo tayari bilioni 4.5 zipotee fedha ambazo zinaweza kwenda kutumika kusaidia watu wengine? Serikali chonde chode msimtie Rais wetu doa, msimtie narudia tena nazungumza nikiwa na macho nimeyakaza bila kumwogopa mtu msimtie Rais aliyepo madarakani doa, fuateni taratibu na sheria za nchi mama huyu kazi anazozifanya kwa Taifa hatutaki 2024 kwenda 2025 Rais wetu tunapomnadi tunataka ni kutoboa na kuteleza kwa maslahi ya Taifa…

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimuongezee taarifa Mheshimiwa Kingu kwamba Kampuni hii anayoitaja ya *SISPA* ndio pia inayoendesha sasa uchapaji wa zile stempu za kieletroniki za *ETS*. Kwa hiyo malalamiko haya ni mapata kwenye uwanda wa biashara zinazofanywa na *SISPA* wakati nchi nyingine zilimkataa na ushahidi upo hata mimi ukiniambia nitenge ushahidi kwako nitakuletea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kingu unapokea taarifa?

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa ninapokea taarifa…

**MWENYEKITI:** ...na muda wako sasa umekwisha.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka kwa Mbunge makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja Mheshimiwa January na Naibu wako fanyeni kazi mumsaidie Mama, Bunge na Watanzania tupo na ninyi mpaka kieleweke. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Nashon Bidyanguze wakati huo Mheshimiwa Hamida Abdallah anajiandaa.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii naomba nichangie na mimi kwenye hotuba hii ya Waziri wa Nishati ambayo ameileta kwetu ili tuweze kufanya uchambuzi, lakini kabla

sijaendelea naomba nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoendelea kufanya katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba nimpongeze mdogo wangu Mheshimiwa January kwa kazi nzuri anayofanya kwenye Wizara hii na mimi lazima niwaambie na nimwambie kwamba Mheshimiwa January ninamfahamu na kwa kweli Mheshimiwa January yupo makini katika uongozi wake lakini ninaimani kabisa kwamba Wizara hii ipo kwenye mikono salama pamoja na Naibu wake Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiit, sisi Wabunge wa Kigoma naamini tulikuwa tuwe wakali sana kama Mheshimiwa January hakuja na mpango wa kuhakikisha kwamba tunapata umeme wa Gridi ya Taifa katika Mkoa wetu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa Gridi ya Taifa imekuwa ni kizungumkuti kwa maana ya kwamba Wabunge wengi waliopita walikuwa wakizungumza na kulalamika sana kuhusu Gridi ya Taifa kutokuingia katika Mkoa wa Kigoma na imepelekea Kigoma kuendelea kubakia nyuma sana kimaendeleo kwa sababu tuliendelea kukosa umeme wa uhakika, haiwezekani kukawekezwa viwanda katika Mkoa wa Kigoma ambao unaendelea kutumia mashine zinazotumia dizeli, isingewezekana kupata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa January kwa kuja na mkakati wa kuhakikisha kwamba kabla ya mwaka huu haujaisha tumepata umeme wa Gridi ya Taifa katika Mkoa wa Kigoma mimi ninakuhakikishia sisi

Wabunge wa Kigoma sasa tunakwenda kukuunga mkono katika kupitisha bajeti yako hii ili kusudi tupate huo umeme wa Gridi ya Taifa ili na sisi tuweze kupata viwanda sasa kwa sababu tunaenda kuhakikisha kwamba tunakwenda kuwekeza kwenye kilimo cha michikichi, sasa je, michikichi itakapolimwa, je, bila umeme kiwanda kitakwenda kupatikana namna gani, kwa hiyo hili jambo ni jema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba nizungumzie kwenye eneo la umeme wa maji wa Mto Malagarasi. Mheshimiwa Waziri eneo hili huu mradi umekuwa ukitajwa katika miaka mbalimbali iliyopita, lakini nafurahi kuona kwamba Mheshimiwa January anakwenda kuandika historia katika mradi huu kwenda kuanzishwa mwaka huu wa fedha, naomba nikupongeze sana Mheshimiwa January na jambo hili ukilifanya kwa kweli utakuwa umeandika historia kwa wananchi wa Kigoma kwa sababu huu mradi utakwenda kutusaidia sisi Kigoma lakini pia na Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye eneo hili naomba uhakikishe wananchi wanafidiwa maana yake huu mradi unakwenda kuutekeleza kwenye Jimbo langu la Kigoma Kusini, wananchi walisimamishwa katika maeneo yao wasiendeleze kilimo, sasa naomba uhakikishe kwamba unapokwenda kutekeleza mradi huu wananchi hawa wawe wamefidiwa. Ninayo taarifa kwamba Gridi ya Taifa inapopita kote tayari wananchi wamekwisha tambuliwa wa maeneo yale wanaokwenda kupoteza baadhi ya mazao na maeneo kwamba tayari, lakini sina taarifa ya kwamba tayari wamelipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba eneo hilo waweze kulipwa fidia wananchi, wasibaki wanalalamika,

mradi wanautaka lakini tafadhali sana Mheshimiwa Waziri fidia itolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la umeme wa *REA* mimi nina vijiji 61 lakini nashukuru kuona kwamba kusema kwamba tunavyo vijiji 29 tayari vimeshapata umeme, lakini bado vijiji 32 havijapata umeme, lakini ninavyo vitongoji 350. Sasa unaposema umeme unakwenda kupatikana mwishoni mwa mwaka huu, mimi siamini kwamba vitongoji hivi vitakuwa vimekwenda kupata umeme kwa sababu kuna Mbunge mwenzangu alizungumza juzi kwamba yeye alipata *t-shirt* ambayo inaonesha kwamba sasa tunakwenda kwenye vitongoji wakati kumbe hata vijiji vyenyewe bado hatujakamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina vijiji 32 ni vingi sana, lakini ukienda kwenye vitongoji 350 yaani vitongoji vyenyewe vina ukubwa sawa na vijiji, sasa kama umeme umechelewa kwa muda huu kwa vijiji 61 tu, je, vitongoji 350 itachukua muda gani, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri wananchi tuwaambie ukweli kwamba ni lini umeme utapatikana katika vijiji vyetu, lakini ni lini umeme utapatikana kwenye vitongoji. Lakini tukizungumza kwamba ni mwaka huu mwezi wa 12, mimi siamini kwamba hilo jambo litawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika Jimbo langu pia wapo wawekezaji wa umeme mmoja anaitwa Jumeme na mwingine anaitwa *Power Corner;* hawa watu wamechukua baadhi ya kata kwa maana ya vijiji wamepeleka umeme lakini wananchi wanalalamika sana, wanalalamika mambo mawili, kwanza moja umeme haupo yaani umeme haupo wakati wa mvua umeme haupo, hata wakati wa kiangazi umeme haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaweza ukajiuliza hivi hawa wananchi kupewa huu mradi kwa hawa watu wa Jumeme na *Power Corner* maana yake ilikuwa ni nini, wanahisi kwamba Serikali iliwadanganya, lakini kero nyingine ya pili ina maana wao wanapewa *unit* mbili kwa wiki, sasa *unit* mbili ni ndogo sana na ukilinganisha kwamba umeme wenyewe haupo, kwa hiyo wananchi wanalalamika, wakati mwingine wanaweka vitu vyao kwenye *deep freezers* zao, lakini mwisho wa siku vinaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini makampuni haya ofisi zao hazijulikani, wananchi hawajui waende kulalamika wapi, lakini pia lipo jambo ambalo limelalamikiwa na Wabunge wengi hili ambalo baadhi ya vijiji vimeongezewa kutambuliwa kwamba ni miji waweze kulipa shilingi 320,000 kuingiza umeme; kwa kweli ni jambo la kushangaza sana.

Mheshimiwa Waziri unafahamu Nguruka na unafahamu Uvinza hivi ni vijiji, imekuwaje na hawa Nguruka na Uvinza waweze kuwekwa kwenye *tariff* ambayo inalipwa na mijini? Naomba hili jambo uende kuliangalia, nimefurahi kwenye taarifa yako ulipokuwa unatusomea bajeti kwa kweli imeonesha kwamba lalamiko hilo limefika kwako Wizarani, lakini umetuma Tume ya kwenda kuchunguza uhalisia huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jitahidi sana Mheshimiwa Waziri Nguruka watu waende waone na Uvinza wafike, hawa wakifika Uvinza au wakifika Nguruka hakuna sifa ya kuongezewa ikawa shilingi 320,000 hawana hiyo sifa hata Uvinza hawana hiyo sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nimpongeze Mheshimiwa Waziri, lakini nakuomba sana umeme wa Gridi ya Taifa ufike Kigoma, lakini na huu mradi wa umeme wa Malagarasi tuanze kuona kazi ikiendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo mimi naomba niunge mkono hoja nasema kazi iendelee, ahsante kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, nilimwita Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah aweze kuchangia.

Mheshimiwa Hamida Abdallah, *okey* basi ninamwita Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei aweze kuchangia wakati huo Mheshimiwa Benaya Kapinga ana dakika tano za kuchangia.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona na kunipa fursa hii, nitazungumza machache na nitaomba nisitoe pongezi kwanza nimalize kwanza kwa sababu muda wangu ni mfupi na mimi nina mambo mengi ya kusema, lakini nitakuwa nakosa fadhila nisipoanza kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu ambaye wote tunasema tunampenda sana, lakini sisi Wanavunjo tunampenda zaidi kwasababu tumeona miradi mingi imekuja pamoja na kwamba mradi wa ujazilizi *(densification)* ya umeme ulikuja kuzinduliwa pale kwetu kwenye Kijiji cha Nganjoni na ninashukuru sana ni jambo la kumshukuru Mungu sana kwa sababu kwa muda mrefu kule Vunjo tulikuwa hatujaona miradi kama hii chini ya Awamu ya Sita namshukuru sana pia Waziri anayehusika Mheshimiwa Makamba na uongozi mzima wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pamoja na kwamba tulifaidika na tulikuwa na bahati ya kuzinduliwa mradi wa *densification,* lakini ule mradi haukuendelezwa, naona umeanzia pale kwenye Kijiji cha Nganjoni kwenye Jimbo letu, lakini naona haujaendelezwa sana, lakini pia kuna tatizo kubwa sana na ambalo tumeambiwa na tunamshukuru Waziri ametuletea watendaji wetu kwenye mabanda tukazungumza nao wakasema kwamba sasa fedha zimepatikana za kuweza kuwaunganisha wananchi wetu ambao tayari wameshalipia kufungiwa umeme kwa miaka zaidi ya mitatu, lakini hawajafungiwa wananchi zaidi ya 2,500 kwa Wilaya yetu ya Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeambiwa kwamba fedha inapatikana na mpango upo sasa na vifaa vipo, kwa hiyo, wataanza kufanya hiyo kazi na ninaamini kwamba wakati huo hawadanganyi na ninaamini kwamba Waziri tuliye naye ni makini, ataweza sasa kutuhakikishia kwamba hii kazi itafanyika kwa sababu kusema kweli ni kazi ambayo inaendana na kipaumbele chake cha kwanza japokuwa ninaamini kwamba vipaumbele hivi viliorodheshwa vya kwanza mpaka kumi na viwili sio kwa umuhimu wake kwamba vyote vitatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipoanza kusoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri na naomba nieleze pale alipoishia Mheshimiwa Vita Kawawa jana, nilijiuliza maswali machache; swali la kwanza kwamba je, Wizara inaweza ikatuambia mahitaji au makisio ya mahitaji ya umeme hapa nchini katika kipindi cha miaka mitano kwa uhakika yakoje? Kwa sababu ukiangalie kwa miaka 60 tumekuwa na uzalishaji ambao haujazidi megawati 2,000; uzalishaji ulipo kutokana na kielelezo cha kwanza kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni megawati 1,694 na nimekuja

kuangalia matumizi ya kiwango cha juu wanasema kiwango cha juu cha matumizi ni megawati 1,335 na miaka 60 ya uhuru. *(Makofi)*

Sasa ninapoangalia tukienda na uzalishaji huu ambao tunaambiwa nao unaongezeka kwa kasi tukiweka *Kinyerezi Extension* megawati 185 tunaweka Rusumo megawati nane, tunaweka Nyerere megawati 2115 tunakuwa tumeshaongeza megawati 2,700; ni karibu mara mbili ya matumizi yetu ya sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado kuna mingine, kuna hii ya Ruhudji, Kakono, Rumakali, Malagarasi na kuna Kikonge ukiongeza yote hiyo tunakuja kuwa tunaongeza katika haya matumizi yetu tumeshaongeza megawati 4,205 na ukiweka kwenye hii ambayo tunayo tunafikia megawati 5,899. Je, mahitaji haya tunajua tutayatumia kweli kwa kasi hiyo? Kwa sababu kama tunatumia megawati 1,300 sasa tunakuwa na megawati 5,800 makisio ya matumizi yako hapa huwezi kuongeza kukimbizana na ongezeko la uzalishaji au kupanua uzalishaji bila kuwa na uhakika kwamba utapata wanunuzi wa matumizi kwa sababu ni fedha tunaweka na hii fedha tunayoweka kwenye umeme kwa kasi sana tunataka umeme uwepo wa ziada, lakini sio kwa ziada sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunatumia fedha za kukopa kwa kutengeneza miundombinu hii, kwa hiyo lazima twende na kasi ambayo inakubalika, kasi ambayo nayo pia itapunguza ukopaji, kasi ambayo itahimilika. Tukiweka tu *for the sake* tutakuwa tunajiingiza mahali pabaya, lakini tungeweza kuhakikisha kwamba tunajua vianzio na vianzio vile tunajua *deploy quickly* na vingine vinachukua muda sana hiyo ni moja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mchangiaji anachangia ni vizuri tukamsikiliza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pili suala hili la *subsidy* na suala hili la kuhifadhi/kuweka *strategic reserve* ya mafuta. Mimi nafikiri hivi tuangalie *options* za hii kwa sababu unaweza ukaweka akiba kwenye fedha au ukaweka akiba kwenye bidhaa; ukiweka akiba kwenye bidhaa ya mafuta, bidhaa ya mafuta inabadilika badilika bei, kwa hiyo unaweza ukanunua mafuta leo ni dola 100 kwa *bulk,* lakini baada ya siku chache hizi zinazokuja miezi mitatu ikaja mafuta yakashuka bei yakawa dola 73 kwa *bulk,* utakuwa umeshapata hasara ya dola 25 kwa *bulk*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ungeweza ukanunua *option futures option*, *future options* ni kwamba unailipia *premium* kidogo lakini yule m-*supplier* atakwambia endapo unahitaji mafuta kwa mwezi unaokuja wa Juni, mwezi unaokuja wa Julai, Septemba, utampa *stagged delivers.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila *staggered delivery* inategemea ni muda gani unailipia *premium* yake na ile *premium* unayolipa ni *option* kwamba naweza nikanunua au nisinunue. Kama itakuwa bei imeshuka sitanunua kwa ile bei ambayo *nimei-hedge* kama ikipanda basi nitanunua kwa sababu najua kwamba nimekua nimei-*hedge* ile bei kwa bei ambayo ni ya leo na bei ya leo ndiyo hii sasa nimeshalipa *subsidy* na ile *subsidy* badala ya kuitumia kugawa ingetumika kununua *futures options* za kuletewa mafuta kwa bei ambayo tunaijua ya leo, hapo utakuwa ume-*stabilize*. Pia itapanda huna *pressure* ya kwamba bei itapanda halafu nitanunua kwa sababu

umei-*hedge* na ile gharama ya ku-*hedge* ni *very little* ya ile *volume* ambayo tunaweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kwamba tukae chini wale watu ambao wanajua *financing* na hizi *hedging* na *features* tufanye kitu ambacho kinakubalika kitakaa *forever* na kila wakati *TPDC* ipate hiyo *option ya formular* inanua mafuta kwa bei ambazo zinajulikana leo lakini kwa ku-*deliver in the feature* kama ni *six months.* Kwa sababu kama wewe utanunua tu yaani hivi vitu haviendi tu kiholeholea utapata hasara, tutakuja kupata hasara tuhangaike bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kwamba tunapozungumza suala zima la kuzalisha na mimi nakushukuru sana, kipaumbele alichokiweka pale cha uzalishaji na usambazaji. Wanasema hivi, asilimia 78.4 ya Watanzania wamefikiwa na gridi, lakini watu waliounganishwa kwenye gridi ni asilimia 37.7 tu! Wengine hawajaunganishwa na wengine wanaotumia tunasema umeme upo lakini watu wanaotumia *solar* na tunashukuru Serikali hii tukufu ambayo iliweza kushusha *VAT* kwenye *solar panels,* sasa watu asilimia 30 ya Watanzania wanatumia *solar!* Kwa hiyo, inakuwa *about 66 percent* ya Watanzania wanapata umeme lakini wengi nusu yao wanapata kwa *solar* lakini umeme wa *solar* hauwezi kufanya mambo fulani fulani ya viwanda na nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pamoja na hela tulizonazo nyingi hizi tujaribu kuona ni wapi tukimbizane napo ambako ni kusambaza umeme wa gridi ku-*stabilize* ili kile kiwango tulichonacho kiweze kutumika vizuri kisipotee na kila mtu aweze kupata umeme ule usambazwe ufike kwenye nyumba zetu na kwenye

viwanda vidogo vidogo na kwenye maeneo yetu, shuleni na kwenye hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikifanyika hivyo sasa tunaanza kuona tija ya hiki tunachozalisha na hicho ambacho kinapangwa kuzalishwa kwa kuongeza tusikimbizane tu tunafuta lakini tunataka ufafanuzi je, mnasema mta-*export* kama mta-*export;* je, mna bei za ku-*export* kweli ambazo mmeshazifungamanisha vizuri mkajua kwamba mtapata faida? Tusije tuka-*subsidize* kwa wenzetu umeme na sisi tumejenga kwa fedha ya kukopa hiyo ni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba pengine kitu ambacho kingetakiwa pia tukiangalie ni suala zima la kujua mikakati gani hili suala la *stabilization project* kwamba je, itatekelezeka kwa muda gani? Kwa sababu fedha ambayo inahitajika sidhani kama imetengwa yote, walisema Bilioni 500 au Milioni 500, naona hata muda wa kuzungumza unaisha lakini ninaunga mkono hoja, naamini kwamba kweli kuna mambo mazuri yanafanyika kwenye Wizara na mimi nampongeza sana Mheshimiwa January kwa yote hayo anayofanya, waendelee kufanya na waendelee kutuletea vitu vizuri, *summaries* ambazo zimekaa hivi zinasaidia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Daktari Charles Kimei kwa mchango wako lakini kwa kuweza kuwasiliana na Kiti, maana niliposhika *mic* tu ukasema naunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Benaya Kapinga wakati huo mtoa hoja anajiandaa.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa dakika tano ulizonipa, ahsante sana. Nami niungane na wenzangu kuipongeza Wizara na Serikali kwa ujumla. Kwa dakika tano hizi naomba nizungumze jambo moja suala la *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza michango ya Wabunge wenzangu humu ndani wamezungumza kwa hisia sana na wamezungumza kwa hisia kwa namna mradi wa *REA* unavyotekelezwa kwenye Majimbo yao. Pamoja na hisia hizo baadhi ya Wabunge wenzangu atakwambia vijiji vilivyobaki katika Jimbo lake 10, 11, 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa jimbo langu linavijiji vikubwa vipo 117, kati ya vijiji hivyo vijiji vilivyopata umeme ni vijiji 34 na kwa bahati mbaya kati ya vijiji hivyo 34 vijiji Tisa zimesimikwa nguzo tu lakini tunasema vimepata nini umeme, vijiji 86 vyote havina umeme, Kata 15 hazina umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemuomba sana Roho Mtakatifu anishukie hapa nizungumze kwenye kona zile za Mheshimiwa Spika. Kwa sababu wenzangu wamezungumza hapa kwa hisia kali sana ni vijiji 10,15, 20, mimi vijiji 86 ongeza Tisa ni vijiji vingapi havina umeme? Kwa hiyo, kwa masikitiko makubwa sana, nashukuru sana Mheshimiwa Waziri nakuheshimu sana na bahati nzuri nilikuja kukuona umenipa ushirikiano mzuri, ukanikutanisha na Mkurugenzi *REA* naye alinipa ushirikiano mzuri akanikutanisha na Wakurugenzi wake, Wasaidizi wake na bahati nzuri akamuita na Mkandarasi. Kwahiyo, niombe yale tuliyokubaliana yale tuliyozungumza na moja ulilolisema ni kuja Mbinga kuangalia hali ya utekelezaji wa huu mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua ujio wako utatoa *push* sasa tunasema vijiji 23, vijiji 9 zimesimikwa nguzo tu, nguzo imesimikwa hivyo vijiji vingine mwenzangu alisema hapa jana kwamba utekelezaji wa huu mradi ni 0.5, maana yake ni kama wameenda ku-*survey* tu, yaani wamefanya *survey* tu na pengine wamelaza nguzo. Kwa hiyo, kwa ujumla mradi huu Jimbo la Mbinga na nilimwambia waziri sehemu itakayokuonesha wewe umeshindwa kutekeleza mradi huu kwa asilimia 100 ni Mbinga na kama si Mbinga basi Mkoa wa Ruvuma kwa sababu hata Tunduru kuna vijiji 86 havijaingiziwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Waziri atakapofanya majumuisho hapa atueleze namna ya kasi itakavyokwenda katika Jimbo la Mbinga Vijijini ili ifikapo Desemba kama walivyoahidi nasi vijiji vyetu vyote viingie kwenye umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine napata faraja kidogo wanasema kawia ufike, nimeona kwenye hiki kipeperushi kwamba tunaenda kusambaza umeme sasa kwenye vitongoji hasa kwa vile mimi vijiji vyangu 86 havipo kwenye mradi huu vimechelewa kuingia kwenye mradi wa umeme; 86 sasa tunaenda kwenye vitongoji ninauhakika tutaanzia huko na vitongoji kwamba sasa vitongoji vyote na vijiji vyote vitapata umeme ninauhakika huo najua hautaniangusha hapa kwasababu tumechelewa kusubiri umeme sasa tuna bahati sasa tunaaanza vitongoji na kwasababu sisi tulichelewa zaidi basi tutaanzia hapo ndiyo maana nimefarijika kusema kawia ufanye nini? ufike na kutangulia sio kufanya nini? kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona niseme hilo tu kwa hizo dakika na nashukuru sana kwa kuniruhusu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa Benaya Kapinga.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Nishati, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Spika, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Nishati kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa ustawi wa jamii na maendelo endelevu, na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/26 ambayo ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa kuendelea kutekeleza kwa ufanisi mkubwa miradi ya umeme ikiwemo miradi ya kusambaza umeme vijijini *(REA)* na ujenzi mkubwa wa Bwawa la Julius Nyerere *(JNHPP)* litakalozalisha umeme wa megawati 2,115. Miradi hii ya kusambaza umeme vijijini imeiweka Tanzania katika nafasi ya juu Afrika na imeweza kuchochea kasi ya ukuaji wa viwanda na uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto za vita ya Ukraine na Urusi na kupelekea kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli, napongeza Serikali kushirikisha Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha, *EWURA* na wadau wengine kuweka mkakati wa kuanzisha Mfuko wa Kudhibiti Mabadiliko ya Bei za Mafuta *(Fuel Price Stabilization Fund)* ili kukabiliana na kupanda kwa bei za mafuta. Pia Serikali inachukua hatua stahiki za kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Kimkakati ya Mafuta *(Strategic Petroleum Reserve-SPR)* ili kukabiliana na dharura na kuimarisha usalama na uhakika wa mafuta kwa Taifa. Mkakati huu uende sambamba na uanzishaji wa bandari kavu Mbeya na ujenzi wa matenki makubwa kuhifadhi mafuta kwa nchi jirani za Zambia, DR Congo, Malawi na pia kwa matumizi ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *REA* kuendelea kutekeleza miradi ya kupeleka umeme kwenye makao makuu katika vijiji vyote vya Jimbo la Mbeya Vijijini bado kuna uhitaji mkubwa wa umeme kufika kwenye vitongoji vyote. Napendekeza kuendelea kwa kasi utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mradi wa *REA III (REA III, Round II)* na kufikisha umeme katika vijiji vyote vilivyobakia na pia kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Ujazilizi *(Densification)*. Napendekeza utekelezaji utoe

kipaumbele kwa kata za Itawa na Shizuvi ambavyo hakuna kijiji kilichowashiwa umeme, na pia kwenye vitongoji vinavyolizunguka Jiji la Mbeya ikiwemo Mina na Lusungo Kata ya Iwindi, Kijiji cha Shongo, Kijiji cha Wambishe kwenye shule zote ikiwemo Shule ya Sekondari Iwiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vijiji vilivyopatiwa umeme kwa kiasi kikubwa imechochea ukuaji wa viwanda hasusani viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo. Nashauri *TANESCO* iongeze *speed* ya kuunganisha umeme na pia kushughulikia maombi ya wateja wengi wanaosubiri umeme ikichukuliwa hii ni fursa pia kwa *TANESCO* kuongeza mapato ya shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na vyanzo vya sasa, napendekeza Serikali itekeleze miradi ya vyanzo vingine kama vile vyanzo vya Jotoardhi, Umeme wa Jua, Upepo na Makaa ya Mawe ili nchi yetu iendane na mahitaji makubwa ya umeme kwa hapa Tanzania na hata nchi zingine za Afrika. Ni muda mrefu sasa, *TANESCO* kupitia Kampuni tanzu ya Uendelezaji wa Jotoardhi nchini *(TGDC)* inaanze uzalishaji katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo eneo la Ziwa Ngozi, Kata za Ijombe na Bonde la Songwe Mkoani Mbeya ambapo ndipo yalipo makutano ya Bonde la Ufa la upande wa Mashariki na lile la Magharibi.

Napendekeza Serikali iharakishe utekelezaji wa miradi hii ya Jotoardhi na ule wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma na Kiwira ili tuweza kuzalisha umeme zaidi kwa mahitaji ya ndani na nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia amani, upendo, afya, mshikamano na utashi wa kisiasa katika Taifa letu. Aidha, tunampongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa usimamizi wao thabiti katika utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2022-2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawapongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika wetu, Mawaziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote Serikalini kwa kuitumikia vizuri sana nafasi zao kikamilifu hongereni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali na Wizara waangalie upya wa kutafuta fedha zaidi katika kufanikisha mpango wa kupeleka umeme kwenye vijiji ambavyo bado hadi sasa *line* kubwa haijafika ili kurahisisha utekelezaji wa dhamira ya Serikali yetu na Ilani ya CCM ya mwaka 2020-2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa malengo ya Serikali ya kupeleka umeme kila kijiji unasubiriwa na wananchi kwa hamu kubwa sana, na kwa kuwa bado kuna maeneo makubwa ambayo makandarasi tayari wamesimika nguzo zaidi ya miezi sita sasa, tunaiomba Serikali iwalipe makandarasi fedha zao kwa kazi ambayo tayari wamekamilisha ili waweze kuwasha umeme katika baadhi kwenye majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapendekezo ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati kiasi cha fedha zilizotengwa kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu

mzunguko wa pili ni kidogo sana kulingana na mahitaji halisi ya mradi huu wa shilingi bilioni 1.240. Hivyo basi ni muhimu Serikali iangalie mpango mbadala wa kutafuta fedha zaidi, na mradi huu ni muhimu sana ukaanza kwenye vijiji ambavyo *line* kubwa ilishapita kwa zaidi ya miaka mitatu na maeneo yenye uzalishaji mkubwa kwa mfano taasisi za umma na binafsi, taasisi za dini, migodi, vijiwe vyenye biashara na maeneo ambayo yana uwezekano wa kuanzishwa viwanda vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri kupitia hotuba yake aweze kutoa kauli ya Serikali kuhusu matumizi sahihi ya *unit* kwa watumiaji wadogo hususan umeme wa matumizi majumbani. Kwani eneo hilo lina mkanganyiko kati ya *TANESCO* na *TRA,* na wananchi wa kipato cha chini vijijini kuona tofauti ya umeme wa matumizi na ule wa kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho siyo kwa umuhimu, tunaiomba Serikali itume utafiti kuzalisha umeme wa upepo ili kuongeza vyanzo vya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara ya Nishati kwa kazi nzuri wanayoifanya na mikakati mizuri ambayo wameipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza *TANESCO* kwa mfumo rahisi wa maombi ya huduma ya umeme kwa njia ya mtandao ambayo inamuwezesha mteja kupata huduma mbalimbali bila kufika katika ofisi za *TANESCO.* Natoa rai kwa Serikali kutoa elimu zaidi kwa wananchi ili wauelewe mfumo huu ili kupunguza usumbufu na

mazingira yote ya rushwa na kurahisisha upatikanaji wa huduma ya kuingiza umeme kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa hatua kubwa ya majadiliano kuhusu mradi wa *LNG* Lindi. Ni hatua gani majadiliano yamefikia mpaka sasa na lini mradi huu utaanza na kampuni zipi zinahusika na mradi huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo kama kuna *National Fuel Reserve*; kama ipo ni kiasi gani? Katika changamoto tunazopitia za upatikanaji wa mafuta kama nchi ni lazma tuwe na *Strategic Fuel Reserve*. Serikali ianzishe *Fuel Price Stabilization Fund* ambapo kukitokea kuvurugika kwa bei ya mafuta duniani Serikali iweze kuingilia kati na kutumia hii *fund* kutuliza bei za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nawatakia utekelezaji mwema wa vipaumbele vya bajeti.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuwapongeza kwa hotuba ya bajeti ambayo iko *well detailed,* aidha, nawapongeza kwa ubunifu wa kutuletea maonesho hapa kwenye viwanja vya Bunge. Ilitusaidia sana kupata uelewa sio tu wa masuala ya umeme lakini nishati kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla utendaji wenu kuanzia *TANESCO* hadi *REA* ni wa kuvutia na shirikishi. Aidha, kwa niaba ya wananchi wa Mafinga, Mufindi na Mikoa yote ya Iringa na Njombe tunawapongeza na kuwashukuru ambavyo tumeshirikiana katika suala la Serikali kukubali kuendelea kununua nguzo za umeme hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu; ninatambua kwamba ni haki ya kila Mtanzania kufikishiwa umeme. Hata hivyo pamoja na kuwa umeme ni huduma, lakini pia ni biashara, kwa sababu hiyo nashauri baadhi ya maeneo kama Mafinga na Mufindi ambako kuna viwanda vingi tuanze kuelekeza nguvu huko ambako umeme ni biashara ili *TANESCO* ipate *returns* ambayo itaenda kugharamia umeme kule ambako wao ni huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu ni pamoja na kutufungia transfoma zenye *KV* kubwa na kuwapa *TANESCO* bajeti kubwa. Hili linaweza kufanyika kwa kuangalia tu mapato katika maeneo hayo kama Mufindi, mtabaini wazi kwamba *TANESCO* inapata mapato makubwa, kwa hiyo, hapa tunapopata mapato makubwa tuongezewe nguvu ili mapato yaongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa muktadha huo nawasilisha maombi ya Mradi wa Ujazilizi kuwa na wigo mpana hasa katika vijiji vya Halmashauri ya Mafinga Mji ambayo *administratively* ni mji lakini una vijiji kumi na moja, ambapo Kijiji kama Matanana wananchi wana mashine za kuchana mbao lakini wamezifungia ndani kama ambavyo wananchi wa Kata ya *Sao Hill* ambapo kuna ujenzi wa shule ya sekondari chini ya mradi wa *SEQUIP* wamefungia ndani mashine zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali iko sawa katika Kijiji cha Ndolezi na pia Mitaa ya Luganga, Mtangani, Majengo mapya katika Kata ya Wambi. Hali hii pia iko katika Mtaa wa Lumwago ambao wanaishi vijana wengi wanaojenga kwa kasi sana, kama ambavyo hali hii ipo Ifingo, Miami na Kijiji cha Rungemba na Itimbo ambako kuna eneo kubwa la viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu hiyo nashauri kwamba *densification* na bajeti ya *TANESCO* walau iongezeke kuendana na kasi ya ukuaji wa Mji wa Mafinga na hasa kuelekea katika maeneo ya uzalishaji kwa maana ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa nimeshatuma mchango wangu kwa maandishi, nimewiwa kushauri jambo kuhusu LUKU, je, hatuwezi kutumia mifumo ya kisasa kama tunavyofanya katika huduma za ving'amuzi ambapo ukinunua tu inaji-*update* yenyewe *automatic*? Nashauri tuje na mfumo huo.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Nishati Ndugu January Makamba na Naibu wake *Engineer* Stephen Byabato pamoja na jopo la wataalamu wa Wizara kwa kazi kubwa wanazofanya kupeleka umeme na nishati nyingine muhimu kwa wananchi wetu hapa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utahusu umuhimu wa kupeleka huduma ya gesi asilia katika Jimbo la Moshi Vijijini na huduma ya umeme katika maeneo ambayo hayajaunganishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya bajeti Waziri ameeleza kwamba kuna mradi wa gesi asilia utakaojengwa kupeleka huduma hii Mombasa nchini Kenya. Katika hotuba yake, ameeleza kuwa mikoa ya Pwani, Tanga Kilimanjaro na Arusha itanufaika na mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Moshi Vijijini limepakana na Mlima Kilimanjaro, wananchi wengi hutegemea nishati ya kuni kutoka katika misitu ya Mlima Kilimanjaro na maeneo mengine ya jirani. Wanasayansi wamesema kwamba matumizi ya kuni kwa kiasi kikubwa yamesababisha uharibifu wa mazingira na nishati mbadala inahitajika kukabiliana na changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ujio tarajiwa wa mradi wa gesi asilia Mkoani Kilimanjaro, ninaishauri Serikali ianze kwa kusambaza miundombinu ya gesi hii katika vijiji vinavyozunguka Mlima Kilimanjaro ili kuunusuru mlima na ukataji wa nishati ya kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali kupeleka umeme vijijini, bado wananchi wengi wa Jimbo la Moshi Vijijini hawajapatiwa nishati ya umeme. Hivyo basi ninaiomba Wizara ya Nishati isaidie kutatua changamoto za nishati ya umeme katika jimbo langu la Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yenye changamoto ya umeme Jimbo la Moshi Vijijini ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kimochi, Kitongoji cha Kiwalaa kilichopo Kijiji cha Sango, Kitongoji cha Iryaroho kilichopo katika Kijiji cha Mowo na Kitongoji cha Maryaseli katika Kijiji cha Lyakombila havina umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali ikamilishe ujenzi wa miundombinu ya umeme katika maeneo niliyotaja hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Okaoni, vijiji vya Sisamaro, Omarini na Mkomilo vinahitaji kuunganishwa japo baadhi ya maeneo nguzo zimepita ila bado kuunganishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Kindi, Kijiji cha Chekereni Weruweru, Vitongoji vya Miembeni, na Kisiwani havina umeme kabisa, ninaiomba Serikali ipeleke huduma kwenye vijiji hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kayta ya Kibosho Kirima, Mbunge ametokea kata hii. Kama nilivyoomba mwaka jana katika Kijiji cha Boro kwenye vitongoji vya Boro Kati na Boro Juu (anakotokea Mbunge), *voltage* za umeme ni kidogo sana na hupelekea kushindwa kuendesha vifaa vya ndani kama friji na vyombo mbalimbali vya ndani. Mashine za *welding* (kwenye vitongoji hivi) na *pump* ya kuvuta maji katika shule ya sekondari Masoka hushindwa kufanya kazi kutokana na umeme kidogo. Wajasiriamali wameshindwa kuweka mashine za kusaga unga, mashine za kutengeneza matofali na miradi mingine midogo inayohitaji umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wa bweni wa sekondari ya Masoka hushindwa kupata huduma ya umeme ili wajisomee usiku kutokana na umeme kidogo. Umeme huwaka kuanzia saa tano usiku. Ninaiomba Wizara isaidie kutatua changamoto hii, kwani pamoja na maombi yangu mwaka jana, bado Wizara haijatusaidia kutatua changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kibosho Mashariki, kama nilivyoomba kwenye bajeti ya mwaka jana inahitaji huduma katika Kijiji cha Sungu Vitongoji vya Kyareni na

Nkoitiko havijaunganishwa; katika Kijiji cha Singa, Kitongoji cha Singa Juu hakijaunganishwa; na katika Kijiji cha Mweka, kitongoji cha Mweka Juu na Omi havijaunganishwa. Ninaiomba Serikali ipeleke huduma kwenye vijiji na vitongoji vilivyotajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Kibosho Kati, kama nilivyoomba kwenye bajeti ya mwaka jana, Vijiji vya Uri na Otaruni umeme una nguvu kidogo *(low voltage)* na kunahitajika transfoma. Katika Kijiji cha Otaruni, Kitongoji cha Ngoroshi hakuna umeme na tunaomba wananchi wapatiwe huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoomba kwenye bajeti ya mwaka jana, katika Kata ya Uru Mashariki, Kijiji cha Materuni, Kitongoji cha Wondo hakijaunganishwa, ninaiomba Serikali ipeleke huduma kwenye kitongoji hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Mbokomu kama nilivyoomba kwenye bajeti ya mwaka jana, Kitongoji cha Mmbede Kyaroni, Tema na Masanga na baadhi ya maeneo ya Korini Kati havijaunganishwa, pia ninaiomba Serikali ipeleke huduma kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoomba kwenye bajeti ya mwaka jana, katika Kata ya Mabogini sehemu ambazo hazijapata umeme hadi sasa ni Vitongoji vya Sanya *"Line A"* na Mjohoroni vilivyopo katika kijiji cha Mabogini; Kitongoji cha Uru - katika Kijiji cha Muungano; katika Kijiji cha Maendeleo, Vitongoji vya Mshikamano na Uarushani; Mgungani - katika Kijiji cha Mtakuja, na katika Kijiji cha Mserekia hakuna umeme katika Vitongoji vya Mbeya kubwa, Mbeya ndogo, Remit, Mkwajuni, na Mafuriko. Kijiji cha Mji mpya, Kitongoji cha Utamaduni

hakijaunganishwa. Ninaiomba Serikali ipeleke huduma kwenye maeneo yaliyotajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. SAADA MONSOUR HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kuipongeza Wizara ya Nishati chini ya ndugu yangu Mheshimiwa January Makamba kwa kazi kubwa anazozifanya kwa kuhakikisha Taifa letu linaendelea kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni kuhusu Bwawa la Mwalimu Nyerere lililopo Rufiji, napongeza ujenzi kufikia asilimia zaidi ya 60. Bwawa hili ni muhimu sana kwa maendeleo na pia tunalitegemea kuboresha hali ya umeme hadi Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mkoa wangu wa Kaskazini Unguja kuna uwekezaji mkubwa wa hoteli kubwa na ndogo ndogo, ujenzi wa hoteli hizi kwa kiwango kikubwa utakwenda kusaidia wananchi kwa kupata ajira na fursa za biashara. Aidha bwawa likikamilika uzalishaji ukianza hoteli zitapata umeme wa uhakika na wananchi wa Zanzibar watafaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ihakikishe fedha zinapatikana kwa miradi yote kutoka Hazina kwa wakati ili ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere usikwame na uende kwa muda. Ahsante.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika

hotuba hii ya makadirio na mapato ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwasilisha hotuba hii katika Bunge lako tukufu kwa ufasaha na umakini mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; nikianza na usambazaji wa umeme vijijini. Napenda kuipongeza Serikali yetu kwa kuendelea na utararibu wa kusambaza umeme vijijini. Katika nchi yetu ya Tanzania sasa hivi kuna engezeko kubwa la mahitaji ya umeme. Hivyo ni jambo jema sana kuwapelekea nishati hii wananchi wetu. Umeme una matumizi mengi lakini mpaka sasa wananchi wa vijijini wanaelewa kuwa umeme unatumika kwa matumizi ya taa za majumbani mwao tu, hii sio sahihi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika jambo hili kwa Wizara ni kuweka utararibu maalum wa kwenda vijijini kwa lengo la kuwaelimisha matumizi sahihi ya umeme, kama vile kupikia ili kunusuru ukataji wa miti ambao hivi sasa unaendelea kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa gesi asilia; Tanzania tunapaswa kumshukuru Mungu kwa kutujaalia kuwa na gesi asilia katika nchi yetu. Gesi ni nishati muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Nchi yetu ilipogundua nishati hii wananchi tulijawa na matumaini makubwa. Tulidhani kuwa usambazaji wa nishati hii tulitegemea kuwa itasambazwa kwa *speed* ile kama inavyosambazwa nishati ya umeme

inavyosambaa, lakini mpaka leo usambazaji wa nishati hii hauridhishi hata kidogo. Bado wananchi wanaotumia nishati hii ni wachache mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika jambo hili kwa Wizara ni kuweka utaratibu maalum wa kuisambaza huduma hii kwa wananchi wa mijini na vijijini ili kukidhi matumaini ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu deni la *TANESCO* kwa *TPDC; TANESCO* kwa muda mrefu sasa wamekuwa wa kudaiwa fedha nyingi na *TPDC*. Deni hili ambalo ni zaidi ya bilioni mia tano ni deni ambalo linaudhi sana kuona kila mwaka linajitokeza kwenye vitabu vya bajeti na wakati mwingine kwenye vitabu vya wakaguzi. Masharika haya mawili yote yako chini ya Wizara moja hivyo ni jambo la aibu kidogo kuona kuwa mpaka sasa halijapatikana ufumbuzi wake.

Ushauri wangu katika jambo hili kwa Wizara ni kuwaelekeza Maafisa Mausuuli wa Mashirika haya mawili kukaa pamoja kutafuta namna ya kulisawazisha deni hili. Matumaini yangu ni kwamba suala hili litapatiwa ufumbuzi muafaka na halitajitokeza tena kwenye vitabu vya ripoti za wakaguzi na ripoti nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ushirikiano kati ya *TANESCO* na *ZECO; ZECO* na *TANESCO* ni mashirika mawili katika nchi yetu ya Tanzania yanayoshughulika na usambazaji wa umeme. Mashirika haya ni vyema yakaimarisha ushirikiano wao katika nyanja zote. Hivi sasa inaonekana ushirika wao upo kwenye mambo ya kiufundi tu na sio kwenye ngazi za maamuzi. Hapo zamani ushirikano wao ulikuwa mpaka kwenye mambo ya maamuzi. Kwa mfano ulikuwepo

ushirikishwaji wa *member* wa bodi ya mashirika hayo kuhudhuria kwenye vikao vya maamuzi ya mashirika hayo. Kulikuwa na utaratibu wa mjumbe mmoja wa kila upande kuhudhuria kwenye vikao vya maamuzi ya mashirika haya. Ushauri wangu kwa Wizara kuchukua juhudi za makusudi kuurejesha utaratibu huu kwa maslahi ya pande zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwakilisha.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutulinda na kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Hii ni kwa sababu sikuweza kupata nafasi ya kuchangia kwa njia ya hotuba Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Wizara iangalie na kukiondoa Kijiji cha Kilolo ambacho ndipo makao makuu ya Wilaya yalipo. Hiki ni kijiji na si mji na kina hati ya Kijiji, kina Serikali ya kijiji na kina vitongoji; kwa hiyo siyo sawa wao kuwekwa kwenye orodha ya miji na kulipa zaidi ya shilingi 27,000. Ifahamike kwamba vipo vijiji vyenye hali bora zaidi kuliko Kilolo na vinalipa shilingi 27,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umuhimu wa kutengeneza kanuni na taratibu za kusajili vituo vya vijijini; hii itapunguza gharama za mafuta na kufanya biashara halali kuliko sasa ambapo biashara haramu na hatari inaendelea.

Kuhusu Bwawa la Mwalimu Nyerere naiomba Serikali kuweka mkazo katika ujenzi wa bwawa hili na kuondoa vikwazo vyote vinavyochelewesha ujenzi huo.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu kwa ajili ya Mheshimiwa Rais Mama Samia kwa kazi nzuri anayoifanya kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Wizara nzima ya Nishati kwa kazi nzuri pamoja na changamoto zilizopo, lakini mmekuwa mnapambana nazo na zinaendelea kutatuliwa, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kuchangia kuhusiana na Jimbo la Temeke ukizingatia ni mji mkongwe na miundombinu ya umeme ni ya muda mrefu. Kwanza nguzo nyingi zimeoza hivyo kupelekea kuanguka kila mara na wananchi kukosa umeme, lakini pia miundombinu inayopita chini ya ardhi inasumbua muda mrefu, niiombe Wizara hii iangalie namna Temeke itakavyoweza kurudi kwenye hali ya kawaida kwani bado umeme wetu tunapata kutokea Ilala. Ni mkakati gani sasa Serikali itafanya kuhusu Temeke kwani ni jimbo lenye viwanda vingi, umeme hautoshi na tunakosa mapato ya ndani kwani kila tukitembelea viwandani umeme haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana mtuangalie upya kwani hali si nzuri, hata *TANESCO* mnakosa mapato kwani viwanda vingi hawalipi kulingana na utumiaji wa umeme kwani umeme ukipatikana kwa mfululizo nao watafanya kazi kwa muda mrefu na *bill* zitakuja na kuleta mapato ndani ya Shirika la *TANESCO*. Niiombe Wizara itushughulikie tupate umeme katikati ya Jiji la Dar es Salaam ambalo ni jiji la biashara, kukosa umeme haieleweki, mtuangalie. Ahsanteni sana.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu

kwa kunipa uhai na uzima. Nishukuru pia kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake za makusudi kabisa kuwa na utashi wa kupunguza ukali ya bei ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa January Makamba - Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Wakili Msomi Byabato - Naibu Waziri wa Nishati pamoja na watalaam wote wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri mnayoifanya ili kuhakikisha wananchi wanapata umeme. Chapa kazi msigeuke nyuma mkawa mlima wa chumvi, songa mbele na Mungu atawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee kwenye hotuba ya bajeti iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri na kuchangia kwenye vipengele vifuatavyo; kwanza katika hotuba yake ya bajeti Mheshimiwa Waziri ameeleza kuwa gesi asilia sasa itapelekwa nchini Uganda. Niishauri Serikali ihakikishe mikoa ambayo gesi hii inapitia wapate huduma hii ya gesi asilia majumbani kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida yake kwanza itafanya wananchi kujiona ni sehemu ya mradi na kuwa walinzi wa bomba hilo lisihujumiwe na itapunguza gharama za matumizi ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migodi kuunganishwa kwenye gridi ya umeme ya Taifa, migodi hii inatumia umeme mwingi hivyo ni chanzo cha mapato kwa *TANESCO*. Pia *exemption* kwenye mafuta Serikali inapoteza fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya gesi asilia kwenye magari na Wizara ya Nishati na Taasisi zilizo chini ya Wizara kutumia gesi asilia, niombe na kushauri litolewe tamko kwa magari yote ya Serikali na Taasisi zote magari yake yatumie gesi ili kubana matumizi ya Serikali kwa kipindi hiki ambacho mafuta yamepanda bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungehamasisha matumizi ya gesi asilia kwa wananchi wote, lakini hapa kikwazo ni gharama ya ubadilishaji wa mfumo wa gari kwenda kwenye gesi. Kiasi cha shilingi milioni mbili ni kikubwa mno. Ushauri wangu uangaliwe uwezekano wa kupunguza gharama lakini pia viwekwe vituo vya kutosha vya ubadilishaji mifuko ya magari, kwa kuanzia kila Wilaya ili huduma ipatikane kirahisi wananchi waweze kutumia gesi kwenye magari yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipongeze Shirika letu la *TANESCO* kwa jinsi linavyobadilika kwa haraka sana. Kwa mimi niliyefanyakazi Wizara ya Nishati ukilinganisha miaka hiyo ya 1990 na sasa ni vitu viwili tofauti kabisa kazi imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Shirika kuanzisha *Nikonekt App* ambayo itarahisisha huduma za kufungiwa umeme kwa Dar es Salaam, Pwani na sasa imezinduliwa Kanda ya Kati na Kanda ya Kaskazini. Hii itaondoa ukiritimba na wateja kupoteza muda ambao ungetumika kufanya shughuli zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa watumishi; watumishi wengi wanafanya kazi kwa mikataba kwa muda mrefu na kwa weledi na uadilifu.

Shida na changamoto iliyopo wanapotangaza kazi, hawa hawapewi kipaumbele, wanaajiriwa wapya, matokeo yake na mikataba yao inavunjwa, wanakuwa mitaani, baada ya muda wanafuatwa tena wafanye kama vibarua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili tunapoteza watumishi wenye uzoefu na waliolitumikia shirika kwa uaminifu. Pia tunavunja sheria ya kibarua ambaye hutakiwa kufanya kazi kwa muda wa miezi mitatu. Nikuombe Mheshimiwa Waziri wasaidie hawa watumishi waliolitumikia shirika kwa muda mrefu, wale wenye sifa wapewe ajira za kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya Wizara iliyoletwa mbele yetu na baada ya kuunga mkono naomba nichangie baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la uunganishaji wa Mkoa wa Rukwa na gridi ya Taifa; ili kuwa na umeme wa ukakika kwa Mkoa wa Rukwa ni sisi kuunganishwa na gridi ya Taifa. Sisi wananchi wa Mkoa wa Rukwa tumekuwa na umeme usio na uhakika ukitokea nchi ya jirani ya Zambia ambao umekuwa ukikatika mara kwa mara. Zipo taarifa ambazo zimekuwa zikitolewa na *TANESCO* kwamba kukatika huko kumekuwa kukitokana na umbali mrefu ambao umeme huu umekuwa ukisafirishwa, wakati mwingine tunapoambiwa hitilafu inatokea nchi jirani, lakini kiuhalisia unakuta nchi jirani umeme unakuwa unawaka bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijaribu kufanya utafiti tunaambiwa mkataba ulioingiwa wa kuuziwa umeme kutoka Zambia bei ni ndogo ukilinganisha na bei wanayouza kwa wananchi wao, hivyo wanaona hakuna tija ya kuuza umeme upande wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuwe na umeme wa uhakika ni pale tu Mkoa wa Rukwa utakapounganishwa na gridi ya Taifa mpango ambao ulikuwa ukitajwa na Serikali kwa muda mrefu. Jambo la kushangaza katika kipindi hiki cha bajeti ya Wizara katika kazi ambazo zimepewa kipaumbele kutekelezwa ni pamoja na kuiunganisha mikoa ya Katavi na Kigoma kwenye gridi ya Taifa bila kuutaja mkoa wa Rukwa ambao ndiyo mkoa uliouzaa mkoa wa Katavi. Siamini kama Wizara imekusudia kuuruka mkoa wa Rukwa. Hivyo niiombe Wizara ihakikishe mkoa wa Rukwa unawekwa kwenye vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hoja ya wakandarasi waliopewa kazi za kusambaza umeme vijijini kwa kupitia *REA* kwa kuachia miradi njiani bila kuikamilisha na bila kutoa maelezo kuonesha tatizo ni nini na ukubwa wa tatizo na kwamba tatizo hilo linatatuliwaje ili wananchi wapate huduma yao ya msingi, tatizo hili ni kubwa sana kwa wananchi wa Kalambo ambapo katika vijiji 111 kuna vijiji zaidi ya 40 havina umeme. Naiomba Wizara itupie macho yake kwa upekee katika Wilaya yetu ya Kalambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naomba kuwasilisha.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa leo nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendeleza miradi mikubwa iliyopo kwenye sekta ya nishati. Nikitaja michache ni pamoja na Mradi wa Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - *JNHPP MW 2115* ambao sasa upo 60%; Mradi wa Gesi Mtwara na Miradi ya *REA* Awamu ya tatu Mzunguko wa Pili ambao vijijini vyote nchini vitapata umeme, pia tunaenda kuanza umeme jazilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ikitekelezwa kikamilifu tutakuwa na umeme wa kutosha kwa mahitaji yetu ya sasa na kuwa na ziada itakayotusaidia kwenye uchumi wa viwanda. Utekelezaji wa *REA* Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili ukikamilika utasaidia sana uchumi wa wananchi wetu kuanzisha viwanda vidogo vidogo na vya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali iharakishe utekelezaji wa miradi ya kimkakati katika sekta hii ya nishati ili kuchochea maendeleo ya wananchi na nchi kwa ujumla. Kwa sasa mradi wa *REA* Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili utekelezaji upo chini ya 20% na kwenye Jimbo langu la Hanang kati ya vijiji 42 hakuna hata kimoja ambacho umeme umewashwa na mkataba bado miezi sita tu. Wananchi wangu wa Hanang wanasubiri mradi huu kwa hamu kubwa, naomba Wizara iwabane wakandarasi ili utekelezaji ufanyike kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Hanang ni kati ya maeneo katika nchi hii ambapo umeme unakatika sana, kwa wastani tunapata umeme kwa 50% kwa sababu ya ukatikaji wa mara kwa mara. Niliiomba Wizara ya Nishati itusaidie kutatua kero hii kwa kujengwa kwa kituo cha kupooza umeme Hanang ili isaidie Wilaya yetu ya Hanang na maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Byabato akijibu swali langu la msingi hapa Bungeni aliahidi kuwa kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023 watatenga shilingi bilioni 2.2 kwa ajili ya kujenga kituo cha kupooza umeme eneo la Mogitu-Hanang lakini kwenye bajeti hili halionekani. Naomba sana ahadi hii iliyotolewa hapa Bungeni itekelezwe ili isionekane Wanahanang wamedanganywa kupitia Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Sasa nitamuita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Stephen Byabato, wakati huo mtoa hoja anajiandaa kwa ajili ya kuhitimisha.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwakupata nafasi ya angalau kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati nikiwa ni msaidizi wake, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutubariki na kutupa nafasi ya kukutana tena na kuleta zawadi nyingine ya Mama kama ambavyo amekuwa akisema Mheshimiwa Mwijage kutoka katika Wizara ya Nishati kama ambavyo imeanza kutolewa tangu jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa sababu ya muda nitakimbia kimbia ili nimuachie Mheshimiwa Waziri nafasi pana zaidi ya kuweza kueleza mambo makubwa zaidi ya kisera ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge katika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais

Samia Suluhu Hassan. Moja, kwa kuendelea kuwa na imani na mimi na kunibakiza nitumie neno hil,o katika Wizara hii ya Nishati nikiendelea kumsaidia Mheshimiwa Waziri majukumu lakini na kumsaidia yeye pia, lakini cha muhimu zaidi mimi nimshukuru kwa sababu yeye ndiyo anayefanya kila kitu katika Wizara yetu ya Nishati nasi tunaleta ujumbe ambao anatupatia yeye. Haya mambo yote ambayo mmeyasema hapa sisi tunayofaraja kwamba Mheshimiwa Rais ametuamini na kuturuhusu tuje kuyasema kwenu na kupokea maoni yenu na tunawahakikishieni kwamba hatutawaangusha ninyi wala hatutamuangusha Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa yale yote ambayo tumekubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya muda mimi niseme maeneo kama matano lakini kwa haraka haraka. Kwanza yametolewa maoni na maswali mengi ya msingi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge katika maeneo mbalimbali, kwa niaba ya Serikali niseme mambo kadhaa ambayo yamesemwa yapo wazi kabisa na tunayachukua tunayafanyia kazi mengine yanahitaji mjadala mpana zaidi, tutauleta hapa ili uweze kufanyiwa kazi lakini kwa sababu ya muda sasa angalau nitaje machache ambayo moja kwa moja Serikali imeyachukua na tunaahidi kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la mafuta kwa haraka haraka nikuboresha miundombinu ya kupokea mafuta pale Bandari ya Dar es Salaam na bandari nyingine na kama tulivyosema na ambavyo mmesema nyie zipo gharama ambazo zinaongezeka katika bei zetu za mafuta kwasababu ya miundombinu yetu ya kupokea mafuta kutokuwa mizuri limesemwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na tunalichukua na litaanza kufanyiwa kazi mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga *single receiving terminal,* Mheshimiwa Waziri mara kadhaa ameeleza jitihada ambazo Wizara inazifanya jinsi ambavyo tumewatafuta wadau mbalimbali ili hilo jambo liweze kufanyika na itatusaidia sisi kuwa na nafasi nzuri zaidi ya kuweza kufanya biashara ya mafuta katika hali ambayo inatuwezesha kuwa na ushindani mzuri. Wameshauri kwamba katika muda huu ambao tunajiandaa sasa tunakamilisha taratibu za kujenga *single receiving terminal* basi matenki yetu ambayo yapo pale *tipper* ambayo sisi tunayamiliki kwa sehemu kubwa basi yaweze kutumika kufanya kazi hiyo. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba hilo nalo limechukuliwa na tayari Serikali imeshaanza kulifanyia kazi na katika muda mfupi ujao mafuta yataanza kushushwa pale *tipper*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wameshauri pia *TBS* iache kuwa inazunguka na sampuli za mafuta kutoka maeneo mbalimbali na kwenda kwenye maabara moja zitengenezwe maabara kila eneo ambapo mafuta yanashushwa na hilo limechukuliwa na katika muda mfupi litafanyiwa kazi na wanaotoka maeneo hayo ni mashahidi watakuja kuwaambieni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Waheshimiwa Wabunge wameshauri zitengenezwe kanuni za kuwezesha biashara ya mafuta katika vijiji vyetu kuwa rafiki zaidi. Niseme kwanza mwaka 2020 zilishatengenezwa kanuni za kuweka mazingira rafiki katika maeneo ya miji na vijiji kufanya biashara za mafuta lakini hiyo kama haitoshi Serikali tayari imeanza kupitia upya kanuni hizo ili kuona namna ambavyo inaweza ikashusha zaidi zile gharama za wale watu wanaweka katika vituo maeneo ya vijijini na katika muda mfupi tutaona matokeo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge wameshauri kwamba mfumo wetu wa *BPS* au mfumo mwingine wowote utakaotumika katika kuagiza mafuta uzingatie kuhakikisha kwamba mafuta yanayokuja ni safi ni salama na uhakika wa kupatikana kwa mafuta hayo. Nasi tunawahakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba wakati wote ambapo tunatafuta njia nzuri zaidi ya pamoja ya kuwezesha gharama za mafuta kushuka lakini tunahakikisha tunazingatia uhakika wa upatikanaji wa mafuta katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine uliotolewa ni kuweka mazingira mazuri ya kuhakikisha wale wanaoleta mafuta wanaochezea chezea taratibu zetu hizi wakaleta katika *compartment* yao unakuta mtu ana Meli na *compartment* tatu, *compartment* moja ina mafuta machafu nyingine mbili zinakubalika tuwashughulikie sawasawa ili kuepusha kutuchezea chezea na kututania mara kwa mara. Nami kwa niaba ya Serikali niwaahidi tutaendelea kushughulika nao kwelikweli ili waendelee kupata adabu na kutotuchezea chezea kwa sababu sisi ni *hub* ya wengine wanaotutazama kutoka huko nyuma yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeshauriwa kuhakikisha kwamba tunafanyia kazi chanzo cha umeme cha cha jotoardhi *(geotherm)* kwa kuhakikisha kwamba sheria ile tunairekebisha ili iweze sasa kukidhi matakwa ya kuwa chini ya Wizara ya Nishati na kuiwezesha pia Wizara yenyewe kuwa ndiyo msimamizi sasa mkubwa wa *TPDC* na kuipa kipaumbele *TPDC* kwa ajili ya kuweza kuleta mabadiliko katika eneo la nishati ya joto ardhi kama wenzetu Wakenya walivyofanya. Tuwahakikishieni

kwamba hilo tumelichukua na kwenye bajeti hii pesa imetengwa zaidi ya Bilioni Ishirini kwa kuendelea kuiwezesha *TPDC* kufanya kazi zake katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni maeneo ambayo kwa uchache kabisa yapo mengi sana nimeona niyagusie na mengine Mheshimiwa Waziri atakuja kuyamalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa ufupi niende kwenye maeneo mengine mawili. Eneo ambalo kila Mheshimiwa kila aliposimama ameligusia eneo la umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafurahi kwanza kwa Mheshimiwa Rais kuendelea kui-*support* sekta ya nishati kwa kupeleka umeme vijijini bila kupepesa macho bila kupepesa kope, katika hili Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amepambana kwelikweli. Ni uwazi usiopingika kwamba kwa sehemu kubwa sana umeme vijijini siyo biashara umeme vijijini ni huduma kwa sehemu kubwa sana. Kwa sababu umeme ule unaounganishwa tunazifahamu familia zetu za vijijini, kwa sehemu kubwa mtu anaweka umeme wa Shilingi 9,150 *unit* 75 anakaa nazo miezi mitatu, miezi sita siyo biashara. Pamoja na hilo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza pelekeni umeme kwenye vijiji, pelekeni umeme kwenye vitongoji na gharama ibakie kuwa Shilingi 27,000. Katika hili Wizara ya Nishati tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, Trilioni Moja na Bilioni Mia Mbili na Hamsini zipo zinaendelea kupelekwa katika maeneo yetu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba miradi ya *REA* inakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye eneo jingine tulisaini mikataba mingi kwa ajili ya kupeleka umeme vijijini, mikataba ile mingi ilikuwa inadondokea Desemba mwaka 2022, mingine ilikuwa ina *overlap* Desemba, 22 kwa sababu mkataba unamiezi 18. Sasa tuwahakikishieni kwamba wale ambao walitakiwa kukamilisha mikataba mwezi Desemba ambao walianza mapema, tutapambana nao na kuhakikisha kwamba kipindi hicho kikifika mikataba inakamilika. Wale ambao mikataba yao ilikuwa ina-*overlap* basi tutakubali kuhakikisha kwamba muda ule wa mkataba unafikiwa lakini endapo kutatokea kuongezeka kwa muda wa kukamilisha mkataba yapo mambo kadhaa ambayo yatasababisha kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yapo mawili chanya na mengine ni hasi, jambo la kwanza sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge tunapenda maeneo tunayopeleka umeme yaongezeke, sasa unapoongeza *scope* ya kazi siyo rahisi kumbana mtu afanye kazi katika muda uleule mliokuwa mmekubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine ni kuongeza wigo sasa si kazi ya awali lakini Mheshimiwa Waziri tayari ameshatoa ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuongeza kilometa mbili kwenye maeneo yetu ya vijiji sasa inapoongezwa kilometa mbili si rahisi sasa ukamilishe ndani ya uleule muda uliokuwepo wa awali. Changamoto hasi ambazo tumezipata cha kwanza ni kupanda kwa gharama za vifaa, ni uwazi usiopingika gharama zimepanda lakini tunahakikisha kwamba jambo hili tunalifanyia kazi lakini pia tumebadilisha kutoka kwenye *goods* kuja kwenye *works.* Nisema kidogo hapa huko nyuma tulikuwa tunafanya mikataba ya upelekaji wa umeme vijijini kwa kutumia taratibu zinazoitwa *goods*

ambapo mnampa Mkandarasi fedha ya kununua vifaa vyote asilimia karibia 80 ya mkataba ananunua vifaa anavitunza halafu ile asilimia 20 anaanza kufanyia kazi. Tuliona mtu anaponunua vifaa akapata faida yake anaingia mitini, sasa tukabadilisha utaratibu twende na *works* kwamba tutakulipa fedha kidogo *advance payment* asilimia 20 utanunua vifaa kidogo na pesa ya *mobilization* halafu sasa ukifanyakazi tukaja tukakagua tunakulipa. Sasa kwenye hiyo habari yakuja kukukagua tukakulipa ili ukanunue vifaa vingine tumekutana na habari ya kupanda kwa bei lakini tunahakikisha kwamba tunashughulika nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya nini katika eneo hili, hatua za utekelezaji tumeshazisema mara kadhaa, jambo la kwanza ambalo tumelifanya. Tumewaleta Wakandarasi wote chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Waziri January Makamba hapa Bungeni, wamekaa hapa siku tatu, Waheshimiwa Wabunge wameenda wamewaona, wamewahoji wamejua shida iko wapi na tunatatua vipi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo tumelifanya ni kuongeza usimamizi. Mheshimiwa Waziri ameshasema, tunao wasimamizi ngazi ya Kanda, tunao wasimamizi ngazi za Mikoa lakini sasa wanakuja wasimamizi ngazi za Jimbo, waje wasimamizi wa miradi yetu ya *REA* kwenye Majimbo yetu. Ukiamka unaamka naye ukilala unalala naye na hiyo ni zawadi nyingine ya Mama ambayo Mheshimiwa Waziri ametuambia, nia ni kuhakikisha kwamba tunafikia sehemu ambapo mradi hautakwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la tatu na la mwisho katika eneo hili; tumekaa na wakandarasi, tumejadiliana

nao, tumekubaliana kwamba jambo hili sasa liishe, waendelee na kazi wakati sisi tunaendelea na mchakato wa kurekebisha mikataba yao na kuwawekea katika mazingira mazuri. Tunaahidi kwamba mikataba hii itakamilika, tutaisimamia vizuri kabisa na itakuwa ni ya tija kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vitongoji tayari zawadi nyingine ya Mama imeshasemwa, tuko katika taratibu za kutafuta shilingi trilioni 6.5 kwa ajili ya kuhakikisha vitongoji vile vyote zaidi ya 30,000 vinapelekewa umeme kwa pamoja katika muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda niende kwenye eneo lingine la mwisho la *TANESCO;* kila Mbunge aliyesimama amezungumzia kukatika kwa umeme. Wanasema mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni. Katika eneo hili hali siyo mbaya kama ilivyokuwa siku chache zilizopita, tulisimama Bungeni, tukakiri tatizo na upungufu lakini tukawaambieni njia za kuchukua na mimi nilikuwa mmojawapo niliyeahidi kwamba *TANESCO* hatuajiri mtu kwa ajili ya kukatakata umeme na kweli inaonekana wazi kwamba umeme haukatwi bila sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini umeme unakatika? Iko miundombinu ambayo ni chakavu inatuletea shida; kuna mambo ya asili yanatokea, radi, mvua, tingatinga na mambo kama hayo; kuna miundombinu kuzidiwa na umeme, transfoma tuliifunga, tulikuwa tuna watu 25 watu wameongezeka wamekuwa 50/70 hatujaibadilisha, tunakuwa na tatizo. Tumefanya nini katika eneo hili? Mheshimiwa Rais ametupa zawadi nyingine ya shilingi bilioni 500 ambayo itakuja kumaliza changamoto zote hizi katika maeneo yetu, zitapelekwa

kujenga vituo vya kupoza umeme, zitapelekwa kujenga njia za kupeleka umeme, zitapelekwa kubadilisha transfoma na kuwekwa kubwa, zitapelekwa kutengeneza miundombinu mipya, tunakoelekea habari ya kukatikakatika kwa umeme itakuwa ni historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachomshukuru Mwenyezi Mungu wakati mabadiliko haya mazuri yanakuja na zawadi za Mama zinakuja, niko hapa tayari kutumika kuendelea kuhakikisha kwamba watanzania wanapata kile walichokistahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda ninaomba niishie hapo, nashukuru sana ushirikiano ambao Waheshimiwa Wabunge wanatupatia na mimi binafsi niwaahidi nitaendelea kutumika na baada ya Bunge hili mtatuona sana majimboni tukiwa tunahakikisha tunafuatilia yale tuliyoyaahidi na kuyafanyia kazi kwa niaba ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, ahsante sana Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Stephen Byabato kwa mchango wako.

Sasa namuita mtoa hoja ambaye ni Waziri wa Nishati, Mheshimiwa January Makamba kwa ajili ya kuhitimisha hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini labda makofi haya ni kwa sababu ya kuwezesha mapumziko ya nusu saa asubuhi. Lakini naomba nianze na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuomba radhi na ni uungwana kwa Mheshimiwa Spika, kwa Bunge na Wabunge wote kwamba asubuhi kutokana na wingi na uzito wa hoja zilizotoka jana, asubuhi tuliamkia kwenye kuandaa majibu tukiamini kuna uwezekano tukamaliza mchana na kosa tulilofanya tulichojifunza ni kutabiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutabiri kwamba maswali huwa yanaisha saa nne na dakika 10 au 15 na utabiri huo umetokana na uzoefu wetu tu wa hapa kwamba dakika tano mpaka pale nimeshaingia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kumbe leo yameisha kabla ya saa nne, kwa hiyo, tunaingia tunapishana na msafara hapa wote na Naibu Waziri, tukatamani kuingia chini ya viti, lakini tunashukuru kwa uelewa wa Bunge na Waheshimiwa Wabunge tumejifunza. Kila jambo lina elimu, kuanzia leo hatutatabiri tena maswali yanachukua muda gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa shukrani, shukrani nyingi sana kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kweli tumepata michango mingi na mizuri na yenye tija sana, sana, sana na imetusaidia sana na wataalam wetu kwa kweli wa Wizara nzima mmefanya wachemshe mbongo zao sana katika kutafuta majibu. Kwa hiyo, *quality,* ubora wa michango ya Waheshimiwa Wabunge kwenye Wizara yetu ulikuwa kiwango cha juu sana, sana, sana. Kwa hiyo, sisi tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pia kwa pongezi nyingi ambazo mmezitoa na kwa kweli hatukuzitegemea kwa sababu kuna mambo mengi yalikuwa yanapitapita

kuhusu bajeti ya Wizara yetu, lakini sisi tulikaa kimya, tukawa tunafanya kazi, kila akija Mbunge tunampa msaada, tunajaribu ku-*engage,* tunajaribu kutoa taarifa na naamini kwamba kutokana na hayo kazi mmeiona na pongezi tunazipokea na pongezi ni deni. Kwa hiyo, tutaendelea kuhakikisha kwamba yale ambayo tumeyaahidi, tutayafanya na sisi tunaahidi ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa mchango wake ambao umesaidia kueleza baadhi ya mambo. Sasa michango ni mingi, ni zaidi ya 50 na ningependa kuwataja Waheshimiwa Wabunge wote na nataka kuahidi kwamba kwa yale ambayo sitayafikia tutawajibu kwa maandishi kabla ya Bunge hili la Bajeti kuahirishwa ili kila mmoja apate majibu ya yale ambayo tumeyaeleza. Nitajaribu kujibu kwa ujumla na nitarajibu kupitia michango ambayo imetolewa kwa Mbunge mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa masuala ya jumla ambayo nadhani ni muhimu nikayazungumza la kwanza ni hili la *TPDC* kushiriki kwenye biashara ya mafuta. Kwa sababu nadhani hili ni kubwa na la kisera na lazima tulitolee kauli na msimamo.

Kwanza ili uamue kwamba taasisi gani inafanya shughuli gani, lazima urudi nyuma uangalie imeundwa kwa mamlaka gani, kwa *instrument* gani na imepewa kazi gani ilipokuwa inaundwa yenyewe kwa sheria yake na sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukienda kwenye sheria kubwa kabisa tuliitunga hapa ya *Petroleum Act* ya

mwaka 2015. Sheria ile ina i-*define TPDC* kwamba ni *National Oil Company,* ni Kampuni ya Mafuta ya Taifa na imepewa kazi gani mle? Imepewa kazi nyingi, lakini moja ya kazi mle ni kwamba itashiriki katika mnyororo mzima wa biashara ya mafuta na gesi. Tunaposema mnyororo mzima, maana yake kuanzia utafiti, utafutaji, uendelezaji na uuzaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu tukayajua pia matakwa ya sheria kuhusu hili jambo, acha tu mambo mengine ya kibiashara lakini matakwa ya sheria kuhusu hii taasisi yetu. Lakini sisi imani yetu ni kwamba kushiriki kwenye mkondo wa juu kwa maana kutafuta na kuchimba siyo *mutually exclusive* na kuuza huku chini, unaweza kufanya vyote na vyote vikawa sahihi. Sisi tunayo mifano ya *National Oil Companies* za nchi nyingi na baadhi ya hizi tuna ushirikiano nazo. Mimi nilipata bahati ya kusafiri na Mkurugenzi wa *TPDC* kwenda kumtambulisha na kutambulishana kwenye *National Oil Companies* za nchi rafiki na nyingine tumeingia nazo makubaliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulienda *Abu Dhabi National Oil Company* kubwa sana, hii kampuni ina visima vya kuchimba, lakini wana-*training* wanauza rejareja na sisi kampuni tunayoshirikiana nayo ukisikia *TPDC* imeshinda *tender,* imenunua mafuta haya yaliyochakatwa kutoka *Abu Dhabi National Oil Company* ambayo ina mafuta, ina visima lakini pia inauza. Kuna kampuni inaitwa *Sonatrach National Oil Company* ya Algeria kubwa, ina visima, ina ma-*refinery* lakini inauza mafuta pia rejareja. Kuna nyingine inaitwa Sonangol ya Angola. Vilevile naweza nikataja kuna Aramco ya Saudi Arabia kama alivyosema ndugu yangu Mheshimiwa King.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa lazima tuliweke sawa, sisi kama Serikali tutaendelea kuiunga mkono *TPDC* na kuiwezesha ifanye kazi zake katika mnyororo mzima wa biashara ya mafuta na gesi. Lakini pia tukumbuke hili jambo ni kubwa la kimkakati, huwezi kuliacha. Sisi tulienda vitani, mzee wangu Kepteni George Mkuchika anafahamu, tulienda sisi na majeshi ya Idd Amin. Nchi zote na wauzaji wote wa mafuta walikataa ku-*supply* mafuta, nani alipeleka mafuta mstari wa mbele? Ni *TPDC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale kwenye ofisi zetu kuna nishani imesainiwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Nishani wamepewa *TPDC* kutunukiwa na Mwalimu kwa kuhudumia nchi katika kipindi cha vita. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kuna baadhi ya mambo hauwezi ukayaacha, ukaweka mkono wa Serikali na moja wapo ni mafuta. Hata hizo nchi tunazoziita za mabepari na nini kwenye haya mambo yaziondoi mkono zipo kwa sababu ni suala la usalama wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hapa katikati kidogo tulilegea legea lakini tumerudi kwa nguvu kabisa kuiwezesha *TPDC* liwe shirika kubwa la mafuta ya Taifa na la kimkakati na liweze kufanya hii shughuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na pale kwenye *TPDC* kuna idara mbalimbali, kuna idara ya *exploration* wao wataendelea nao. Lakini kuna *directorate*/ Kurugenzi ya *Oil and Gas Business* ndiyo wanafanya hii shughuli. Kwa hiyo, idara hii wanaendelea, idara ile wanaendelea na shughuli nyingine wala haina mgogoro. Kwa hiyo,

nisingependa hili likawa ni jambo ambalo likaaminika hapa na sisi tukalichukua. Kwa hiyo, hilo nilitaka niliseme kama jambo kubwa la kisera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni hili suala la kukatikakatika kwa umeme, amelizungumza Naibu Waziri na nataka niseme kwamba ipo miradi kuna *package,* labda niseme wote mnafahamu, sisi tulivyopewa nafasi hii na hapa Bungeni ikajitokeza hoja ikiwemo tuunde tume ya kusema kwa nini Waziri Makamba ameingia na umeme unakatikakatika sana. Ikawa ni kama jambo msukumiwa la mtu. Lakini sisi tukafanya utafiti na timu pale *TANESCO,* maana yake kulikuwa na maneno hujuma, hujuma, Hapana, siyo hujuma, mimi nilikuwa siamini kabisa kama watumishi wa Serikali na wa *TANESCO* wanaweza wakaihujumu nchi yao, kabisa hilo halipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tukagundua kwamba kuna baadhi ya maeneo na Wabunge ni mashahidi mmesema kuna baadhi ya *line* ni ndefu sana na zimewekwa kipindi kirefu kabla matumizi hayajapanuka na ni dhahiri kabisa hayatoshelezi. Kwa hiyo, tukafanya utafiti kila eneo ni karibu nchi nzima kuna vituo vidogo, kuna nyaya ndogo, nyembamba, kuna nyaya zingine zina-*serve* watu wengi, kuna transfoma nyingine zinahudumia wateja wengi zaidi kuliko uwezo na tukatengeneza *package* ya miradi inaitwa *National Grid Stabilization Project* ambayo ukiiweka thamani yake ni shilingi trilioni nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa safari hii tumebarikiwa, tumepewa shilingi bilioni 500. Nafahamu nimesikia suala la Mheshimiwa Kimei kwamba itaisha lini kwa sababu bilioni 500 ukilinganisha na trilioni nne na

hapa ni *under investment* tuna-*cover* vitu ambavyo havikuwekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba hatutategemea peke yake pesa hizi za bajeti kila mwaka katika kutafuta rasilimali za kurekebisha hali ya umeme. Zipo njia nyingi ambazo tunazifanya za kutafuta fedha ikiwemo hii ambayo tuliisema kwamba tukirekebisha vitabu vya *TANESCO* na Serikali ikafuta au ikachukua nusu ya deni; *TANESCO* itakuwa na uwezo wa kifedha wa kwenda kutafuta *resources* na kufanya hii miradi ambayo iko kwenye *grid stabilization* bila haja ya kuja hapa Bungeni mara kwa mara, kwa hiyo, hilo tunaendelea nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la kisera ambalo napenda kulizungumza hapa ni suala ambalo limezungumzwa kidogo kwa kirefu, ni hili suala la *strategic reserve* ya mafuta na amelizungumza Mheshimiwa Mwijage, Kamati imelizungumza, Mheshimiwa Kimei pia amelizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda niweke vizuri, hifadhi ya mafuta ya kimkakati ni nyenzo ya usalama wa Taifa vilevile. Sisi hapa sheria zetu zinahitaji kwamba kwa wakati wowote hapa nchini mtu mwenye maghala ya mafuta au kituo cha mafuta awe na mafuta ya siku 15 za mbele kwa sababu ya dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tayari katika hiyo sheria, hiyo kanuni kuna *element* za kutaka kujikinga, kuwa na hifadhi nchini *incase* kuna dharura. Sasa sisi tumeweka siku 15 kwa sababu tu ya uwezo, uwezo wa hifadhi, uwezo wa mafuta na kadhalika. Kuna nchi nyingine zinahitaji siku 90, kuna nchi nyingine mpaka miezi

sita kwamba *at any given time* nchi iwe na mafuta ndani ya nchi ya kutosheleza miezi sita, sisi tumeweka siku 15 zinatosha. Sasa ikitokea dharura ya siku ya zaidi ya siku 15 maana yake ni kwamba hamna mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tumeamua safari hii tufanye mambo ambayo yatatupeleka zaidi ya siku 15. Sasa mambo yenyewe ni yapi? Hifadhi ya kimkakati ya mafuta ya Taifa siyo lazima iwe ni *physical* kwamba mmechimba mashimo au matenki kuna mafuta pale yanasubiri tu dharura. Ukifanya hiyo, hiyo ni *dead capital* na mafuta pia yenyewe yanapungua ubora kadri yanavyokaa. Kwa hiyo, tunaposema hifadhi ya kimkakati ya mafuta hatuna maana tununue mafuta tuyaweke kwenye matenki, tusubiri dharura, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *instruments* nyingi za kuwa na *petroleum strategic reserve* na mojawapo ni aliyosema Mzee Kimei. Kikubwa ni kwamba *at any given time* ndani ya nchi *either* kupitia *instrument* mojawapo ni kuifanya nchi yetu iwe kituo kikubwa cha biashara ya mafuta, yaani nchi zote za ukanda huu ziwe zinanunua mafuta hapa, zinapitishia hapa, pana matenki hapa pia iwe *trading hub,* kwamba kama upo nchi nyingine unapiga simu kwamba nataka kununua mafuta chapchap basi unaambiwa Tanzania kuna tani 200,000 unaweza kuzipata haraka haraka na zile zinarudishwa haraka haraka. Hiyo ndiyo *strategic reserve* kwamba unayo *at any given time,* siyo ipo imelala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa tunachosema ni kwamba tutatumia na tutaleta hapa Bungeni, tutatumia baadhi ya hizi *instruments* za kisasa na za kibiashara za kuwa na mafuta mengi ya kutosha hapa nchini ikiwemo kuibadilisha Tanzania iwe kituo kikubwa

cha mafuta katika ukanda huu. Kwa hiyo, hili ni jambo la kisera nataka niliweke, kwa sababu ukisema pesa, ukiwa na *cash* kwamba mimi nimeweka pembeni *cash* nikipata dharura niwe na uwezo wa kuagiza mafuta, saa nyingine unaweza kuwa na pesa za kutosha tu lakini *physical* huwezi kuyaleta mafuta hapa nchini. Kwa hiyo, lazima uwe na namna ambayo mafuta yanakuwa *traded* hapa hapa nchini. Kwa hiyo, hiyo tutaendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine la kisera ni suala la umeme kwa ujumla. Malengo yetu ya kufikia megawati 5,000, tunafikaje, mahitaji ya nchi tunayajuaje, tunayapangaje, umeme wa aina gani, tunaufikishaje kwa watumiaji. Sasa moja ya vielelezo vya maendeleo ya nchi ni moja ni alilosema Profesa Muhongo *per capital consumption* ya *energy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyingine ni aina ya nishati watu wanayotumia, nyingine ni idadi ya watu wanaofikiwa na nishati hiyo na mwisho ni nishati hiyo inatumika wapi. Hiyo ndiyo *energy profile*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia nchi yetu aina ya nishati inayoongoza kwa matumizi siyo mafuta, siyo umeme, siyo gesi ni nishati inaitwa *biomass*. Kuni, mkaa, pumba, mavi ya ng'ombe na kadhalika. Asilimia zaidi ya watu 80 ya Watanzania ukichukua *unit* ya *energy,* magari yote yanayosafiri, mitambo yote inayozalisha umeme bado kiwango cha nishati kinachotumika ni kidogo kuliko kuni, mkaa, pumba. Sasa hiyo peke yake *proportion* ya *biomass consumption* inaelekeza kiwango cha maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maendeleo yanapatikana mnapoondoka kwenye *biomass* na kuingia kwenye *commercial traded modern cleaner energy,* kwa sababu *biomass* moja ya sifa yake kwa mwaka hapa watu 22,000 wanakufa kwa kuvuta moshi wa kuni na mkaa watu 22,000, hizo ni *statistic* za Wizara ya Afya. Kwa hiyo, kwa kadri unavyoenda kwenye nishati safi ndivyo ambavyo unaokoa watu wako na unaingia kwenye uchumi wa kisasa. Sasa hiyo ya kwanza aina ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili je, nishati ya hapa Tanzania inatumika zaidi wapi kwenye usafirishaji, kwenye viwanda, majumbani? Ukitizama *profile* ya nishati hapa nchini haitumiki viwandani, inatumika majumbani na majumbani inatumika wapi. Je, kupoza vichwaji? Je, kupoza hewa? inatumika kupika. Kwa hiyo, utaona kwamba kwa nchi yetu kama wewe ni Waziri wa Nishati haujajielekeza kwenye nishati ya kupikia haujafanya kazi yako, kwa sababu ndipo ambapo *consumption* kumbwa ya *energy* ilipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka kwenda kwenye maendeleo ya viwanda, tunahitaji umeme zaidi, nami nakubaliana kabisa kwamba *per capital energy consumption* yaani kiwango cha nishati kinachosomeka kwa mtu lazima kipande, lakini hiyo ni *function* ya unazalisha kiasi gani; Pili je, una uwezo wa kuusafirisha huo umeme kwa hao watumiaji; Tatu je, wana-*appliances* za kutosha za kutumia umeme mwingi; na mwisho je, una viwanda vya kutosha kutumia umeme wa kutosha? Lakini ni yai na kuku kipi kimeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutazalisha umeme mwingi tumeongea na wenzetu wa *TANESCO,*

tunataka sisi kama tutapata dhambi, dhambi yetu iwe kuwa na umeme mwingi kuliko unaohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuweze kuusambaza na kuupeleka kila mahala katika nchi hii, ndiyo maana utaona bajeti yetu hii ya safari hii ambayo sio mwisho ni mwanzo wa safari inatupeleka kwenye kuzalisha umeme mwingi lakini mtaona miradi mingi ya usafirishaji na mradi wa usambazaji ni hii ya vijijini. Kwa hiyo jambo la kisera sisi la kwetu ni siku zote kuendelea kuzalisha umeme mwingi wa kuwafikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri tuliyonayo sisi katika ukanda huu tuna *natural resource base* ya kuzalisha umeme kuliko nchi nyingi katika uwanda huu ukiondoa Congo. Tunayo makaa ya mawe, gesi, jua, upepo na tunayo maporomoko ya maji. Kwa hiyo, ukilinganisha sisi leo tulikuwa tunapiga hesabu uki-*exhaust resource base* yote tuliyokuwa nayo sasa hivi tuna uwezo hata wa kufika hata megawatt 60,000 hatuzihitaji sasa lakini ndiyo safari hiyo tunayoelekea. Sasa nilitaka kusema kisera huo ndiyo mwendo na mwendo wa haraka na hatutasita kukimbia kwenye kupata umeme mwingi kiasi kikubwa, sasa hili nilitaka nisema jingine la kisera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *Symbion* ambalo alilizungumza Halima Mdee na suala la Mwalimu Nyerere na suala la *TANESCO* kwa ujumla. Sasa nianze na suala la *Symbion* sasa hili ni muhimu niliseme hapa Bungeni ili kuliweka vizuri kwa sababu limekuwa linasemwasemwa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri una dakika Kumi.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nahitaji zaidi lakini nashukuru. Suala la *Symbion* limekuwa linasemwa sana, nataka kulisema kama ifuatavyo na hili litaendana na Mwalimu Nyerere ambalo nitalieleza. Suala la Symbion tunaweza tukarudi sana lakini nianzie 2011 ambapo *TANESCO* iliingia kwenye mkataba wa muda na kampuni hii *Symbion* ambayo ilikuwa na mitambo pale, ilikuwa mitambo ipo pale imekaa huko nyuma kulikuwa na mambo mengine kulikuwa na shida ya umeme wakaingia mkataba wa muda wa miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba ukaisha 2013 wakaingia mwingine wa muda mpaka Septemba 2014, *EWURA* wakaandikia barua *TANESCO* kwamba hii mikataba ya muda mfupi mfupi ina gharama, *TANESCO* wakachukua ushauri wa *EWURA* wakaingia mkataba wa muda mrefu kati ya *TANESCO, Symbion* na muda mredu kati ya *TANESCO* na *symbion* Julai 2015. Septemba mwaka huohuo *EWURA* ikapitisha huo mkataba na mwezi Disemba Mwanasheria Mkuu naye akaupitisha, Tarehe 10 Disemba, 2015 Mkataba ukasainiwa lakini siku hiyohiyo ukaitishwa na baada ya hapo Tarehe 24 mwezi Mei mwaka 2016 mkataba ule ukavunjwa rasmi Machi 27, *Symbion* akaenda kwenye Mahakama ya Kimataifa ICC kudai fidia ya dola za Kimarekani Milioni 566 kwa kuvunjwa mkataba isivyo kufuata utaratibu na hasara ambayo itapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye *shareholders* wa *Symbion* wakaenda kudai Dola Bilioni Moja kutokana na kuvunjwa kwa *industrial protection treat,* tukawa tunadaiwa Dola Bilioni Moja na Nusu kutokana kwenye huo mkataba, mashauriano yakafanyika baadaye ikakubalika kwamba tuzungumze nje ya *court* na

mazungumzo hayo yalikubalika Julai 28 na Februari 2021 makubaliano yakafikiwa, yalikuwa na sehemu tatu, Serikali *TANESCO* kulipa zile bilioni 300 na aliyosema Mheshimiwa Mdee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ilikuwa baada ya Serikali kulipa *TANESCO* kuchukua ule mtambo wa *megawatt 112* kwa sababu ile ndiyo kisehemu kinaachwa, kukawa na ratiba ya kulipa hayo malipo la sivyo inarudi kwenye Mahakama. Sasa mwezi Agosti malipo yakafanyika kulingana *Deed of Settlement* ambayo Serikali ilisaini ili kuokoa adhabu kubwa ambayo tulikuwa tunaelekea kushindwa na mwezi Oktoba *TANESCO* ikauchukua mtambo, sasa kuanzia mwezi Novemba mtambo ukaanza kuzalisha umeme na tangu umeanza kuzalisha umeme mwezi Novemba mpaka sasa umezalisha *unit* hapa ziko nyingi ninazoweza kuzitaja, *TANESCO* imezalisha umeme na kuuza kwa faida, kwa hiyo ukipiga hesabu thamani ya mtambo wa *megawatt 112* na mauzo ya umeme yanayopatikana katika mtambo ule basi unaweza kujua kama hayo makubaliano yalikuwa na tija, lakini sisi tunaamini kwamba Serikali kupitia Wanasheria na waliamini kabisa kwamba ni jambo ambalo lilipaswa kuiepushia Serikali hasara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huo ndiyo ukweli kama unaweza kuutafsiri unavyotaka lakini mwisho wake maamuzi yalichukuliwa na Wanasheria wa nchi yetu walioangalia maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa Bwawa la Julius Nyerere, sisi tuna mkataba mradi ule unaendeshwa kwa mkataba, mkataba unatoa haki na wajibu kwa kila upande, mkataba umeweka utaratibu wa kushughulikia

kutofautiana, mkataba unatoa adhabu na *sanctions* mbalimbali, muda wa mkataba haujaisha, nasi tusingependa ku-*litigate contractual matters* kati ya *two parties* kwenye *contract* ambayo *its operational* hapa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mkataba huo unaendelea zitakapofika ratiba ambazo zimepangwa basi zitafika. Je, mradi utachelewa ndiyo mradi utachelewa kwa miaka miwili. Je, *implication* ya kuchelewa ipoje ipo ndani ya mkataba. Sisi kwetu mkataba uishe ukiwa bora na usalama mradi na sisi hatuoni kuchelewa kwa mradi wa Julius Nyerere kama ni *disasters,* mradi hapa wa Kidatu umejengwa miaka mitano, Kihansi miaka minne, Mtera miaka minne, Pangani miaka mitano, duniani kote miradi hii inapita ratiba, sisi *focus* yetu uishe kwa ubora na viwango na malengo yake yatimie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasa naomba nitumie muda mchache uliobaki harakaharaka kumaliza na ndugu zangu wa Kigoma. *Grid* naomba Mzee Bidyanguze, Mama yangu Samizi, Kaka yangu hapa Kirumbe na wananchi wa Kigoma na Wazee wangu wa kule Buhigwe wote mnafahamu mimi ni wa Kigoma lakini siyo sababu ya kuweka *grid.* Kwa hiyo nafahamu ipo miradi minne ya kupeleka *grid* Kigoma. Katika miradi hiyo minne, miradi miwili Wakandarasi wapo *site,* mmoja anaitwa TATA anapeleka wa *Kv* 400 kutoka Nyakanazi mpaka Kigoma tumemlipa yupo *site. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkandarasi wa pili yupo *site* anaitwa *Sinotech* anautoa Nyakanazi - Kakonko mpaka Kibondo tunayo *line,* kwa hiyo Kibondo – Kasulu - Buhigwe - Kigoma hii inaisha Oktoba, hii siyo *story* wako

*site*. Kwa hiyo tunaposema *grid* inakuja Kigoma kabla ya Oktoba tunamaanisha hivyo. Waheshimiwa Wabunge nimalize kwa kusema Mzee wangu Salum nimekusikia mchango wako tumeuchukua, Mheshimiwa Mwakasaka vijiji vyako tumevichukuwa, Mheshimiwa Zedi, Mheshimiwa Jesca Kishoa tutakujibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shanif Mansoor, Mzee Usi Salum Pondeza, Mheshimiwa Lucy kutoka Simiyu tumetenga Milioni 725 kwenye mradi ule wa kupeleka umeme Bariadi, kwa sababu ndiyo kazi za kuanzia ikiwemo kulipa fidia, tukishalipa fidia na kumaliza ile *EIA* pesa Bilioni 65 zipo za kupeleka umeme wa *grid* Bariadi. Mheshimiwa Vuma nimeshajibu kuhusu *grid* na kukatika kwa umeme tumejibu, Mheshimiwa Makoa ndugu yangu vijiji vyako Kondoa Mjini na hapa siyo mbali, Mheshimiwa Monni nitakuja Chemba siyo mbali na Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava suala la mafuta tutakujibu kwa maandishi na umeme kukatikakatika tumejibu. Mheshimiwa Gulamali Bwawa la Mwalimu Nyerere hongera tumezipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la hii Tume tuliyoiunda ya kwenda kuchunguza, labda niseme tu kwamba samahani tulipata shida moja, kwamba kama *TANESCO* na kama Wizara, tunaposema kwamba bei ya kuunganisha itokane na nguvu ya kiuchumi ya wahusika ambayo *assumption* ilikuwa ni aina ya *settlement* wanazokaa, kwamba watu wa mjini wana nguvu za kiuchumi wanaweza kulipa zaidi, watu wa vijiji tuwasaidie walipe chini. Sasa *problem* tuliyoipata ni hiyo katika miji kuna watu pembezoni mwa miji ambao pamoja na kwamba jiografia imewaweka ndani ya mji lakini hali yao inafanana na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na *option mbili, either* kutengeneza *a general rule* ambayo itakuwa *applicable* kwa maeneo ya aina hiyo, jambo ambalo ni gumu, pili ni sisi kwenda *physically* wenyewe kuuchukua mtaa kwa mtaa inayofanana kama kijiji. Nadhani kwa hoja kama itachukuwa muda nadhani ni njia salama zaidi itakayo-*target* wahusika moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tunaomba mkubali hii na kama tulivyosema kwenye hotuba yetu tutawashirikisha katika hii, watu wetu mtawaona watakuja huko na tutafanya kazi.

Meshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Vita suala la kupeleka umeme kwenye hizi sehemu za huduma tumelipokea, kwenye bajeti tunao mradi wa kupeleka umeme katika mashule vituo vya maji na zahanati. Mheshimiwa Festo nimekuelewa sana vizuri sana kuhusu mchango wako ambao umetokana na *experience* yako ya kutembelea kiwanda cha kule ulipoenda, kuhusu Lumakali na Luhuji naomba niseme kwamba tumepata watu ambao wana-*interest* ya kuwekeza. Zile hela ulizoziona Bilioni Nane ni za kazi za awali kuhuisha ile *feasibility study* lakini tunakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *GGM* ambalo limezungumza na Mheshimiwa Musukuma nadhani na wewe na mwingine, pale kuna *confusion*, tumeingia nao mktaba nao mwezi Novemba tuwapelekee umeme, sasa ile *substation* inayoonekana pale Geita Mjini siyo yenyewe ya kupokelea umeme wa *GGM*. Tulikubaliana sisi tutaupeleka mpaka getini wao watajenga *substation* ndani, kwa hiyo kuna *substation* inayojengwa ndani ya mgodi ambayo inaisha mwezi Oktaba kwa mujibu wa makubaliano yetu, kwa hiyo bado tutapeleka umeme

*GGM* na ile sheria uliyosema ya hovyo ya kwamba ukizalisha umeme huu, lazima tutaipitia kwa hakika kabisa ili kuwezesha wawekezaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Deo Mwanyika, suala la Mapembasi tutalimaliza na la Masista pia tutalimaliza. Mheshimiwa Getere mambo mengine uliyosema umepitisha kidogo lakini tunapokea pongezi. Hiyo Tume itakuja nashukuru kwamba umeona mambo yanaenda vizuri. Mzee Magessa naomba tisheti uivai ya vitongoji kwa sababu siyo tu tumeanza lakini dhamira ya kupeleka umeme kwenye vitongoji ipo kwenye bajeti yetu tunazo Shilingi Bilioni 140 za maandalizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, migodini mtaleta lini? Mkitazama kwenye bajeti yetu ya sasa tumetenga Shilingi Bilioni 20 kupeleka umeme migodini, viwandani na kwenye maeneo ya uzalishaji wa kilimo, haijawahi kutokea na tutaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee wangu rafiki yangu Kamonga Ludewa tumekupata tumekusika, Mheshimiwa Mohamed Saidi Issa ile sheria *geothermal* tutaifanyia mabadiliko, Mheshimiwa Ighondo Abeid tutakuja pamoja kama ulivyosema katika vijiji Tisa kuwasha pale Singida, Mheshimiwa Shabiby suala la bili la *KVA* naomba sana kwa ridhaa yako tuchukue haya makaratasi yako tuende pamoja *TANESCO* tukalitazame kama ni suala la mahsusu kama suala la jumla tutalifanyia kazi lakini suala la mafuta hizo taarifa ulizonazo za kuhusu bei zinavyopigwa tuko tayari kuzipokea, tuko tayari kuzifanyia kazi, wewe tuletee kwa pamoja ukitaka unaweza kuja na mtu mwingine ambae atakuwa shahidi wako namna

tunavyolishughulikia hilo jambo kama huna imani na uwezo wetu wa kushughulikia hilo jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nusrat kuhusu Singida kuna miradi mitatu, katika hiyo uko mradi wa Manyoni, mradi wa Singida pale *DC* na Ikungi yote hiyo ipo katika uelekeo wa kutekelezwa. Manyoni tayari wako Masdar kampuni ya *UAE* kubwa kabisa ya *renewable* huu mwingine ipo kampuni ya upepo ambayo imepata zabuni na iko kwenye majadiliano na kampuni, lakini sasa muhimu kujua ni umeme unapozalishwa pale Singida siyo kwamba ni wa Singida ni kwa sababu tu Singida ipo kwenye *grid* utaenda pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la hospitali hazijaunganishwa ukitazama kwenye bajeti yetu utaona kwamba katika mwaka huu tuna hospitali zaidi na vituo vya afya zahanati zaidi ya 114 ambazo tumezipelekea umeme mahsusi na hapa ndipo tunapoanza, tunaongea na wenzetu katika TAMISEMI na kwingineko kwamba tunapopanga hii miradi tupange pia na *component* ya umeme, kwa sababu saa nyingine tunasahau unaweka kule halafu kumbe umeme hakuna kwa hiyo *REA* leteni, kwa hiyo kwenye *cost* ya miradi tuta-*coordinate* na wenzetu ili *cost* ya mradi wote iwe pia na gharama ya kupeleka umeme pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mhagama nimekupata, Mzee George Malima, *REA* ipo *center* ni kweli, Mpwawa na bei ya kuunganisha nimezungumza, Mheshimiwa George Mwenisongole suala la wakandarasi amelizungumza Naibu Waziri, suala la Mkuu wa Mkoa nadhani mimi na wewe tutalizungumza pamoja na Waziri wa TAMISEMI kuliweka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dada yangu Mariam Mtanda megawati 300 za Mtwara ambayo pia amezizungumza Mheshimiwa Mwambe megawati 300 za Mtwara pesa imepatikana na siyo tu ya megawati 300 lakini pia na waya wa kuleta mpaka Somangafungu, Wajapan watatuchangia.

Mheshimiwa Francis Isack, Mkalama nimechukua, tutakujibu kwa maandishi; ndugu yangu Mheshimiwa Hassan Kungu kutoka Tunduru naelewa kabisa ile KV 33 kutoka Songea ni ndefu bila shaka na katika ule Mradi wa *Grid Stabilization* ipo ya ku-*upgrade* ule waya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjomba wangu Mheshimiwa Rweikiza kazi bado sana; ni kweli na umeme unazimika sana tumelizungumza, Mheshimiwa Florence Samizi, gridi nimezungumza, Malagarasi pia tunaanza; Mheshimiwa Bidyanguze pesa ipo tumamazila *evaluation,* ndani ya mwezi tuna-*award* Mkandarasi aanze ujenzi pale.

Kuhusu madeni makubwa *TANESCO* labda niweke tu vizuri *status* ya *TANESCO*, *TANESCO assets value* yake ni trilioni 17, madeni yake ni trilioni tatu, katika hayo madeni trilioni mbili ni madeni ya Serikali ya *on landing* na trilioni moja ni watoaji huduma ikiwemo *TPDC*, *PAET* na kadhalika. Kwa hiyo, ni vizuri hizi takwimu za *financial position* ya *TANESCO* zikajulikana kwa sababu saa nyingine tunachanganya, ukisema *TANESCO* ina deni la trilioni 13 si kweli ni ina *asset* ya trilioni 13.

Mheshimiwa Anastazia Wambura la megawati 300 nimelizungumzia, Mzee Mulugo, lile suala la *helium* tumelizungumza ofisini, ni la ndani ya Serikali tutaliweka vizuri; Mzee Felix wa Buhigwe nimejibu na mengine

tutajibu; Mheshimiwa Issa Mchungahela, umelihutubia Taifa, hotuba yako imepokelewa basi tutayafanyia kazi ambayo umeyasema. *(Makofi)*

Mzee Almas nimeelewa sana kuhusu Msamvu na ni *critical* na kuungua mara mbili ndani ya miezi sita ni jambo ambalo inabidi lituinue, na mambo mengine hatuyasemi hapa, lakini kuna hatua tumechukua za kiusalama za kuuchunguza lakini pia na kuimarisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafutaji wa mafuta tumeongea kwenye bajeti tutaenda nao; Mheshimiwa Godwin Kunambi na Mheshiwa Vedasto tulizungumza kuhusu watu wanataka kuunganisha umeme, je, kwa nini tusiwakopeshe halafu wakalipa kidogo kidogo kwenye bili zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tumelitafakari na tunaendelea kulitafakari, tumepokea *proposal* mbalimbali na wachambuzi wa fedha wanafanya, *challenge* iliyopo ni kwamba vifaa vya kuunganisha vile vinaweza vikafika labda shilingi 200,000 au shilingi 300,000 lakini kasi ya kununua umeme ikawa ni shilingi 2,000 kwa mwezi au mtu ananunua LUKU anakaa nayo miezi sita, mnalazimika kutafutana, kutaka kung'oa, kukatiana umeme, mtu akiongeza tu umeme wake umeukata, kwa hiyo inaweza ikaleta ugomvi.

Kwa hiyo *the debt collection component* ya hii programu ni lazima tuiweke vizuri ili tusigombane na watu wetu kwa sababu kama mtu yuko nyuma ya deni akiweka LUKU tu maana yake imeliwa, sasa tutakuwa tunagombana na wateja. Lakini ni jambo ambalo tunalitafakari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa mafuta Mheshimiwa Mohamed Monni nimeshazungumza; Mheshimiwa Mama Stella Manyanya ile *evacuation* ya umeme kutoka Julius Nyerere nielezee kidogo tu, Julius Nyerere siyo mradi mmoja, siyo bwawa; kuna bwawa, kuna usafirishaji yote inaenda kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwambe kuhusu *LNG,* tutafanya na tunafanya na tumeanza bila shaka yoyote Bandari ya Mtwara na miundombinu ya Mtwara itatumika katika utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mariam kuhusu teknolojia ya *live wire* na usalama kwenye *LNG* tumepokea; Mheshimiwa Kingu ahsante sana kwa shukrani, kuhusu *tender* iliyofutwa, *tender* hii safari hii ilisimamiwa na *GPSA, GPSA* iko chini ya mamlaka mengine na sisi tutakachofanya ni kufuatilia nini kilitokea, ila jambo ambalo ni la kweli kabisa ni kwamba *fuel marking* bado ni shida, haifanyiki kwa mtu yoyote wa mafuta atakwambia *fuel marking* haifanyiki kwa viwango vinavyohitajika na bado ni mtihani *capacity* ya *TBS* bado iko chini, tunaongea na wenzetu kuweza kuiinua. Kwa hiyo la *tender* tutalifuatilia halafu tutatoa taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee Bidyanguze, nimezungumzia la Malagarasi nashukuru na umeme utapatikana lini kwenye vitongoji tutaeleza kwenye siku zijazo; Mzee Kimei tumezungumza kuhusu *densification* inaendelea na kutafuta *sources* zingine kwa sababu umeme vijijini ndiyo *densification* yenyewe; ndugu yangu wa Mbinga kweli basi kwa kuchelewa basi tutafika na mimi ahadi yangu iko palepale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mwisho kabisa najua huwezi kuzungumza hapo ulipo ila Mfindi Kusini hatujaisahau kupeleka umeme katika sahanati, shule na sehemu za huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mengi na niseme tu kwamba nishukuru tena kwa michango kwa kweli mmetutia moyo sana, mmetupa nguvu na haya ambayo tumeyaweka kwenye kitabu chetu ni safari ni mwanzo wa safari siyo yote yataisha mwaka ujao wa fedha, tumeyaweka pale mengine ni endelevu kama mnavyojua yanaonekana ni masuala ya kuendelea. Lakini naomba niwashukuru sana kwa ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. *(Makofi)*

Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa January Makamba. Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**MWENYEKITI:** Kamati ya Matumizi. *(Makofi)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

*Hapa (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Haya Ahsanteni sana. *(Makofi/Kicheko)*

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na kitabu cha pili Matumizi ya Kawaida ukurasa wa 395, Fungu 58 - Wizara ya Nishati.

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 58 – Wizara ya Nishati**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*......................Sh. 3,518,284,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina mshahara wa Mheshimiwa Waziri na kanuni zetu zinaruhusu Mbunge anayetaka ufafanuzi wa jambo mahsusi la kisera anaweza kuomba ufafanuzi kwenye ngazi hii, na hapa nina jina moja la Mheshimiwa Halima James Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina hoja ya kisera japo nimesikitishwa kidogo na Waziri, shilingi bilioni 355 bila kufanya kazi hapa anaona poa. Nina jambo moja kuhusiana na suala la Julius Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Waziri yanaeleza kwamba hawezi kuyatolea majibu kwa kina hiyo *remedy* ambayo nchi tutaipata kwa sababu muda

wa mkataba haujafika kwa mantiki ya kwamba tarehe 14 mwezi wa Sita bado, ndiyo majibu aliyonijibu.

Sasa nchi iliingia mkataba tarehe 15 Februari, 2018; tarehe 14 Juni, ndiyo tunamaliza kama nilivyosema, tarehe 31 Oktoba, 2021 tulikuwa tumefika asilimia 48.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee hebu ili tuwe tunaenda pamoja kwenye hoja yako unazungumzia nini maana umeanza mahali bilioni ngani zimefanyaje, halafu najaribu kukusikiliza kwa bidii sana na sielewi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay*, ile nilikuwa nimechomekea tu ile ya kwanza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya msingi ni suala la Mradi wa Mwalimu Julius Nyerere. Wakati natoa mchango wangu nilizungumza lugha ambayo imezungumzwa na Kamati yako pia kuhusiana na namna gani mradi huo hautekelezwi kwa kasi inayotakiwa na kuna hatihati kubwa sana itakapofika mwisho wa mradi ambayo ni siku 10 zijazo mradi utakuwa haujakamilika.

Sasa swali langu mimi lilikuwa ni dogo tu kwa sababu kama *trend* ya Mkataba ilikuwa inataka *by 31 December, 2021* mradi uwe umefika asilimia 97, sasa hivi ulitakiwa uwe umefika asilimia 100 ila tulitakiwa tuwe tunafanya majaribio. Sasa hivi tumefika asilimia 56; nikauliza tu vizuri tu kwamba jamani nchi yetu kwenye mikataba ya barabara, kwenye mikataba ya ujenzi pale ambapo upande wetu hatutekelezi wajibu wetu tunalipa mabilioni ya shilingi. *(Makofi)*

Sasa kwa kuwa mkataba huu unaonekana unaisha na utekelezaji wa kazi uko bado duni, nchi yetu inapata nini kwenye hili? *My question was very simple*, sasa nimejibiwa kwamba tarehe 14 bado, *yes*, lakini kama Desemba, 2021 ilikuwa asilimia 53, Februari, 2022 ni asilimia 56 yaani miezi mitatu imefanyika asilimia mbili kwa vyovyote vile hizo siku 10 haiwezekani tukamaliza asilimia hizo 40 zilizobaki. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nikamuuliza Waziri tu vizuri hivi *remedy* yetu kama nchi kwenye hiyo mikataba kwa sababu changamoto iliyopo mikataba nchi hii ni siri. Sasa kwa sababu ni siri ndiyo maana tunauliza kwa maslahi mapana ya nchi kuna kitu tutapata, lakini kama vilevile mkataba wetu hatupati Mheshimiwa January unaweza ukaniambia tulivyoingia mkataba hatupati kitu, si tumemaliza hapo kiroho safi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nisipopata majibu mazuri kwa sababu hizi hoja zinaonesha siku 10 zijazo mkataba ukaisha nitakamata shilingi, nisipopata majibu mazuri. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee kengele imeshagonga.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni yetu ya 120(4) inasema Mbunge atakayeamua kutumia kifungu chenye mshahara wa Waziri ataruhusiwa tu iwapo ataomba ufafanuzi wa suala mahsusi la sera na hatazungumzia zaidi ya jambo moja.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Halima Mdee, amesimama hapa ameeleza kuhusu jambo ni mahsusi la Mradi wa Bwawa la Nyerere, lakini ile sasa siyo sera, yaani ungeweza kueleza sera halafu ndiyo useme pengine ule ni mfano. Ameeleza hapa mikataba ya barabara sasa hayo ni mambo mangapi katika jambo moja. Kwa hiyo Mheshimiwa hiyo kanuni lazima iwe imefuatiliwa kikamilifu. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*..........................Sh. 871,559,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*.....Sh. 1,211,656,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*....................Sh. 487,795,000
Kifungu 1005 – *Legal Services Unit*.................Sh. 506,103,000
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*..........................................Sh. 475,726,000
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*..........................................Sh. 471,158,000
Kifungu 1008 – *Environment Management Unit*..........................................Sh. 345,769,000
Kifungu 1009 – *Management Information System Unit*.............................Sh. 524,216,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 – *Electricity and Renewable Energy*...........Sh. 55,314,972,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki mtakumbuka Mheshimiwa Waziri wakati akisoma hotuba yake alieleza kwamba katika ile bajeti yake ya shilingi

trilioni 2.7 ilikuwa imeongezeka shilingi bilioni 200. Kwa hiyo zile shilingi bilioni 200 zilizoongezeka kifungu kimojawapo ambacho kinapata mababadiliko ni hiki kifungu kidogo cha 3001.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu 3002 – *Petroleum and Gas*............Sh. 19,224,719,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kwenye Kitabu cha Nne Matumizi ya Kugharamia Miradi ya Maendeleo, Fungu 58 ukurasa wa 161 Wizara ya Nishati.

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 58 – Wizara ya Nishati**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*...................Sh. 10,500,000,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*.....Sh. 1,500,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3002 – *Petroleum and Gas*......Sh. 2,784,909,598,000

**MWENYEKITI:** Soma upya.

Kifungu 3001 – *Electricity and Renewable Energy*............................Sh. 2,784,909,598,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hiki kifungu nacho ni sehemu ya zile fedha ambazo shilingi bilioni 200 zimeongezeka. Kwa hiyo nacho kina marekebisho kama alivyosoma Katibu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu 3002 – *Petroleum and Gas*...........Sh. 26,119,978,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa Hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Taarifa kuwa Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi yake, naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na kwa utaratibu wetu sasa nitawahoji hoja ya Waziri wa Nishati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati pamoja na Naibu Waziri kwa kupitishiwa makadirio yao ya mapato na matumizi na Bunge, lakini pia kwa kuwa wasikivu kwa hoja zilizotolewa na Kamati yetu ya Bunge ya Nishati na Madini. Wameshauriwa mambo mbalimbali na wao wameyafanyia kazi na pia wamesikiliza Waheshimiwa Wabunge ushauri mlioutoa na wao wakati wakijibu hoja hapa wameonesha utayari wao wa kuchukua yale mawazo mliyoyatoa Waheshimiwa Wabunge na kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji kazi wote ambao mnafanya nao kazi kwenye kuhakikisha Wizara hii inalifanya Taifa letu lisonge mbele na sasa kwa sababu Bunge limeshapitisha haya tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa ahadi zote mlizozitoa, kwamba mnakwenda kuzifanya na vipaumbele ambavyo mmevionesha na mambo makubwa na mazito ambayo mmeonesha mnakwenda kuyafanya na sisi tunawatakia

kila la kheri kwa sababu Bunge limeshafanya kazi kwa sehemu yake. *(Makofi)*

Lakini pia nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Kamati hii ya Kudumu ya Bunge na Naibu wake na Wajumbe wa Kamati hii kwa kufanya kazi kwa niaba yetu sisi sote. Wamefanya kazi nzuri kufika sehemu hii ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi mnasimama kupongeza kwenye hotuba hii sio jambo rahisi kwa Wizara ya Nishati kupita kirahisi namna hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawapongeza sana Kamati yetu kwa kufanya kazi nzuri ambayo imetufikisha mahali hapa ambapo, nyinyi mmetoa ushauri, Wizara wamewasikiliza na sasa sote tunazungumza lugha moja. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo nitangaze rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yamepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Yalipitishwa kwa Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mambo mawili la kwanza asubuhi wakati wa kipindi cha maswali kutoka kwenu Waheshimiwa Wabunge na majibu kutoka upande wa Serikali, swali namba 316 la Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini liliulizwa na Mheshimiwa Mbunge na kujibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Baada ya kujibu majibu yale ya msingi Mheshimiwa Mwita

Waitara aliposimama kuuliza swali la nyongeza akaonesha kwamba majibu yaliyosomwa ama aliyopelekewa na Mheshimiwa Naibu Waziri sio majibu mahususi kwa swali alilouliza, moja,lakini la pili ni kwamba sio majibu sahihi kwa sababu amesema jambo ambalo yeye kwa taarifa alizonazo hayajafanyika lakini jibu lilionesha mambo hayo yamefanyika. *(Makofi)*

Ni mambo gani? Swali lile la msingi lilikuwa na majibu yaliyoonesha kwamba wodi ya wanawake imekamilika, lakini pia ilisema kwamba wodi ya wanaume imekamilika. Mheshimiwa Mwita Waitara aliposimama akasema hizo wodi mbili hazijakamilika. Sasa nilimruhusu Mheshimiwa Naibu Waziri ajibu swali alilokuwa ameulizwa, lakini hili nilimuambia asijibu ataleta ufafanuzi baadaye.

Sasa kama angekuwa ameleta ufafanuzi wakati wa kipindi cha maswali ningekuwa nimempa fursa Mheshimiwa Naibu Waziri ili atoe ufafanuzi yeye mwenyewe. Lakini nimeletewa ufafanuzi hapa, kwa hiyo nitautoa huo ufafanuzi kwa sababu hatuko tena kwenye kipindi cha maswali na majibu.

Waheshimiwa Wabunge, hapa nimeletewa taarifa ya hospitali ya Halmashauri ya Tarime ambayo imejengwa kwa kutumia fedha za *Corporate Social Responsibility (CSR)* majengo 11. Fedha za kupitia Mpango wa Maendeleo na Ustawi wa Taifa *(TCRP 54, 41*) majengo mawili; na mchanganuo nimeletewa hapa wa majengo hayo ambayo Waheshimiwa Wabunge, sina haja ya kuyasoma isipokuwa yale ambayo yalikuwa yametajwa kwenye majibu ya msingi yaliyosomwa hapa asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, taarifa inasema jengo la wodi ya wanawake imekamilika na inatumika na mimi nimeletewa picha za kuonesha wodi inatumika. Hapa pia inasema jengo la wodi ya wanaume limekamilika kwa asilimia 99; pia nimeletewa picha ambazo zinaonesha wodi hiyo imefikia asilimia 99.

Majibu kwa swali hilo la 316 kwa kadri yalivyotolewa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI yako sawasawa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waitara inawezekana ulipata taarifa hiyo kabla hayajakamilika, lakini sasa yamekamilika na hiyo wodi ya wanawake inatumika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, jambo la pili ambalo nataka kulizungumzia ni lile ambalo nafafanua hapa kila siku lakini kwa sababu Wabunge wengine tunakuwa na majukumu mengine kwa hiyo huwa hatujapata pengine kulisikia nikiwa nasema.

Waheshimiwa Wabunge, uchangiaji humu ndani Wabunge wote hadhi yetu inafanana. Wabunge wote hadhi yetu inafanana, yako maeneo tunayoyawakilisha na kama sio maeneo basi kuna kundi la watu unaloliwakilisha humu ndani. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kila mtu ana haki sawa na Mbunge mwingine kuwawakilisha wananchi wake na hivyo hivyo, kuchangia pia kila Mbunge anahaki ya kuchangia. Hakuna Mbunge ambaye yeye ana mambo mazito sana kupita Mbunge mwingine kwamba yeye ndio lazima apewe nafasi ya kuchangia. Kila Mbunge anahaki sawa ndio maana Waheshimiwa Wabunge huwa mnapewa fursa ya kuonesha vipaumbele vyenu na tunaposema vipaumbele vyenu vipaumbele vya wananchi wenu waliowachagua. Wananchi wako waliokuchagua kama

umeona wewe wale unaowawakilisha vipaumbele vyao vitano umevileta, zungumza hivyo vipaumbele vitano ukipata muda wa ziada basi ongeza hayo mengine. *(Makofi)*

Lakini usimalize muda wako wa kuchangia halafu ukataka kuonesha kana kwamba unaonewa hakuna Mbunge anayeonewa; na Spika wenu hiyo ndio kazi yangu kuhakikisha wote mnapewa haki sawa. Kwa hiyo, yako mazingira ambayo naweza kuwa nimeletewa hapa mbele ninavyosema nimeletewa hapa mbele sio lazima niwe nimekaa mimi, hata akikaa mwingine ni msaidizi wangu mimi, kwa hiyo nimeletewa hapa mbele. Ile orodha hata kama nimeletewa, lakini yuko ambaye hajachangia na hajapewa nafasi, atapewa huyo na wewe ambaye jina lako liko kwenye orodha hutaitwa, kwa nini? Kwa sababu Wabunge wote mnahaki sawa. Hakuna Mbunge zaidi ya Mbunge mwingine humu Bungeni na ni kazi yangu kulinda hizo hadhi zenu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge niondoe tu hiyo inapita pita huko kana kwamba kuna mtu ameonewa ama nani amefanya nini, hapana tunaweka usawa kila mtu apate fursa ya kuwakilisha wananchi wake. Nadhani hilo limeeleweka Waheshimiwa Wabunge na ninaamini halitarejea tena kiasi kwamba litanitaka nitoe tena ufafanuzi.

Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge lengo letu na nia yetu ni njema, Wabunge wote mmetumwa na wananchi wenu kuwawakilisha hapa na sisi ni kazi yetu kuhakikisha mnapata hiyo fursa ya kuyasema yale ambayo wananchi wamewatuma myawakilishe kwa Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.30 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 3 Juni, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*